**Monasteri ya Utatu Mutakatifu**
**Oropos ya njimbo Atiki**
**Grekia**

# ZAWADI YA WENYE ZAWADI

**KITABU YA MBILI**

**CENTRE DE LA MISSION ORTODOKSE**
**KOLWEZI KONGO**
**2000**

# ZAWADI YA MAONO

Zawadi ya maono ni zawadi moja wa ajabu na kabaila. Lakini ni kabisa wa hatari, kwa sababu watu wingi walijivuna juu yao na wengine walipotesha akili yao, kwani waliona maono wa uwongo. Kwa hivi hii zawadi haionekane katikati ya Watakatifu wingi. Inaonekana paka kwa wale walichunga unyenyekevu mingi.

Maono haina alama wa daima inaituonyesha juu ya utakaso ya mtu moja. Katika onekano yao tunaweza kuitengeneza na vipande vipende, hivi:

1. Maono ile inaonekana katika ndoto.
2. Wakati ya sala, na
3. Ya kila wakati.

Lakini namna ya ono ukubwa ni ile Mungu alisuburia pamoja na Nabii Musa ni kusema kinywa na kinywa.

Hile maono inatokea ya Mungu inaikalaka na maonmyesha hii:

a). Inafanyika katika mapenzi ya Mungu na hapana na mapenzi ya mutu. Mtu moja munyenyekevu kwa ajili ya unyenyekevu yake hasiombe kuona maono.

b). Inaonekana bila makelele na paka ya ukimya. Hii maono inaishituka hule mutu, lakini ilimupatia amani na ilimujaza furaha, nguvu na mapendo.

c) Inazala matakio nguvu na utamu juu ya kupanda mwenendo ya uzima takatifu.

Watakatifu wetu wanatwaambia ni wa nani maonyesho ya hile maono inatoka ya shetani. Wanasema hivi:

a) Maono iliyetokea ya shetani wanaleta tetemeko, woga na makelele.
b) Wanazala mu nafsi jivuno, chuki, uzaifu na woga.
c) Wanashusha mapendo ya uzima takatifu na maendeleo ya kupata mafazila ya Kristu.

Akili ya mutu iko na nguvu kuzalisha teke-teke ma picha ndani yake. Lakini, wakati mutu atafanya picha ndani ya akili yake juu ya kuonyesha uso ya Mungu, mara moja anamupatia kwa shetani uhuru kwa kumutupa ku mutoni ya majivuno. Kwa hivi tukona maono unatoka ya shetani. Shetani iko na nguvu kuonekana sawa malaika ya nuru na anaharabisha akili ya watu wasiyosopoka mu uzima yao. Hivi tunaona watu waminifu, wenye wanatwelejea maono na ma ndoto yao na maonekano ya «watakatifu na malaika», lakini hii ma picha yao haina ya kweli; ni ma uso mbali-mbali ya shetani. Hii maono tunaweza kuona katikati ya mafumu na watu wengine, wenye wanaonekana sawa waaminifu wa kweli, lakini shetani aliharabisha akili yao na matendo ya shetani hawa watu wanaiona sawa matendo ya Mungu, bila kuuliza ma padri ya roho yao.

Kwa hivi na Watakatifu wetu wanatushauria kusopoka mingi sisi kama tunaona maono na ma ndoto, kwa sababu hatujue kama hii inatoka ya Mungu ao ya shetani? Pa hii fasi sisi tunapashw akuuliza mapadri ya roho yetu ao askofu yetu. Shetani eko muovu na mukalamushi na iko namna kuharabisha akili yetu na haipashwe sisi kusadiki akili yetu na kusema ya kama hii ndoto ao ono fulani inatoka paka ya Mungu.

Wale watu wanapenda kuwaambia maono na ufunuo yao mbele ya watu wengine, bila akili na uwazo ya kama iko namna shetani awalanda sana, hii ni onyesho ya upumbafu yao.

Mtakaitfu Pakhomio anatwaambia: «Ni mambo ya sikitiko kwangu, kama nitaacha kazi ya kukumbuka zambi yangu na kutubu na kisha ninatafuta kuona maono.. . Unataka kuona ono moja kubwa? Ona mtu moja bikira na munyenyekevu! Hii ono ni kupita ukubwa kwa sababu unaona Mungu muzima ya kuingia na kuikaa ndani ya mtu moja wa hii dunia».

Mtakatifu Ipolitos aksofu ya Roma wa zamani aliaandika jambo moja ya askofu moja, aliyekuwa mtu mwaminifu, lakini alisopoka sana hile ma ndoto aliona mu musingizi yake. Usiku moja aliona ndoto moja ya kama kisha mwaka moja itafanyika Siku ya Uhukumu wa mwisho!

Taifa yake ilianza kulia na kuomboleza. Kwa ajili ya hii sikitiko yake alisimamisha kazi ma shamba yake! Wakati ilitimizwa hile mwaka na Siku ya uhukumu wa mwisho haikufike, ilionekana tendo ya kulanda ya hule askofu na waaminifu wake walishituka, waliteshwa na walizunguluka hile mwaska kuomba saidio kwa sababu hakuna kintu ya kula yao!

Vile na watu wengine hii wakati yetu wanasema ya kama wanaona maono ya Mungu na wanaleta woga na tetemeko kwa watu wengine.

Siku moja alionekana shetani na uso ya Bwana Yesu Kristu kwa mtakatifu moja na alimwaambia: «Mini ni Yesu Kristu.. . ». Mtakatifu mutawa alimujibu: «Mimi misipende kuona pa hii uzima Yesu Kristu, lakini ninapenda kumuona mu uzima wa milele». Na shetani alikimbia.

Shetani alionekana na uso ya malaika Gabrieli kwa mutawa moja, lakini mutawea alimujibu: «Sopoka, iko namna kufanya kosa ufike kwangu. Mimi, kwani ninaishi ndani ya zambi yangu, hakuna namna kuwa stahili kuona malaika ya Mungu.. . ».

Mtakatifu Diadokhos askofu ya Fotiki wa Albania anatufundisha hivi: «Ni onyesho ya akili mingi na safi, kama sisi tunakataa kupokelea hata ono moja.. Na, kama, kwa mfano Mungu atatutuma kwa sisi ono yake moja na sisi tutaikataa kuipokea, Mungu hasitasirika, kwani anajua ya kama tunakombana kuchunga akili na roho yetu safi na katika unyenyekevu toka mitego ya shetani».

Ninyi watu wanapokelea maono, bila kusopoka na kuuliza mapadri ya roho yao na wanasema maono yao na mbele ya watu wengine, hawa watu walipotesha akili yao kwa ajili ya majivuno yao na shetani anawalanda.

## Sala na kazi..

Wakati Antonio mkubwa alikuwa tena kijana na ku mwanzo mu uzima ya utawa, alianguka mu uzaifu. Alikombana yeye mwenyewe ndani ya jangwa, bila mwongozi na mawazo yake walimuletea ngiza na woga. Lakini hasikupoteshe kitumaini yake mbele ya Mungu. Alipika magoti mbele yake na aliomba Kwake hivi:

-Ee Bwana, ninataka kuokolewa, lakini mawazo yangu wananiuzi sana. Misi na mwingine, ee Bwana wangu, juu ya anifundishe kufanya nini. Na wewe usiniache.

Sala ilimupatia utulivu! Mara moja alibeba na jibu hile aliongojea. Alisimama, aliona pa fasi ya kona ya chumba yake Antonio moja mwingine, aliyeikaa pa kiti na alifanya ma kitunga yake! Alisimama ya kushituka na alimuangalia, bila kusema sauti. Kisha hule mwingine Antonio alisimamisha kazi yake, alinyanyua mikono yake mbinguni na alianza mara ingine sala mbele ya Mungu. Ku mwisho alipindula kichwa yake kwake na alimwaambia:

-Fanya na weye hivi na utaokolewa.

Vile alisema na alikimbia hule Andonio mwingine.

Hile saa alisikia Mutawa Antonio ya kama Mungu alimutuma kwake malaika yake juu ya kumufundisha. Alikamata nguvu na alianza kutumika hivi na uvumilia na mapendo afanbye kazi ya mwili na kazi ya roho.

## Ma Adui na marafiki

Wakati Mtakatifu Mutawa Musa wa Ethiopia alikuwa kijana alijikombana mingi ku matakio ya mwili. Basi, alienda na makelele mu akili yake kwa baba ya roho mtak. Isidoros.

Padri ya roho Isidoros alimusikia na mapendo na alimushauria nzuri na alimuwaambia arudie ku mulango yake. Kwani yeye aliogopa ya kama, kama atarudia kwake, itaanza kumukombanisha mara ingine majaribu ya zambi ya mwili, mtakatifu Isidoros alimukamata na mukono, alimupeleka ndani ya nyumba (chumba) moja kidogo.

-Angalia hapa, alimwaambia, na alimuonyesha fasi ya mangaribi.

Hile saa Mutawa Musa aliona kundi moja mzima ya askari (walikuwa ma roho maovu ya shetani) na walikuwa tayari ya nvita na alishituka sana.

-Angalia sasa pa fasi ya mashariki, alimuwaambia padri ya roho yake Isidoros.

Ilikuwa kundi ya malaika ya Mungu na walikuwa tayari kukombana kundi ya ma shetani.

-Hawa, alimwaambia padri Isidoros, aliwatuma Mungu kwa kumusaidia kula mushindani. Unaona ya kama marafiki yetu ni kupita wingi ya ma adui wetu.

Mutawa Musa alimushukuru Mungu katika roho yake kwa ajili ya hii ufunuo Yake; alikamata nguvu, alirudia kwake kuendelesha ushindani yake.

## Maongozi ya malaika

Uzima takatifu ya mutawa mtakatifu Pakhomios ilizambalala ma fasi yote na ndugu wingi walikuja kwake kumfwata uzima yake katika shauria yake.

Huyu mukuona ya kama alipotesha ukimya upendwa wake na alianza kutumika juu ya uzima na wokovu ya wa ndugu wake, alijiuliza maungo yake ni nani mapenzi ya Mungu.

Hile saa alionekana malaika moja na alimusema:

-Ee Pakhomio, mapenzi ya Mungu ni kusaidia wa ndugu yako!

Kisha alimushauria namna gani ataongoza kundi ya wafwasi wandugu wake. Alimwaambia hivi: «Chakula ya wa ndugu wote itakuwa umoja. Kati ya tumbo yao watavaa musipi na pa kichwa yao kofya na mbele yake msalaba nyekundu. Utawachanisha na vipande makumi mbili na inne (24), katika tabia yao. Wale watu wanakuja kupima juu ya kufata hii uzima utawachunga wakati ya miaka tatu. Wa ndugu, hile wakati wanakula pa meza, watavaa kofya na yule yake kukuli (Nguo umeushi) juu ya hapana kuona moja mwingine na wanasuburia».

Hii ma sauti na ingine alimupatia malaika kwa mtakatifu Pakhomios na vile yeye aliongoza kundi ya Watawa wake katika mapenzi ya Mungu.

## Kipimo ya margonio

Wakati moja, mutawa mt. Theodoros, musaidizi ya mt. Pakhomios, aliingia ndani ya mutubwi moja kutabuka mtoni Nilos wa Misiri. Ndani ya mutubwi walikuwa na watawa wengine wasiyowafahamu. Moja alianza kumutukuza na masemo mazuri kwa mutawa mwingine. Alimusema hivi:

-Huyu mutawa ni mwenye heri!

Mwingine alimujibu: Juu ya ninyi unamutukuza? Bado kufika mu kipimo ya ma fazila ya margonio (Margonio iliitwa kitunga moja hile wakati na ye waliitumia sawa kipimo yao).

-Ni nini hii kipimo?

-Tazama, alikuwa mulimaji moja mugumu sana. Pamoja naye hakuna namna kuikaa na kutumika mtu mwingine. Mtu moja alikuja kwake wakati fulani na alimwaambia:

-Ninataka kutumika na weye.

-Muzuri, a;imujibu hule mtu.

Hile siku ya kumwangisha maji mu shamba yake, mulimaji alimwaambia:

-Twende hii usiku kukokota maji ku mutoni ya kumwangisha ma shamba yangu na hapana siku ya muchana.

-Alimujibu mutumishi yake: Aa, hii kazi ni nzuri, kwa sababu hawataweze wakunywa maji siku ya muchana hata watu, hata ma nyama, hata nyama ingine ku kijito yetu.

Wakati ilikuja wakati ya kulima ma shamba yake mulimaji alisema kwa mutumishi yake:

Ahamba yetu tataweka mustari moja bego ya ngano, mustari ingine bego ya mahalaki na mustari ingine bego ya mwinji, na paka vile. Mutumishi alimujibu:

-Mu akili yako  inaikalaka hekima mingi, kwa sababu hivi, kama mayani yao itaota na itakomea, itakuwa muzuri kwa sababu itaonekana kundi moja na mayani na maua ya kuachana na watu na sisi tutafurahi sana.

Katikati ya mistari iliota na ilikomea nyasi ya bure. Mulimaji al;isema kwa mutumihsi wake:

-Sasa, mbele ya kutosha bego yake hile nyasi iliota katikati ya mistari, twende kuitosha.

-Mutumishi alimujibu:  Twende. Faida yetu itakuwa mingi juu yake. Ni mubichi na nzuri. Kisha mavuno ya hil;e nyasi mulimaji alimwambia kwa mutumishi yake amulete margonio. Alimwaambia mara ingine:  Sasa tutapima ngapi ni uzito hii nyasi na tutaipeleka ndani ya nyumba yetu. Mutumihsi alimujibu:

-Hii ulisema ni muzuri sana, kwa sababu tutaichunga nyasi.

Vile huyu mulimaji alimupima mutumishi yake na aliona ya kama alikuwa mutilivu sana, bila ubishano na ku mwisho alimuwaambia:

-Tangu leo usitakuwa mutumihsi yangu wa malipo, lakini mtoto na muriti wangu.

Basi, kama na huyu mutawa atafika pa hii cheo ya utii, bila ubishano, vile atakuwa mutawa mwenye heri.

-Ni nini maana ya hii mufano?  Alimuuliza mutawa wa kwanza.

-Ndivyo!  Mulimaji ni Mungu. Anaonekana mugumu, kwani anatwaambia kuchunga sisi msalaba yetu na kukata mapenzi yetu. Mutawa mtak. Pakhomios, padri mkubwa ya hule mutawa, alionyesha utii ya kila kazi na alikuwa mufazili mbele ya Mungu. Kama, na huyu ataonyesha utii, bila ubishano, paka vile ataweza kufurahisha Mungu.

Mtakatifu mutawa Theodoros alisikia wa ajabu hii mazungumuzo ya wenye safari yake. Kwa ajili ya hii mazungumuzo na roho yake ilikomea ya kufanya na huyu utii. Lakini, wakati alitoka inje ya mutubwi, hasikuwaone mara ingine. Sawa vile alimukikisha kisha saa kidogo mtakatifu Pakhomios, hawa walikuwa malaika wa wili, wenye Mungu aliwatuma juu ya kumusaidia na kumutulivu namna gani na yeye ataishi juu ya kupata wokovu wake..

## Rafiki ya Mashahidi Kleopatra

Wakati alikuwa mufalme ya ufalme ya Roma Maksimianos, alikufa na mateso mengi mu Misiri mtakatifu Uaros, aliyekuwa mkubwa wa askari ya kundi ya wa askari ya Roma. Alikuwa mukristu wa kweli. Walimubamba ndani ya buloko, hile wakati alikwenda pale juu ya kusaidia wakristiani wengine na sauti na shauria yake na aliwapatia na chakula. Ilikuja na mustari yake kwa kumwanga damu yake kwa mapendo ya Kristu. Pa hile fasi alikufa, alikuwa na mwaaminifu moja mwanamuke, jina yake Kleopatra. Huyu alikuwa balaka muke, mutajiri sana na alikuwa na mtoto mwanaume wake. Huyu mama aliangalia na uovu mingi hii mateso walimufanyisia kwa hule Mushahidi kijana, mwenye alisimama mzuri juu ya kuchunga imani yake kwa Kristu. Hile wakati mwili yake ilikuwa chini bila nafsi, mama Kleopatra aliwapatia makuta mengi kwa askari, wenye walimuua na alibeba mwili ya mushahidi Uaros. Alipeleka nyumbani yake na heshima mingi na alifanya maziko yake.

Kisha miaka kidogo, hile wakati alikuwa mfalme ya Konstantinopoli mufalme mukubwa Konstantinos na mafukuzo waliisha kusimama kupingana ya wakristtu, mama Kleopatra aliondoka Misiri na alirudia mu inchi yake, Palestina. Pamoja naye alibeba na mwili ya mt. Mushahidi Uaros sawa zahabu kubwa. Pa hile fasi ya inchi yake aliyenga kanisa kwa jina ya huyu Mushahidi na aliweka ndani ya hile kanisa mwili yake ndani ya sanduku moja wa zahabu.

Wakati iliisha majengo ya hile kanisa huyu mama aliita askofu na mapadri ya hii njimbo juu ya kufanya sala mu kanisa. Kisha Liturgia, alipokea watu wote mu nyumba yake na aliwapatia chakula. Huyu balaka muke pamoja na mtoto yake walisaidia kwa mapokeo watu wote, bila hile siku kukula hata kidogo chakula. Ilikuja usiku na nyumba ilikuwa mara ingine

wazi na huyu kijana, mtoto yake, kwani alikuwa na muchoko mingi, alienda mu chumba yake kupumuzika. Kisha saa kidogo aliingia ndani na mama yake amupatie chakula. Alikuwa na lakini kivukutu mingi pa mwili yake! Mama yake alimusaidia, pasipo kuwaza muchoko na njaa yake. Saa ilipita na kivukutu ilipanda mbaya na mbele ya kufika munganga, mtoto yake alikufa ndani ya mikono ya mama yake. Hule mama, kwa ajili ya hii mateso yake, alikuwa sawa mazimu. Alilamusha mwili ya mtoto yake na aliipeleka mu kanisa ya Mushahidi Uaros. Aliweka pa sanduku ya mwili ya Mushahidi na huyu alipika magoti mbele yake alianza kuomboleza na kulia sana. Alimukumbusha kwa Mushahidi hii kazi yote alifanya kwa ajili ya mapendo yake na sasa alimuwaambia na alimuombea kufufusha mtoto yake!

Kwa ajili ya sikitiko na maombolezo na kutosha machozi yake, alichoka na alilala mbele ya sanduku ya Mushahdi Uaros. Hile saa aliona ndoto moja muzuri na ilimuletea utulivu mu roho yake.

Mbele ya ma macho yake ilifunguliwa mbingu na katikati alionekana Mushahidi Uaros ndani ya mwangaza mingi na pempeni ya kichwa yake ilikuwa taji wa zahabu! . Alikuwa ya kukamata na mukono mtoto ya mama Kleopatra na huyu alivaa pa kichwa yake taji ya maua yoyote na kichwa yake ilikuwa muzuri sana.

-Ee Kleopatra, usinichukie kwa hii namna, bila shukrani, alimwamabia na sauti utamu Mushahidi Uaros. Unakumbuka mara ngapi ulipika magoti mbele ya mwili yangu na uliomba saidio ya mtoto yako? Hii zawadi kubwa mimi niliweza kumupatia ilikuwa hii utukufu sasa weye unaiona. Kama, kisha hii ono ya utukufu ya mtoto yako, wewe unapenda arudie mtoto yako kwako, huyu ni muhuru arudie kwako.

Alipindula kwa kijnana, alimuonyesha mama yake na alimuuliza:

-Rafiki wangu, kama unapenda, unaweza kuenda karibu ya mama yako.

Lakini huyu alianguka ndani ya mikono ya Mushahidi, kwani hasikupenda kuepuka mbali ya mikono yake. Kisha alipindula kidogo kichwa yake pa hile fasi alikuwa mama yake, na alimuwaambia:

-Ee mama wangu, unataka tena kunitoshaku hii utukufu yangu? Unataka nilete mimi toka hii uzima wa mielel mu uzima ya zambi ndani ya dunia yako? Simamisha mama ya kulia na kuwa tayari juu ya kunipokea na nikuta.

Utulivu mingi ilijaza roho ya hule mama, kisha hii ono wa ajabu huyu aliiona. Alizika mtoto yake ndani ya hii kanisa mupya na kisha alikabula uriti yake yote, alivaa manguo wa bure na alibakia karibu ya kaburi ya Mushahidi na mtoto wake. Alitumika mu kanisa sawa musaidizi yake miaka saba na kisha alikufa sawa mtakatifu.

## **Malipo ya uvumilia.**

Mutawa moja wa jangwa alibaki ndani ya nyumba moja ya jangwa, karibu 3 kilometre mbali ya chemchem pahali watawa wote walibeba maji yao. Viule, huyu kila siku ilikuwa lazima kutembea mbali juu ya kubeba maji yake. Siku moja kivukutu ilikuwa mingi zaidi na huyu alipotesha uvumilia yake.

-Aliwaza na akil;i yake: Juu ya nini ni lazima kuchoka hata mingi kila siku? Haina namna kuikaa hapa karibu ya chemchemu?

Hile waakti aliwaza hivi, alisikia ya kama mtu moja alitembea mukongo yake. Alipindula kiichwa yake na aliona kijana moja wa nuru sana.

-Nani uko weye? Alimuuliza na ajabu na kushituka.

-Mimi ni malaika ya Mungu. Alinituma juu ya kuhesabu ngapi mwendo unafanya kila siku juu ya nikupatie mimi malipo ya uvumilie yako, alimujibu huyu malaika na alikimbia mara moja.

Hii ma sauti ya malaiuka walimupatia kwa hule mutawa wa jangwa nguvu mingi na hasikujenga nyumba karibu ya chemchem, lakini kupita mbali juu ya kutembea wakati kuliko mingi.

## Ukimya na ukaribisho

Mtakatifu mkubwa Arsenios, katika amri takaitfu, aliacha nyumba ya mfalme ya muji Konstantinopoli na alienda mu shkiti (Mukini) ya Nitria ya inchi Misri. Pale alifanyikamupendwa mkubwa ya ukimywa na unyamasha.

Wakati moja, mugeni moja alitaka amutembelea kwake. Basi, alienda mu kanisa ya Skiti na aliomba amupeleke kwake. Wakati walikokola mulango ya Arsenios, huyu aliwafungula mara moja, aliwapokea na furaha na aliwabusu na mapendo ya Kristu. Kisha waliikaa wote wa tatu na unyamasha. Hawakuseme hata sauti moja! Vile saa ilipita mingi na mwongozi alisema kwa mugeni:

-Mimi, ndugu, nitarudia kwangu.

-Nitakufata na mimi, alimujibu hulke mugeni. Juu ya nini nitaikaa hapa, bila faida?

Hile wakati walitembea aliomba hule mugeno mwongozi yake amupeleke kwa mutawa wa jangwa Musa, wa inchi Ethiopia, aliyekuwa zamani munyanganyi. Mutawa mt. Musa aliwapokelea na furaha na alisuburia nawao fundisho ya roho. Mugeni alifurahi sana! Kwa kutoka mwongozi alimuuliza huyu mugeni:

-Ni nani katikati ya hawa wa wili ni mkubwa mu fazila?

-Kweli, huyu Musa, aliyekutukaribisha na alitufurahisha roho yetu, alimujibu hule mugeni.

Hii jambo aliisikia muzee moja mutawa mkubwa na hasikujue atatukuza nini: Unyamasha kubwa ya hule mutawa wa kwanza (Arsenios) ao zungumuzo wa roho ya mutawa wa wili? Basi, aliomba kwa Mungu amuonyeshe mapenzi na furaha yake.

Usiku aliona mu usingizi yake ndoto moja ya kama alikuwa pa ngabo moja ya mutoni Nilos wa inchio Misiri, pahali walitembea ma chombo wa wili. Ndani ya chombo moja alikuwa mutawa Arsenios. Alitembeea chombo na ukimywa na kujaza katika utulivu na mwangaza ya Roho Mtakatifu. Mu chombo ingine alisafiri mutawa Musa. Walimusindikiza na malaika nyingi na walimupatia kula asali.

Hile saa huyu muzee mutawa alisikia ya kama watawa wa wili walikuwa wenye stahili mbele ya Mungu. Lakini unyamasha ya Arsenios ilikuwa kuliko kubwa mbele ya Mungu ku ukaribisho ya mutawa Musa. Katika hii ndoto, muytawa Musa, walimupatia kula malaika, lakini Roho Mtakaitfu alisimama ndani ya unyamasha ya mtakatifu Arsenios.

## Ugonjwa ya mutawa moja wa jangwa

Asubui moja alienda Zakharias, mtoto ya roho ya mutawa muzee Siluanos nyumbani yake juu ya kuomba baraka kufanya kazi moja. Alikokola mulango, na kwa sababu hasikubeba jibu ya baba ya roho yake, alifungula kidogo mulango kuangalia kama yeye ni ndani na alifanya nini. Alimuona padri ya roho yake pa hali kimungu. Aliisha kupandisha mikono yake mbinguni! Kisha huyu kijana aliondoka bila kumuuzi. Wakati alienda mara ingine kati ya muchana, alimuona padri ya roho yake paka pa hile fasi. Vile alifanya na mangaribi na alimuona kufanya sala. Usiku alienda mara ingine na alipata padri ya roho yake asimame pa kiti ya aliikaa na mikono yake pa kilari na aliwaza.

-Zakharias, mtoto ya roho yake, alimujibu, mabo gani ukona yo, padri wangu?

-Nikona ugonjwa kidogo. Lakini haina mambo. Usisikitike.

Lakini Zakharias, hasikusadiki jibu yake. Alipika magoti mbele yake na alimuomba:

-Misitatoke ya huku, padri wangu, mpaka utaniambia hii jambo ya ajabu uliiona.

Hile saa yeye, bila kuweza kukataa, alimwaambia ya kama akili yake ilikuwa na sala na aliona na akili yake utukufu ya Mungu!

## Mutawa moja na musaidizi mwanamuke ya Kanisa

Musaidizi ya Kanisa kubwa ya Konstantinopoli, jina lake Vasilina, alikuja mu Yerusalema pamoja na mwipwa yake, aliyekuwa mkubwa wa askari, lakini alifata kanisa ya uwongo. Vasilina alikombana kumugeuza akili na mafundisho yake, lakini hakuna namna. Alianza kutembelea kwa watu watakatifu juu ya kufanya sala ya mwipwa yake.

Wakati alisikia ya kama askofu Yoano wa jangwa alikuwa mtakatifu na aliishi sawa mutawa mupole mu monasteri ya mt. Savvas, jangwani ya Palestini, alienda kwake kwa kumuomba baraka na sala yake.

Lakini, kwa sababu ilikatazwa mwanamuke moja aingie ndani ya monasteri ya watawa wanaume, vile ilikuwa desturi yake, aliwaza kuvaa manguo sawa mwanaume na vile atamukuta hule mutawa askofu juu ya amwaambie mambo yake.

Askofu  mtakatifu Yoano Mungu alipata tangazo toka Mungu juu ya mawazo ya hule mwanamuke na alimwaambia hivi:

-Sikia muzuri, kama unapenda kuja ndani ya monasteri yangu, hautaweze kunikuta!  Basi, usichoke na fanya uvumilia. Pa hile fasi weye unaikaa mimi nitafika mu ndoto yako, nitasikia mambo yako na hii sauti Mungu atanishauria, nitakuwaambia.

Huyu mwanamuke alisikia na imani hii ma sauti ya askofu Yoano na alistahiliwa kuona ono moja wa ajabu. Mutawa alikuja mu ndoto yake mukusema:

-Tazama, basi, Mungu alinituma kwako. Uniseme, unataka nini.

Na huyu mama alimwaambia kila mambo yake na alisikia na kila jibu. Kisha alilamuka na alimushukuru Mungu.

Kisha waakti kidogo alikuta mtoto ya roho ya mtakatifu Theodosios na alimuuliza namna gani ni kipimo na uso na mwili ya askofu Yoano. Mtoto ya roho alimuelejea hivi na hivi na huyu mama alifurahi, kwa sababu alimuona na hii namna mtakaitfu askofu Yoano.

## Mama ya mutawa  mt. Alipios

Mama ya mutawa mt. Alipios aliyeitwa Stilitis, kwani aliishi pa nguzo moja, alikuwa na fazila munene ya mapendo. Huyu mama alipenda kuikaa karibu ya mtoto yake, mu jangwa kusudi amusaidie kwa ushindani ya roho yake. Alikataa ma furaha na mapumziko ya hii dunia, aliweka hema moja karibu ya nguzo (colone)ya mtoto wake na alitumika na mikono yake juu kupata chakula yake na mtoto yake.

Mtakatifu mtoto yake Alipios alimwaambia mara nyingi afwate uzima ya utawa, lakini huyu asikuichike. Alitaka kuwa paka musaidizi na musimamizi yake mbele ya kila mateso na mambo ya mtoto yake. Wakati moja, lakini alipokea wakati ya musingizi yake, ono moja takatifu na kisha kwa ajili ya hii ono, alikamata mpango afanyike mutawa.

Alisikia mu ndoto yake kundi moja ya wanawake watakatifu, wenye waliimba wimbo watamu na matakatifu kwa Bwana na Mfalme wao. Alifuraha hata mingi na alipenda kuingia ndani ya hile nyumba, pahali ilikuwa kundi ya waimbaji wanawake kusudi aimbe na yeye pamoja nao mbele ya Bwana. Lakini mtu moja, aliyekuwa pa mlango na alikuwa mujukumu nani ataingia ndani na nani aipashwe kuingia, alimuwambia:

-Hautaingie ndani!  Hautaweze kuchanga pamoja na hawa wanawake, kwa sababu weye usiwe mutawa.

Huyu mama ya mt. Alipios alisikia haya mingi. Alishituka na alilamuka. Kisha wakati kidogo alimuwaambia mtoto yake amufanyisie sala juu ya kuwa na yeye mutawa. Kisha sala ya utawa nafsi ya hule mama ilijaza na utulivu na furaha, kwani alivaa Alama ya uzima ya watawa.

## Mkubwa ya monasteri moja na mupisi

Ndani ya monasteri moja aliishi mutawa moja aliyeitwa Efrosinos. Alitumika sawa mupisi ndani ya hile monasteri. Kila siku alikuwa ndani ya upisi, ndani ya moto na ma chungu na simoko na hata mutu moja hasipende kumuona. Vile, aliishi na unyenyekevu na bila sifa na alifuchika ma fazila yake. Tena, na watawa vijana, mukuona huyu ndani ya simoko, walimuchekelea na walimuzarau.

Hule mupisi, lakini, alivumilia uzito kazi yake na kila uzarau na machekeleo ya wa ndugu wengine wake. Hasikuseme sauti moja na hasikuhukumu mtu mwingine.

Mkubwa baba ya hile monasteri alikuwa mtu mufazili na alisimama na uwezo mbele ya Mungu. Basi, alimuomba siku moja Mungu amufunue katikati ya watoto ya roho yake nani alikuwa mkubwa mu fazila na kuliko karibu Kwake.

Usiku moja aliona ono moja kitakatifu na aliona ya kama alikuwa ndani ya shamba moja na ndani ilikuwa miti vizuri na matunda matamu. Chini ya hile miti alitembea mutoni moja na maji safi. Ono ya hile shamba ilikuwa wa ajabu. Huyu padri ya roho mkubwa alimushukuru Mungu kwani na yeye alikuwa ndani ya hii fasi wa ajabu.

Lakini alitakia kupima na matunda wa ajabu ya hile shamba. Alipima kukata matunda filani, lakini asikuweze. Wakati alitaka kukata matunda moja mayani yao pamoja na matunda walinyanyua yulu kidogo-kidogo!  Alikombana mara mingi bila kuweza kukamata mayani na matunda yake. Hile saa aliona mupisi ya monasteri yake Efrosinos, aliyekuwa pale na alitembea ndani ya hii shamba na alikula hii matunda na alifurahi sana. Mayani walinamisha mbele yake na walimutoa matunda yao.

Padri mkubwa yake alishituka na alipaza sauti aseme:

-Mtoto wangu Efrosinos, nani alikuletea huku na alifungula mlango kuingia hapa?

Na huyu katika uso wa furaha, alimujibu:

-Ee Muzee na baba wangu, Mungu mpenda wanadamu alinipatia hii shamba na alinipatia baraka Yake kuingia ndani na nifurahi.

-Unaweza unipatie na mimi tunda moja?

-Beba, ngapi unataka.

-Mtoto wangu, misiweze. Nilipima kukata mara nyingi, lakini misikuweze kukata hata tunda moja.

Hile saa mtakatifu mupisi Efrosinos alikaribia muti moja, alikata matunda tatu na alimupatia kwake.

Wakati padri ya roho yake alikamata hii matunda pa mikono yake, alilamuka na ono yake iliisha. Lakini jambo ingine ya ajabu ilimushituka. Wakati alilamuka aliona ya kama alichunga pa mikono yake hii matunda wa tatu!

Alihamuru mutawa moja apike kengele juu ya Ibada ya asubui. Ku mwisho ya Liturgia, waakti alivaa tena nguo takatifu yake, alituma tangazo watawa wote kuogojea ndani ya kanisa na wataita na mupisi yao Efrosinos. Hile saa huyu Efrosinos aliisha kwenda kwa pisi juu ya kutayasisha chakula yao. mbele ya saa ya kula.

Walienda watawa kwa pisi walimubeba Efrosinos na wal;imupeleka mbele ya padri mkubwa yao. Uso yake ilikuwa na simoko kwa ajili ya moto, tena mikono na manguo yake. Padri ya roho mkubwa alimuuliza:

-Mtoto wangu Efrosinos, ulikuwa wapi hii usiku?

Hule mupisi, alinamisha kichwa yake na hasikuseme kintu. Lakini, kwa sababu padri ya roho alimuuliza mara nyingi, alimujibu na unyenyekevu:

-Usijue, ee padri wangu, sisi wa wili tulikuwa wapi?

Hile saa padri ya roho alitosha hii matunda tatu ya mfuko yake na alimuuliza:

-Unajua hii matunda inatokea wapi?

-Ndivyo, ee padri. Ulinihamuru na mimi nilikuletea.

-Mtoto wangu, Efrosinos, uko mwenye heri kwani ulistahiliwa kupata hii ma furaha mtakatifu. Omba kwa Mungu juu ya mimi mwenye zambi.

Mara moja padri mkubwa yao alielejea mbele ya watoto wa roho yake hii ono takatifu aliona usiku. Kisha alipika magoti mbele ya mtoto yake, mupisi Efrosinos, lakini huyu mtakatifu mupisi alilia kwa ajili ya hii haya alisikia. Kisha padri mkubwa alikata vipande-vipande hii matunda na aliikabula kwa watoto wake wote.

Mtakatifu mutawa Efrosinos mpaka hile saa alivumilia kila uzarau ya wa ndugu wake, lakini tangu hile saa hasikuweze kuvumilia utukufu na sauti wa ajabu ya ndugu wake. Alikimbia kwa siri na hata mutawa moja hasikumuone mara ingine, kwani alienda kuikaa mu fasi ingine bila kumuona na kujua anaenda wapi.

## Kurudia deni.. .

Mtakatifu mutawa Yoano wa Savaitis (toka Monasteri ya mt. Savas, mu Palestini) alienda wakati moja aingie ndani ya monasteri moja iliyekuwa mu fasi Pontos. Uzima pale ya watawa ilikuwa ukali na ugumu sana. Usiku hile ya kwanza alipumzika pale, aliona ndoto moja ya kama watu filani walimuomba miya moja makuta ya zahabu. Alilamuka na alifafanusha ndoto na alisema kwa maungo yake:

-Sawa unaona na weye inapashwa kurudisha deni moja munene!

Basi, huyu mutawa alitimiza ndani ya hile monasteri miaka tatu. Aliitii padri mkubwa yake na alivumilia kila taabu na uzarau ya watawa wengine. Aliona mara ingine mu ndoto yake ya kama mtu moja alimupatia karatasi moja na iliandikwa pa hii karatasi ya kama alirudisha makuta ya zahabu kumi. Wakati alilamuka alisikia maelejeo ya ndoto yake na alisema mbele ya maungo yake:

-Paka kumi makuta? Wakati gani, basi, nitaweza kurudisha deni yangu yote? Ninalazimisha, basi, kutumika na kuliko nguvu na uvumilia na unyenyekevu!

Basi, tangu hile wakati alianza kuonyesha tabia yake sawa yeye alikuwa mazimu, lakini bila kutoka ya ma kazi yake yote. Na mapadri yote, kwani walimuona atembee na aonekane sawa mazimu, walimwaambia afanye ma kazi kuliko magumu na uzito mingi.

Basi, kwani alivumilia hii ushindani yake ya roho tena miaka kumi na tatu, aliona mara ingine mu ndoto yake hawa watu, wenye walikuja ku mwanzo na waliandika ya kama aliisha kuwarudisha deni yake yote!

## Binti wa kwanza ya mufalme

Mtakatifu askofu ya Aleksandria wa Misiri jina yake Yoano (makubusho yake mu Kanisa yetu ni 11 Mwezi Kumi na moja) aliona ono moja wa ajabu na ilimusaidia mu uzima yake.

Wakati moja, anatwaambia huyu askofu, wakati nilikuwa na kipimo miaka kumi na tano, mu inchi yangu Kisanga Kipros, usiku moja niliona katika musingizi yangu, binti moja na uso yake muzuri kabisa na wa mwangaza! Kichwa yake ilipambwa na mayani ya miti Mizeituni. Huyu Binti alitembea pa pepo karibu yangu, alinipika kidogo pa mabeka yangu na mimi nililamuka na ushituko. Niliona nini! Alikuwa kweli mbele yangu binti moja muzuri sana. Nilisikia ya kama huyu Binti hasikukuwe mwanamuke. Nilifanya alama ya msalaba na nilimuuliza:

-Nani uko weye na juu ya nini ulikuja kwangu hii saa?

-Hule alicheka. Uso yake upole ilijaza na mwangaza. Aliniangalia na mapendo na alinijibu:

-Mimi ni binti wa kwanza ya Mfalme mkubwa.

Wakati nilisikia hii ma sauti yake, mara moja nilianguka chini na nilibusu miguu yake. Huyu aliendelea:

-Kama utanipokea na utanibeba sawa rafiki yako daima mu uzima yako, mimi nitakusimamisha mbele ya Mufalme mkubwa na nitakupatia mapendo na saidio yangu juu ya kuwa wewe rafiki ya Hule Mufalme! Hata moja hana na uwezo na utukufu sawa mimi mbele

Yake. Inenea poka kuwaza ya kama mimi nilimwaambia kuonyesha mapendo hata mingi mbele ya watu wote. Mimi nilikuwa sababu kusudi ashuke Yeye duniani na kuwa mutu kwa kuokoa uzazi ubinadamu.

Wakati alisema hii ma sauti yake, alikimbia mara moja. Wakati mimi nilisikia kwa ajili ya hii ono wa ajabu, nilikombana kufafanusha ni nini maana ya hii ono. Faida gani iko juu ya uzima na wokovu yangu, hii ono? Hile saa nilisikia ya kama huyu binti aliyekuwa na taji pa kichwa yake na mayani ya mizeituni, alikuwa huruma. Kwa sababu, juu ya nini Bwana Yesu Kristu alikuja duniani, paka kwa ajili ya wema na huruma Yake?

## Mwito kwa uzima ya upumbafu

Mbele ya mwanzo ya ushindani ya roho yake, mutawa Andreas aliyekuwa mazimu katika Kristu, aliona mu ndoto yake ya kama alikuwa katikati ya kiwanja moja. Pale kambo moja walisimama hawa walivaa manguo maeupe, lakini ngambo ingine pa fasi ya kushoto walikuwa hawa wavaa manguo maeushi. Hawa wenye walivaa manguo maeushi walikuwa na katikati yao na mtu moja kupita mkubwa. Walisemaka kwa wale walikuwa ngambo ingine:

-Nana anataka kukombana naye? Hata moja ya wakati mingi hasikuweze kumushinda. Huyu ni mkubwa ya shetani!

Hile saa kundi ya mkubwa ya shetani walimutukuza na ma sauti nyingi, mtawa Andreas aliikaa pale na alisikia, lakini wale wa manguo maeupe walishituka na hawakuweze kufanya kintu ao kusema sauti moja. Mara moja alionekana katikati yao kijana moja muzuri sana ku uso yake, aliyeshuka hile saa toka mbingu na alichunga ma taji tatu pa mikono yake. Taji ya kwanza ilikuwa na mapambo ya zahabu na maimbwe ya kuachana, taji wa mbili ilipambwa na maimbwe ingine, lakini taji wa tatu ilikuwa na maua maekunda na maua ingine ya paradizo. Ilitosha na harufu nzuri sana na hakuna namna kusema mtu moja ya hii dunia.

Mtakatifu Andreas aliangalia hii ma taji na ajabu na aliongojea nani ataenda kukamata taji moja. Alimukaribia, basi, hule kijana wa mwangaza na alimuuliza:

-Kwa jina ya Kristu, uniambie, ngapi unauzisha hii ma taji? Misina na makuta ya kuinunua. Lakini nitaenda kwa mkubwa yangu na huyu atakupatia hii bei ya zahabu, weye utaomba.

Huyu kijana alicheka na alimwaambia:

-Ee Mupendwa wangu, unisadiki mimi, ya kama, kama utaniletea zahabu yote ya dunia mzima, hautaweza kubebe hata ua moja ya hii ma taji, kwa sababu hii ma taji wanabeba na wanavaa paka hawa watu wanakombana wale watu wenye meushi na wanawashinda.

Mukusikia sauti yake mutawa Andreas alikamata nguvu na alisema:

-Unisadiki, bwana wangu, nitafanya sawa vile uliniambia! Paka ninataka unifundishe mafundi yake yote juu ya kumukombanisha bila woga!

-Hawa watu meushi, alisema huyu kijana, hana na nguvu na wanaogopa sana. Usiogope kipimo urefu ya mwili yao. Hakuna nguvu kwao na wanafanana sawa mayani ya kufubala na kukauka.

Mutawa Andreas alikamata nguvu. Malaika ya Mungu alimufundisha namna gani atamukombanisha hule shetani. Ku mwisho alimwaambia pa maiskio yake:

-Kama yeye atakukamata na mikono yake na atataka akutupe chini, weye, fanya pa uso yake alama ya Msalaba na mara moja utasikia uwezo ya Mungu.

Basi, huyu mwenye heri Andreas aliondoka afanye bugomvi kupingana na shetani. Alikuja katikati ngambo moja mbele ya shetani na alimwita hivi nguvu:

-Kuja, ee mueushi, wa bure, musiyestahili! Kuja; Tutakombana pamoja!

Hule, wakati alimusikia, alitembea mbio mbele yake na majivuno mingi. Alimukamata Andreas na alimupindula pa pepo mara mingi. Wenye meushi walifurahi na walipika mikono, lakini wenye meupe walitaabu na walisikitika. Walizania ya kama hule shetani atamutupa chini

Andrea na atamuua. Lakini Andreas hile saa mubaya, alimukamata na alama ya musalaba na alimutupa chini!  Vijana wenye meupe walifurahi kabisa. Walimukamata Andreas pa mikono yao, walimunyanyua yulu, walimubusu, walimupakaa na manukato, lakini ma shetani nyingi walisikia sikitiko na walikimbia na haya mingi. Hile saa huyu kijana mutukufu alimukaribia Andreas, alimupatia hii ma taji, alimubusu na alimwaambia:

-Tangu hii saa utakuwa rafiki na ndugu yangu. Endelea hii ushindani muzuri. Kuwa tangu leo kwa ajili yangu mazimu na mimi nitakupatia bitu vyote vitakatifu mu ufalme wangu.

Wakati alilamuka huyu mwenye heri Andreas, alishangaa kwa ajili ya hii jambo yote aliona. Alisikia ya kama hii ono ilikuwa mwito ya Mungu kwa kufata uzima yake sawa mazimu katika Kristu. Basi, toka siku ingine alianza kudanganya na kuonekana ya kama alikuwa mazimu juu ya kuchekelea shetani.

## Mufuniko Takatifu

Mu Kanisa ya Vlahernon ya muji Konstantinopoli ilikuwa ndani nguo, kitambala na kipande ya musipi ya Mzazi-Mungu Bikira Maria. Usiku moja pale ilikuwa sala ya usiku na Mt. Andreas alienda pale pamoja na mtoto ya roho yake Epifanios.

Katikati ya usiku aliona mt. Andreas Mzazi-Mungu Maria atembee kutoka milango ya kanisa ku Altari takaitfu. Alionekana murefu sana na walimufata kundi ya malaika na Watakatifu. malaika wengine walitembea mbele yake na waliimba wimbo muzuri na wengien walimufata.

Wakati Mama Mzazi-Mungu alikaribia Meza takatrifu, alisema mt. Andreas kwa mtoto ya roho yake:

-Ee Epifanios, unaona Mama na Malkia ya dunia muzima?

-Ndivyo, padri wangu, ninamuona, alimujibu kijana.

Hile saa Mzazi- Mungu aliisha kupika magoti yake na alifanya sala ya saa  mingi. Alimuomba Mwana wake wa pekee aokoe dunia na alinawa uso yake na machozi yake. Kisha sala yake, aliingia mu mazabahu (Altari takatifu), pahali aliomba juu ya wale walikuwa ndani ya kanisa.

Wakati aliisha maombi yake, alitosha ya kichwa Kitambaa yake wa nuru na aliizambalala sawa mufuniko yulu pa vichwa vyote ya wale waaminifu walikuwa ndani. Vile waliiona hawa wa wili ya saa mingi na ilitoka nuru takatifu ya hii Mufuniko. Hile saa Mufuniko ilikuwa yulu ya vichwa ya hawa waaminifu na Mzazi-Mungi alionekana. Wakati yeye alipanda mbinguni, an Hii Mufuniko takatifu ilipanda yulu na ilikimbia.

Hii ono takatifu aliona kijana Epifanios Kanisa yertu Orhodokse inashangilia kila mwaka mu tarehe 1 ao 28 Mwezi ya Kumi.

## Ulinzi ya paradizo

Mu muji Konstantinopoli pahali aliishi mtakatifu mutawa Andreas, mazimu katika Kristu, wakati moja ilifanya baridi  mingi na ilinesha telugi. Maji iliisha kugandama. Kwa ajili ya pepo nguvu ma nyumba ilijaza na teluji na matafari ilianguka chini ya yulu. Wa masikini waliomboleza na walitaabu bila kitumaini. Wengine walikufa kwa ajili ya njaa na wengine walikufa ndani ya teluji. Ma tuku ya bulongo walipasuka, miti walitosha inje na ma ndege walikufa nyingi.

Hii wakati ya baridi na teluji ilikuwa ma siku nyingi. Kisha ma juma wa wili, pepo ilishuka na mt. Andreas, aliyeteswa hile wakati ya baridi, alikuja kwa padri ya roho yake padri Nikiforos na aliluelejea hii mambo yake yote:

«Misikuweze kuvumilia baridi na pepo, kwani nilikuwa mutupu, bila vilato na bila nyumba. Basi, nilikimbilia kwa watu wamasikini, wa ndugu wnagu, lakini na hawa walinifukuza. Walinizarau na walinitosha na bakora yao sawa ibwa.

-Toka ya huku, ibwa, waliniambia. Toka mbali!

Fasi ya kukimbilia na kuokolewa misikuweze kupata. Nilipotesha kitumaini yangu. Niliogopa ya kama nitakufa. Nilisema, jina ya Mungu iwe kwa utukufu, kwa sababu, kama nitakufa, Mungu atanipokelea sawa mushahidi. Mungu hana musiyehaki. Huyu, aliyetuma baridi, huyu atanipatia na namna ya kuishi na uvumilia. Basi, nilienda mu fasi moja na nilipata ibwa moja, aliyelala pale. Nililaria pale na nilitumainia ya kama ibwa atanipatia kivukutu yake. Halafu, wakati huyu aliniona karibu yake, alisimama na alikimbia.

Nilisema hile saa kwa maungo yangu:

-Unaona, weye mudanganyifu? Unaona ngapi uko mtu mwenye zambi? Tena na maibwa wanakuzarau na wanakimbia mbali yako na wanakataa kwa kupokelea na wanakuzarau sawa shetani muovu. Wandugu wako masikini wanakuzarau. Basi, inabakia nini kwako? Hakuna wokovu kwako ndani ya hii dunia.

Ile saa nilisema hivi na taabu mingi, nilianza kulia. Na kwa sababu baridi ilinipika sana, nilianza kutosha machozi na ma macho ya nafsi yangu nilipandisha kwa Mungu. Vipande vyote ya mwili yangu pole-pole walijaza na baridi na hakuna namna kuitenga. Nilizania hile saa ya kama nitakufa.. .

Mara moja nilisikia kivukutu. Nilifungula ma macho yangu na niliona kijana moja na uso muzuri sana. Aliangaza uso na mwili yake sawa jua! Pa mkono yake alikamata mayani moja wa zahabu. Pempeni yake ilikuwa na maua ya kuachana na haikukuwe umoja na maua ya hii dunia, hapana! Walikuwa maua ya kuachana. Alikamata hii mayani ya ajabu na aliniangalia. Aliniuliza:

-Ee Andrea, ulikuwa wapi?

-Katika ngiza na kivuli ya lufu, nilimujibu.

Hile saa tena nilimujibu, huyu alinipika pa uso yangu na hii mayani na alinisema:

-Tangu sasa mwili yako itakamata nguvu na uzima mupya.

Mara moja harufu ya hile maua iliingia ndani ya roho yangu na mara moja nilipata nguvu mu uzima yangu. Hile saa nilisikia sauti moja aliniambia:

-Mumupeleke kumutulivu ya ma juma wa wili na kisha mumurudishe huku, kwani ninataka kushindana tena ndani ya hii dunia.

Hile saa alisema hii sauti hule Malaika, mimi nilisikia ya kama nilianguka ndani ya musingizi mingi na misikusikie mambo gani ilinifanyika. Niliisha ma juma wa wili pa hile fasi Mungu aliisha kutengeneza na mimi nilisikia ya kama nililala usiku moja na asubui nililamuka.

Mukuona ya kama nilikuwa mu fasi ya paradizo wa ajabu na wa utamu zaidi, nilishituka. Niliuliza maungo yangu: Ni je maana ya hii jambo? Nilijua ya kama nilibakia mu mji Konstantinopoli. Lakini, ya kazi gani, nilibakia ndani ya hile fasi, misikusikie. Nilishangaa na misikuweze kufafanusha hii mambo ya ajabu yangu.

Nilisikia ya kama nilikuwa bila mwili. Nilivaa nguo meupe, wa mwangaza na ma pambo mingi na nilifurahi sana. Pa kichwa yangu nilivaa taji wa zahabu na wa nuru na nilivaa na musipi nyekunda na wa mwangaza. Hii fasi ya paradizo ilijaza na nuru, lakini hii nuru niliiona mara ya kwanza. Harufu moja wa ajabu ilikaribia kinywa na pua yangu na ilinijaza na furaha na nilikuwa sawa mulevi!

Ndani ya hii shamba ya Mungu nilikuwa sawa mufalme! Nilifuraha sana kwani niliona maungo yangu kuikaa ndani ya hii fasi takatifu. Pale walikuwa na miti nyingi bila kufanana na miti ya hii dunia. Walikuwa hii mkti na mayani mingi na kutosha harufu na matunda yao ilikuwa na utamu sana. Mambo ya ajabu ilikuwa na hii jambo: Miti ingine walikuwa na paka maua, ingine matunda na ingine paka mayani. Pa hii mayani walikuwa ma ndege, wadongo na wakubwa na mabwa yao wa zahabu na meupe. Beingine waliimba ndani ya mayani na wimbo yao ilikuwa utamu na wa furaha na ilisikiwa mpaka ya kona ya mbingu.

Hile saa nilitembea ndani ya hii shamba niliona mara moja mutoni moja munene iliyetambuka katikati ya paradizo na miti yote ilimwangishwa ya hii maji yake. pale walikuja kunywa maji ma ndege. Mu fasi ya kuhume na kushoto ya mutoni ilikuwa shamba ya muzabibu na mayani yake ilikuwa sawa wa zahabu na ilizambala pa fasi yote ya paradizo.

Mukuona hii vitu vitakaitfu ndani ya hii paradizo roho yangu ilifurahi sana na nilishangaa kuliko mingi ya kuona kila kintu wa ajabu! Ya saa mingi niliikaa na nilisikia sauti ya pepo moja iliyekuja toka mashariki. Mayani ya miti ilitengwa juu yake na walitosha harufu moija muzuri sana. Nilipumuzi na furaha mingi hii harufu. Nilizania ya kama malaika ya Mungu walifukiza na chetezo na ubani mbele ya Mwana wa Mungu!

-Niliuliza roho yangu: Namna gani ilifanyika hii baraka takatifu?

Ku mwanzo nilikuwana uwazo ya kama nilikuwa pale na mwili yangu. Misikusikie uzito ya mwili yangu, matakio ao kintu ingine ya mwili ya hii dunia. Vile alipenda Mungu kufanya kwangu.

Tena nilisikia ya kama hile wakati ya ma juma wa wili, misikusikie hata saa kidogo usiku. Pale ilikuwa ma siku yote nuru! Pale ilitawala furaha, uzima, mwangaza na shangilio.

## Onekano ya nuru

Mtakatifu mutawa Simeon wa Theologos mupya alistahiliwa, wakati alikuwa ku mwanzo ya uzima yake kuona ndani ya monasteri Studion ya Konstantinopoli, ono takatifu ya nuru ya Mungu, wakati alikuwa na kipimo miaka 277 ku mwaka 977, kisha uzalio ya Kristu.

Mangaribi ya siku moja, padri ya roho yake, mutawa Simeoni Mweshimiwa, kwani aliona mtoto ya roho yake Simeoni bila kula na kunywa, alimwaambia:

-Mtoto wangu, inapashw akujua ya kama wala na kifungo ya chakula, wala na sala ya usiku, wala na mateso, wala na ma fazila ingine iko namna kumufurahisha Mungu, paka na nafsi yako kuishi na unyenyekevu na upole.

Mtoto ya roho yake alipika magoti mbele ya padri ya roho yake na alimuomba hivi:

-Padri wangu, Mtakatifu ya Mungu, umuombe kwa Mungu juu ya kupata na mimi neema yake katika maombi yako. Mimi misi na kintu ya hii matendoi takaitfu weye uliniambia sasa, paka nikona ma zambi nyingi, yenye na weye unajua.

Padri ya roho yake alifurahi; alimuhamuru kusimama na aende kulala na kusema sawa sala paka Trisayo: «Mungu Mtakatifu.. . ».

Anasema sasa, mtawa Simeoni: «Wakati nilianza kusema: «Mungu Mutakatifu.. . »Nilikumbuka ma sauti ya padri muzee yangu na nilianza kulia na nilisikia furaha na shangilio. Hile saa nuru moja nguvu ilionekana na mini nilikuwa sawa wa ajabu! Nilipotesha mahasa yangu na misikusikie nilikuwa wapi. Nilisahabu nilikuwa nani. Wakati akili yangu ilirudia kwangu, nilianza kupaza sauti hivi: «Bwana hurumia» mara nyingi. Tena misijue kama nilikuwa na mwili ao bila mwili ndani ya hii hali ya nuru ya Mungu. Paka Mungu anajua.. . Nilisikia ya kama nilikuwa muhuru ya ngiza, uzaifu, uvivu na muchoko ya mwili yangu. Nilisikia utamu, kuliko mnenen ya kila utamu ya hii dunia.. . Kisha saa kidogo hii nuru ilianza kushuka pole-pole na ku mwisho ilitokea yote.. . Mimi nilisikia ondoko yake na nilipata taabu. Taabu na sikitiko mingi ilijaza roho yangu, kwa sababu nilipotesha ono takatifu ya nuru ya Mungu.. . »..

## Pa chogo ya kilima Athos

Mtakatifu mutawa Maksimos wa Kafsokalivitis (1270-1365) alikuwa mutawa moja kupita mkubwa katikati ya watawa watakatifu wote ya Kilima Takatifu ya inchi Hellas (Grekia).

Huyu mtakatifu alikombana katika sala na kifungo ya kusafisha akili na roho yake. Kisha ilikuja ndani yake, katika ono moja kimungu, mwito moja wa mbingu.

Mu juma ya Watakatifu Wote, kisha Siku Kuu ya Kupanda Yesu Kristu mbinguni, alionekana kwake Mama Mzazi-Mungu! Alikamata pa mikono yake Mwana wake wa pekee na sauti utamu alimwaambia:

-Ee Maksimos unifate. Panda pa chogo ya Kilima Athos na pale utabeba neema ya Roho Mtakatifu katika matakio na mashindani yako.

Chogo ya hii Kilima ni murefu, metre 2. 033 na mara nyingi haionekane kwa sababu ni ndani ya mawingu. Ilipita wakati ya ma siku saba tangu ile siku Mzazi-Mungu alimwita. Mu Posho asubui, mbele ya Siku Kuu ya Pentikoste, mtakatifu Maksimos alipanda kilima pamoja na watawa wengine. Usiku walibakia ndani ya kanisa moja kwa jina ya Mageuzo Uso ya Yesu Kristu na asubui walifanya Liturgia. Kisha watawa wote walirudia na walimuacha paka huyu Mtakatifu ambakie pale ye wa pekee.

Pale alibakia ma siku na usiku tatu na alifanya sala mbele ya Mungu. sala yake ilikuwa wa moto na nguvu mingi na ililungua ma shetani. Na ma shetani juu ya kumuogopesha, walimuletea majaribu nyingi. Ma sauti makali, makelele, sawa walimufokea watu mengi. Tena walionekana ma uso makali na mabaya juu ya kumuogopehs ana kurudia kwake. Ma shetani walimukombana na mukuki na mupila juu ya kumushusha ya hii chogo. Ma shetani hawakuweze kuvumilia waone huyu mutawa mtakatifu ambakie pale na afanye sala.

Kama mushindani ya roho moja anapenda amupatie Mungu zawadi Yake, mbele atamupima na majaribu ya kuachana. Mtakatifu Maksimos alivumilia hii funjo na uharibifu ya ma shetani, bila kuogopa. Muchoko yake ilikuwa mingi. Lakini, kwa sababu yeye alibakia matata bila woga, Mungu alimulipa zawadi yake. Alishuka Mzazi-Mungu, Mufalme wa mbingu na inchi. Pempeni yake walimufata na ma kundi ya Malaika. Mt. Maksimos alimuona na alimufamia. Na furaha mingi alianguka mbele ya miguu yake, alimusujudu na alimusalimia: Salamu, Mujaliwa neema, Bwana ni pamoja na wewe».

Hule Mama alimujibu:

-Ee Maksimo, askari mweheshimiwa ya Bwana, beba zawadi juu ya kukombana na kufukuza ma shetani. Na tangu leo utaikaa karibu chini ya hii Kilima. Mapenzi ya Mwana wangu ni hii: Utafika pa chogo ya ma fazila na utafanyika mwalimu ya roho na mwongozi watu wingi kwa wokovu.

Hile saa Mzazi-Mungu alimupatia mukate wa mbingu juu ya kupata nguvu mwili yake, kwani hasikukule ya ma siku tatu. Wakati aliweka mu kinywa yake kipande moja ya hii mukate, ilimufunika nuru takatifu na wimbo wa malaika moja ilikuja pa masikio yake. Mara moja Mzazi-Mungu Maria alirudia mbinguni. Aliondoka, lakini aliacha mukongo yake mwangaza na harufu muzuri sana! Mtakatifu alisimama na mashituko mingi. Hasipende kushuka ya hii Kilima. Hii fasi ilifanana sawa Kilima Tabori na nyumba ya Pentikoste, wakati alishuka Roho Mtakatifu.

Pale alibakia tena ma siku tatu. Hii harufu iliendelea kuwa. Mtakatifu alipika magoti na alibusu hile fasi alisimama Mzazi-Mungu. Alimuomba afike mara ingine, kwani alitaka amuone, lakini alisikia paka harufu na aliona paka mwangaza mara wa wili. Mama Maria hasikufike mara ingine.

## <u>Ma ndege wa kabaila</u>

Usiku moja mtakatifu Sergios wa Rantonezi ya inchi Rusia (1314-1392) aliomba ndani ya utulivu juu ya kusaidia watoto wa roho yake. Mara moja alisikia sauti moja:

-Ee Sergie.. .

Alishangaa, alifungula dirisha aone nani alimwita. Hile saa nuru moja wa ajabu ilijaza mbingu na alisikia hii sauti:

-Ee Sergie. Bwana Yesu alisikia sala yako, ile unafanya juu ya wanafunzi wako. Angalia kundi ya watawa, wenye watakuja mu monasteri yako.. .

Aliangalia inje mt. Sergios na aliona ma ndege mengi kwa kuluka pempeni yake na waliimba na sauti moja utamu wa ajabu.

Mara ingine alisikia Mtakatifu sauti moja:

-Vile na watoto wa roho yako wataogezeka na kisha lufu yako kundi yao itaogezeka tena. Na wale wanapenda wafate mwendo ya uzima yako, watapata ma zawadi wa ajabu.

Mtakatifu alishituka kwa ajili ya hii ono takatifu na manabii ile alisikia. Kwani alitaka kufurahi na mtu mwingine hii ono takatifu aliita na mutawa Simeoni, aliyeishi pale karibu. Padri Simeoni, alishangaa kwa hii mwito ya mtakatfiu Sergios, padri ya roho yake, alikuja na haraka, lakini hasikustahiliwa kuona hii ono nzima. Alitaguria paka kuona mwangaza wa mbingu. Mta. Sergios alimwaambia aliona nini, alisikia nini na wote wa wili hii usiku walifanya sala usiku mzima kwa kumutukuza na kumushukuru Mungu.

## Matembeleo wa ajabu

Usiku ingine, ku mwaka 1388, mtakatifu Sergios wa rantonezi alisimama mbele ya Picha ya Mzazi-Mungu Bikira maria na aliomba kwake.

-Ee Mtakatifu kamili, Mama ya Bwana wetu Yesu Kristu, kitumaini na ulinzi ya waaminifu wetu, uwe musaidizi kwa sisi wasiyostahili. Umuombe kwa Mwana na Mungu wako aonyeshe wema wake pa hii fasi takaitfu yetu. Sisi watumwa wako, tunakuomba kutusaidie, ee Mama ya Kristu, kwa sababu weye uko kwa sisi wote kimbilio na nguvu.

Mukuisha sala yake, aliikaa kidogo apumuzike. Mara moja alisema kwa mwanafunzi wake, jina lake Mika:

-Mtoto wangu, mbakia hii usiku bila kulala.

Wakati alisema hii sauti yake, mara moja alisikia sauti moja:

-Anakuja Mtakatifu Kamili Mama Maria!

Mtakatifu Sergios alitoka inje ya chumba yake, na pale nuru takatifu ilimufunika! Alistahiliwa kuona na mwangaza mingi Mama wa Mungu, aliyemufwata Mtume Petro na Mwevangelizaji Yoano. Kwa sababu hasikuweze kuvumilia utukufu ya hii ono wa ajabu padri Sergios alianguka chini. Mzazi-Mungu maria alinamisha kidogo, alimugusa na mikono yake na alimwaambia:

-Usiogope!  Nilikuja kukutembelea, kwa sababu nilisikia ma sala yako, ile unafanya juu ya monasteri na watoto ya roho yako. Usitaabu na usisikitike juu ya monasteri yako. Tangu leo na ma siku yote mimi nitalinzi hii fasi takatifu na hile wakati unaishi na kisha lufu yako.

Hii mwangaza ilitoka na mt. Sergios alibakia na musangao. Wakati alisikia kidogo nzuri, aliona mtoto ya roho yake bila kutengwa, sawa mufu kwa ajili ya woga na mashituko. Alimusaidia asimame. Hule alianguka mbele ya miguu yake alimwaambia:

-Ee padri, kwa neema ya Kristu, unisema juu ya hii ono wa ajabu. Ilinishitushe sana na nilisikia ya kama nafsi yangu ilitokea ku mwili yangu.

-Mtoto wangu, ongojea kidogo, kwa sababu na mimi misiweze kusema kintu kwa ajili ya hii musangao.

Kisha alimwaambia:  Wende kumwita wafike hapa padri Isaaka na p. Simeoni.

Wakati walikuja wa padri wa wili, huyu aliwaelejea matembeleo ya Mzazi-Mungu na Mitume wa wili. Ma roho yao ilijaza na furaha. Waliimba Maombi Kidogo ya Mzazi-Mungu na mt. Sergios alibakia hile usiku bila kulala na aliwaza hii ono na mafikisho ya Mama Maria.

## Matembeleo ya Roho Mtakatifu

Asubui moja hile wakati ya baridi mu inchi Rusia ndani ya pori alimutembelea mt. Serafim wa Sarofi mukristu moja aliyeitwa Nikolaos Motovilof ku mwaka 1831. Tazama aliaandika nini bwana Nikolaos:

«Ilikuwa mu Kazi inne. Hile siku ilijaza na mawingu. Teluji ilifika yulu na mt. Serafim alianza kusuburia na mimi. Aliniambia nikale pa muti moja na yeye aliikaa mbele yangu mu ngambo ingine. Tulikuwa pamoja ndani ya pori, karibu ya nyumba wa jangwa wake, pa kilima moja mdogo na pempeni ilitembea mutoni Sarofka.

-Bwana alinifunua, alisema huyu mtakatifu Serafim, ya kama tangu kipimo udongo yenu mulitakia sana kusikia ni nani kikomo ya uzima wa Kristu na muliisha kuuliza juu ya hii mambo na watu wengine wakubwa.. . Lakini hata mtu moja hasikuweze amipatie jibu moja wa kweli. Basi, mimi Serafim maskini, sasa nitamielejea ni nani ya kweli kikomo ya uzima ya mukristu moja. Kikomo wa kweli ya uzima wa Kristu ni upatano ya Roho Mtakatifu!

Kisha hii sauti yake, aliendelea hivi:

-Sala, sala wakati ya usiku (Agripnia), kifungo na huruma na matendo ingine mazuri, hile tunafanya kwa ajili ya Kristu, inatusaidia tupate sisi neema ya Roho Mtakatifu. Lakini, ionapaswa kujua, mupendwa wangu, ya kama, paka, wakati hii tendo inafanyika kwa ajili ya mapendo ya Kristu, ni kazi kizuri na inaleta matunda ya Roho Mtakatifu. Ma bikira wa tano ya Evangelion, walikuwa na fazila ya ubikira, lakini walimbakia inje ya nyumba ya Arusi. Hawakupate na «mafuta». Ni nini maana ya «mafuta»? Ni kusema ni ya kupata neema ya Roho Mtakatifu.

-Ni jee maana ya kupata neema? nilimuuliza padri mkubwa mimi. Misiweze kusikia.

-Ninapata ni maana, nikusema ninakamata kintu kimoja na hii ni yangu, alimujibu mt. Serafim. Munajua maana ya sauti: Ninapata makuta. Umoja ni juu ya kupata Roho ya Mungu.. Bwana Yesu Kristu alitupatia mfano juu ya uzima yetu ya kama ni sawa soko na alitwaambia: «Mutumikeni hii wakati yenu juu ya kupata na vitu vitakatifu wa mbingu. Vitu wa inchi ni matendo mazuri na ma fazile hile tunafanya juu ya Kristu na vile hii ma fazila wanatupatia neema ya Roho Mtakatifu. Kila fazila na tendo kizuri sisi tunaifanya kwa ajili ya Kristu inatupatia neema ya Roho Mtakatifu. Mweye, kwa mfano, mutumikeni na hile fazila, inamipatia faida kuliko mingi ya roho. Kwa mufano, kama inamipatia neema mingi maombi mbele ya Mungu na agripnia, mufanye hivi na mweye. Kama inamisaidia juu ya kupata neema ya Mungu kifungu ya chakula, mufanye kifungu. Kama inamisaidia huruma, mufanye huruma kwa jina ya Kristu. Na, kama mutapata ndani ya roho yenu neema ya Roho Mtakatifu, mutaweza kisha kwa kuikabula na kwa watu wengine. Faida yenu itakuwa mingi mbinguni.

-Ee padri wangu, munanifundisha ya kuendelea juu ya neema ya Roho Mtakatifu ya kama hii ni kikomo ya uzima wa Kristu. Lakini namna gani na fasi wapi nitaweza kuona huyu Roho Mtakatifu? Matendo mazuri inaonekana. Lakini nitaweza kuona na mimi Roho Mtakatifu? namna gani nitaweza kufamia ya kama ndani yangu ni neema ya Roho Mtakatifu?

-Hii ni kintu upole, alinijibu padri Serafim. Bwana Yesu anatwaambia ya kama vitu vyote ni mapole kwa wale wanachukua hekima ya Mungu. Mitume walikuwa hii hekima na kwa hivi walisikia ndani yao neema ya Roho wa Mungu. Unaona, basi, ndugu mpendwa wangu, ya kama hii mambo ni upole?

-Lakini, misiweze kusikie namna gani niko ndani ya Neema ya Roho Mtakatifu? Namna gani nitasikia anguko ya Roho Mtakantifu ndani yangu?

-Nilimiambia, ndugu wangu, ni kintu upole. Basi, kintu ingine unataka?

-Ninataka kusikia hii mambo muzuri sana, nilimujibu.

Hile saa padri Serafim alinibamba ya mabeka yangu na alisema:

-Sasa tuko sisi wa wili ndani ya Roho Mtakatifu! .. . Juu ya nini usinione?

-Misiweze kukuangalia, kwa sababu toka ma macho yenu inatokea kundi-kundi ya mwangaza! Uso yenu ni kuliko wa mwangaza ya jua na ma macho yangu inaniuma.

-Usiogope. Sasa na wewe uko wa mwangaza sawa na mimi. Uko na weye ndani ya neema ya Roho Mtakaitfu.

Kisha alinamisha kichwa yake karibu yangu na aliniambia pa masikio yangu:

-Umushukuru Mungu kwa hii rehema yake takatifu. Uliangalia ya kama mimi misikufanye hata alama ya Msalaba. Paka niliomba ndani ya roho yangu na nilisema: «Ee Bwana, umustahili

huyu ndugu Nikolaos aone na ma macho yake ushuko ya Roho Mtakatifu yako». Na tazama, ndugu wangu, Bwana Yesu alitimiza mara moja matakio ya padri Serafim. Sisi namna gani tutakataa kumushukuru Mungu juu ya hii zawadi yake? Lakini, juu ya nini, mupendwa wangu, usione ma macho yangu? Unione, bila kuogopa. Bwana ni karibu yetu!

Kisha hii ma sauti yake, mimi, anasema bwana Nikolaos, niliangalia uso yake na nilishangaa. Uso yake ilikuwa katikati ya nuru, bilka mimi kuiona na macho yangu! Hakuna namna kuaandika hii hali kimungu niliishi pamoja na padri Serafim.

-Sasa unasikia nini? Aliniuliza padri Serafim.

-Ninasikia muzuri sana!

Uniambie safi, unasikia nini?

-Ninasikia utulivu moja na amani ndani ya nafsi yangu!

-Hii, rafiki wa Mungu, ni hile amani alisema Bwana Yesu mbele ya wanafunzi wake: «Salama yangu ninawapa ninyi; nami ninawapa ninyi si kama dunia inavyotoa» (Yoano 14, 27). Kintu ingine unasikia ninyi?

-Utamu mnene, nilimujibu.

-Tunasikia sisi wa wili utami mnene na hata ulimi moja ya hii dunia haitaweze kuandika na kuisema. Kintu ingine unasikia ninyi?

-Furaha, bila kuweza kuisema, ndani ya roho yangu!

-Wakati Roho Mtakatifu, aliendelea, padri Serafim, anashuka ndani ya mtu moja na anamujaza na neema takatifu yake, hile saa roho yake inajaza na furaha takatifu, kwa sababu pa kila fasi anaonekana Roho Mtakatifu analeta paka furaha.

-Kintu ingine unasikia ninyi?

-Kivukutu ya roho, nilimujibu.

-Namna gani, mupendwa wangu? Tuko ndani ya wakati ya baridi. Inje inanyesha teluji na pepo ni wa baridi sana. Sasa namna gani unasikia kivukutu?

-Ninasikia kivukutu ndani ya roho na mwili yangu yote.

-Unasikia na harufu yake? Alimujibu padri mt. Serafim.

Hapana, nilimujibu. Pa hii inchi hakuna harufu umoja.

-Ninaijua. Ni vile unasema. Kila harufu ya hii dunia ni chini kabisa mbele ya harufu ya Roho Mtakatifu. Uliniambia ya kama unasikia kivukutu, lakini inje teluji inaendelea kuanguka na baridi ma fasi yote pempeni yetu. Basi, hii kivukutu unasikia ni ndani ya roho yetu. Ndani yetu ni ufalme wa mbingu, sawa vile alisema na Bwana Yesu Kristu.

-Misijue, padri wangu, kama Mungu atanistahili kuishi mara ingine hii furaha ninasikia leo.

-Mimi ninazania, alisema padri Serafim, ya kama Bwana Yesu atakusaidia kuchunga ndani ya akili yako hii furaha takatifu mu uzima yako yote. Hii zawadi Mungu alipatia hapana kwako, lakini na kwa wale watu wanapenda kujua ni nini Neema ya Mungu na namna gani wataweza kuishi hii furaha kataktifu.

## Kundi wa bikira

Mwaka moja na mwezi kumi mbele ya lufu ya mtakatifu Serafim, asubui mu tarehe 25 mwezi ya tatu, alistahiliwa p. Serafim kupokelea matembeleo ya Mzazi-Mungu. Mutawa mwanamuke Efpraksia ya monasteri Ntiveyevo anatuelejea:

«Ma siku mbili mukongo padri Serafim aliniambia kumukuta. Wakati nilienda kwake, aliniambia:

-Mzazi-Mungu Mama Maria atakuja kwa sisi! Usitaogope.

Kisha saa kidogo ilisikiwa pepo moja nguvu ndani ya pori. Ilisimama pepo na ilisikiwa wimbo muzuri. Mulango ilifunguliwa hii wa pekee na ilijaza na nuru! Harufu moja ilijaza

chumba kuliko nzuri ya ubani. Padri Serafim alikuwa ya kupika magoti chini na kunyanyua mikono yake yulu. Kisha dakika kidogo alisimama na aliniambia:

-Mtoto wangu, usiogope. Haina kintu wa shetani. Rehema ya Mungu inatupatia hii baraka. Tazama, Malkia Mtakatifu kamili, Mzazi-Mungu anakuja karibu yetu!

Kweli. Ku mbele walionekana malaika wa wili na walikamata pa mikono yao mayani na maua. Ma nywele yao walikuwa sawa zahabu na walianguka mukongo pa mabeka yao. Mukongo yao waliwafata mt. Yoano Mubatizaji na Mt. Yoano Mwevangelizaji. Walivaa manguo wa mwangaza na meupe.

Kisha mukongo yao alikuja Mzazi-Mungu Mama Maria na walimufwata kumi na mbili Watakatifu wanawake ma bikira! Mzazi-Mungu alivaa nguo wa inje wa mwangaza na ndani yake ilikuwa na ma alama ya msalaba. Ndani yake alivaa nguo ingine na ragi sombe. Alivaa tena kintu kimoja sawa epitrakhilio na epimanika. Mu kipimo yake alikuwa kuliko murefu ya ma Bikira wengine. Pa kichwa yake alivaa taji moja pahali ilikwa na msalaba nyingi na ilijaza na mwangaza. Ma nywele yake ilikuwa kupita mazuri ya wa malaika na walianguka hivi pa mabeka yake.

Wanawake watakatifu walimufwata walivaa na hawa ma taji pa vichwa vyao! lakini wlaikuwa ya kuachana kwa rago ya manguo yao na kwa kipimo yao. Lakini wote walikuwa wazuri sana.

Mtakatifu kamili Mzazi-Mungu Maria alikuwa katikati yao. Nyumba yangu iliishja kuwa munene na ilijaza na mwangaza. Hile saa alinikaribia Malkia Maria, alinigusu na mukono yake na aliniambia:

-Simama, ee dada, na usituogope! Karibu yangu walikuja na ma Bikira wengine sawa uko na weye.

Nilisimama, bila kusikia wakati gani. Mufalme Mwanamuke wa mbingu Mama Maria, aliniambia tena:

-Usiogope! Tulikuja juu ya kumitembelea.. .

Padri Serafim, alikuwa ya kusimama mbele ya Mzazi-Mungu na Huyu Mama alisuburia naye na namna upole, sawa alikuwa mtu wake. Mimi, nilipotesha akili yangu na nilimuuliza padri Serafim:

-Tuko wapi? Hawa weko wa nani?

Hile saa alinijibu Mzazi-Mungu Bikira Maria:

-Karibia weye wa pekee hawa Wabikira Wanawake na uwaulize weye.

Nilikaribia. Pa mustari wa kwanza walikuwa Mashahidi wakubwa Varvara na Ekaterini. Pa Mustari ya mbili walikuwa Mushahidi wa kwanza Thekla na mushahidi mkubwa Marina. Ku mustari wa tatu walikuwa mt. Irini na Mutawa Efpraksia. Ku mustari wa inne walikuwa Mashahidi wakubwa Pelagia na Dorothea. Mukongo yao alikuwa Mutawa Makrina na Mushahidi Iustini. Na ku mwisho yao waliwafata mushahidi mkubwa Yuliani na mushahidi Anisia.

Niliwakaribisha na mustari moja moja. na wale walinisema jina yao na waliniambia uzima na mateso yao, ile walivumilia kwa ajili ya Kristu. Kisha waliniambia:

-Hii utukufu Mungu hasikutupatie kwa bure, lakini kwa ajili ya mateso na ushindani yetu! na weye utateshwa mu uzima ya utawa.

Mtakatifu Mzazi-Mungu alisema ma sauti mengi pamoja na mt. Serafim. Niliona na mini hii ono wa ajabu, lakini misikuweze kusikia walisuburia nini. paka nilisikia ma sauti wa wili:

-Usiache watoto wa roho yangu (Nikusema watawa wanawake yake ya monasteri ya Diveyevo).

-Ewe Malkia, alimujibu padri Serafim. Ninawasanyika, lakini misiweze kuwanyolosha paka mimi mwenyewe.

-Mimi nitakusaidia ya kila mambo na kazi yako. Utawafundisha ya kwanza utii. Kama watafata utii watakuwa na karibu yako na karibu yangu. Lakini, kama watapotesha ubikira yao, watapotesha na fasi yao katikati ya hawa wanawake Watakatifu kumi na mbili, wenye ni kabisa

karibu yangu. Kisha hata fasi takatifu, hata taji ya utukufu watapata. Kama mtu fulani atawauzi, mimi nitamulipiza. Na huyu atawasaidia atapata huruma mbele yangu na mbele ya Mungu.

Kisha Mzazi-Mungu Maria alipindula kwangu na aliniambia:

-Angalia hawa Wabikira Watakatifu na ma taji yao! Walitakia kupita ufalme wa mbingu na waliacha matawala na mali ya hii dunia. Hawa wote walipenda umaskini, walipendaka paka Mungu Yesu Kristu na kwa hivi sasa unaona utukufu na sifa yao. Lakini, sawa vile waliteswa mashahidi wa zamani, vile wanateswa na wa sasa. Paka wale wa zamani waliteswa na namna ya kuonekana, lakini wa sasa wanateswa kwa siri.

Alipindula kisha Mzazi-Mungu kichwa yake kwa padri Serafim, alimubariki na alimwaambia:

-Mupendwa wangu, kisha saa kidogo, utakuwa pamoja na sisi!

Salimia Watakatgifu wote sasa. Mt. Yonao Mutangulizi na Mtume Yono walimubariki, lakini Wanawake Watakatifu walimusalimia na mukono yao.

Mara moja kisha hoo ono wqa ajabu ilipotea. Ono iliisha. Saa yake ilikuwa karibu saa moja.

-Unaona, dada wangu, alisema padri Serafim, zawadi nini Mungu wetu alitustahili kuishi sisi watu wa bure? Hii ono ni wa kumi na mbili. Leo Bwana Yesu alistahili na weye kuona hii ono. Roho yetu ilijaza na furaha! Basi, tunaweze kuchunga imani na kitumaini yetu kwa Bwana Yesu. Kombana weye shetani na ishi katika uzima ubikira na safi. Bwana atakusaidia ya kila mambo na sikitiko yako. Omba saidio ya Mzazi-Mungu Mama Maria na Watakatifu wote na unikumbuke na mimi mwenye zambi. Wakati unafanya sala, utasema: «Ee Bwana, namna gani itakuwa saa ya lufu yangu? Ee Bwana, namna gani nitakaribia Uhukumu wa mwisho na matata? Namna gani nitajibu juu ya matendo na ma zambi yangu? Ee Mufalme mwanamuke wa mbingu, unidaidie».

## <u>Picha ya Mzazi-Mungu mu Kisanga Tinos ya Hellas</u>

Mtakatifu mutawa mwanamuke Pelagia (+1834) alikuwa na kipimo miaka kumi na tano, wakati aliingia mu Monasteri ya Kekhrobunio ya Kisanga Tinos kuwa mutawa.

Mu kipimo yake miaka makumi saba, mu juma 9 mwezi ya saba ya mwaka 1822, alistahiliwa kuangalia Mzazi-Mungu, aliyemusaidia kupata Picha (Ikone)wa miujiza yake.

Asubui mapema, aliona mu ndoto yake ya kama aliingia ndani ya chumba yake mama moja, mkubwa sawa mufalme na taji wa mwangaza pa kichwa yake na alimwaambia:

-Ee dada Pelagia, misiweze kuvumilia tena Picha yangu kuwa ndani ya bulongo. Hii siku asubui, utalamuka na utaenda kumukuta bwana Stamatis Kagadis. Utamwaambia ya kama ninataka kutosha mimi Kanisa yangu ile ni ndani ya bulongo mu shamba ya bwana Antonios Doksaras. Na huyu atafanya nguvu kujenga Kanisa yangu ingine mupya.

Mutawa Pelagia alilamuka, aliikaa pa kitanda na alianza kukumbuka ndoto yake. Alijua ya Madiko Takatifu ya kama mara nyingi Mungu alionyesha mapenzi yake katika ma ndoto na alianza kuwaza ya kama alionekana kwake Mzazi-Mungu. Aliwaza lakini hivi na unyenyekevu:

-Namna gani ilifanyika hii ndoto wa ajabu kwa mimi mwenye zambi na wa bure? Iko namna mimi mutawa mupotevu kustahiliwa hii safa munene?

tena aliwaza hivi: Na, kama ndoto ni ya kweli, namna gani mimi nitaweza kuvumilia machekelo na mazarau ya watu wa dunia?

Alivaa raso yake, alienda mu Kanisa, alisikia Liturgia takatifu na alirudia nyumbani yake. Alikamata mpango hapana kusema hii ndoto hata kwa mutu moja.

Kisha juma moja, asubui mapema ya Siku ya Mungu, mu tarehe 16 mwezi ya saba alionekana mara ingine mu ndoto yake Hule mkubwa mwanamuke na mucheko wa mwangaza na alimupatia kwake hii sauti umoja.

Hule mutawa Pelagia, alisimama na alisikia ya kama hii ndoto yake haikukuwe wa zoezo sawa ma ndoto ingine. Mzazi-Mungu na hii ndoto alitaka amuonyeshe mapenzi yake. Alikamata mpango kumukuta bwana Stamaths Kagadis amwaambie hii mambo yake. Huyu alikuwa musaidizi ya Monasteri Kekhrovunion ya kila kazi yake wa inje.

Kisha Liturgia, mawazo mabaya walimubamba na walimuteswa:

-Bwana Kagadis (kwani alikuwa mwenye kusirika mbio-mbio)atanipokelea? Atanisikia? Atanisadiki? Ao atanizarau na ataniona sawa mazimu?

Aliogopa na aliacha kupita ma siku ingine bila kumukuta huyu bwana.

Mu Juma ingine, 23 mwezi ya saba alionekana kwake mara ingine hule Mama, lakini sasa hasikukuwe wa furaha na mutulivu, lakini alikuwa mukali na mwenye sikitiko. Hasimupatie sauti mupya, paka alimuuliza juu ya nini asisadiki na anakanyanga amri yake.

Mutawa Pelagia alilamuka na woga na tetemeko mingi. Mara moja aliona mbele ya ma Ikone ya nyumba yake Mzazi-Mungu muzima. Alimwaambia na namna makali:

-Kama unakataa kumaliza matakio yangu, atateswa na bwana Kagadis na Kisanga muzima.

Mutawa Pelagia alifuchika uso na mikono yake, kwani aliogopa kumuona Mzazi-Mungu, na alimuuliza:

-Na namna gani ataweza bwana Kagadis kujenga hii Kanisa yenu, Mama mkubwa?

-Fanya hii sauti mimi ninakwaambia na mambo yas majengo ya kanisa yangu mimi nitasaidia.

-Na nani uko weye, unanipatia hii amri, mama mkubwa?

Hule Mama alibeba uso yake hali utamu na upendwa, alionyesha dunia muzima na mukono yake, na alimujibu:

«Inchi pokea habari njema na furaha kubwa.. . ». Hule mutawa alipika magoti mbele ya Mfalme mwanamuke Mama Maria na aliongeza hii sauti: «Musifuni ma mbingu wa Mungu utukufu.. . ».

Mzazi-Mungu kisha alikimbia! Ono wa ajabu iliisha. Mutawa Pelagia sasa, bila shaka, alienda mbio kumukuta mama mkubwa ya Monasteri yake na alimuelejea hii jambo wa ajabu. Na baraka yake alimukuta bwana Stamatis Kagadis na kisha askofu ya hii njimbo Gabrieli.

Askofu mweshimiwa alisema hii jambo kwa wapadri na waaminifu wake. Ku mwezi Tisa ya mwaka 1822 walianza kuchibula na magumu mingi. Mu tarehe 30 Mwezi ya kwanza (Yanuarie) ya mwaka 1823, walipata Picha Takatifu ya Mzazi-Mungu, ile ni mpaka sasa mu Kanisa yake mu Kisanga Tinos.

## Huu mweupe

Padri ya roho mkubwa Parthenios (1790-1855) aliheshimiwa na alimusifu Uso wa tatu ya Utatu Mutakatifu, nikusema Roho Mtakatifu. Hile wakati ya kipimo ujana yake alipata zawadi moja munene toka Roho Mtakatifu.

«Pamoja na ndugu mudogo yangu, anasema huyu padri Parthenios, tulirudia ku masomo nyumbani yetu. Njia ilikuwa murefu, ilikuja ngiza ya usiku na sisi tulikuwa mu njia. Basi, tulisimama mu fasi moja tupumuzike kidogo chini ya bulongo. Hile usiku mbingu ilikuwa usafi na ya saa mingi misikuweze kufunga ma macho yangu na kulala. Misijue, lakini ndani ya roho yangu nilikuwa furaha moja munene. Niliangalia yulu mbingu na ma nyota yake yote na mara moja niliona huu (ndege) moja mweupe sawa teluji, aliyekuja kwangu!

Nilishangaa.. . Fasi wapi alikuwa hii ndege? .. . Alikuwa yetu? Lakini sisi tusiko na ma ndege nyumbani yetu. Kweli, alikuwa muzuri sana! Nilimuangalia na misikuweze kushofesha mbali ma macho yangu juu yake. Hasikuluke ma fasi mbali mbali. Alikuwa yulu ya kichwa yangu. Wakati ingine alinyanyua yulu yangu na wakati ingine alishuka.

Nililamuka mbio-mbio na ndugu yangu, aliyelala karibu yangu.

-Angalia! nilimwaambia. Unaona hii huu?

-Huu nani? Eko wapi?

-Tazama, analuka pa kichwa yangu.

-Hapana, ndugu wangu, misione kintu. Weye, ninazania, sasa ulilamuka ku musingizi na usijue unasema nini.. .

Aligeuza ribeka yake na aliendelea kulala ndugu yake. Lakini mimi mpaka asubui mapema misikuweze kuepuka ma macho yangu ku huyu mwenye kutembelea wa usiku. Furaha takatifu iliisha kujaza roho yangu.

Wakati ilifika asubui mapema, huu bila kuruka, mara moja hasikuonekane! Tangu hile saa ilizambalala ndani ya nafsi yangu matakio moja munene juu ya kintu kimoja kitakatifu. Hata kintu ya hii dunia hasikunikokote. Nilisikia ya kama misitaweze kumbakia tena ndani ya hii dunia»

Hii ono wa utamu hasikuweze kuisahabu padri mkubwa Parthenios. Aliaandika sala moja kwa jina ya Roho Mtakaitfu. Anaandika hivi:

«Ewe mufariji asiyekuwandikwa, mwenye unaotka toka Baba na unapumzika kwa Mwana, weka ndani yangu hekalu ya utukufu yako. Ninakumbuka onekano ya neema yako wa utulivu na upole mu kipimo ujana yangu, ile wakati na mfano ya ndege huu ulinitembelea mimi muzaifu na muvivu».

## Mtakatifu kamili Mzazi-Mungu Mwenye kusikia mbio

Siku moja ya kipwa mu mwaka 1931 mutawa munyenyekevu p. Vasilios Ilie (1902-1931) ya Monasteri Sikhastria ya inchi Rumania aliomba mbele ya Kanisa ya monasteri yake. Hile saa aliona ono moja wa ajabu. Kwa ajili ya woga wake alianza kupaza sauti aseme nguvu:

-Mtakatifu kamili ee Mzazi-Mungu, unihurumie.

Na mbele ya wapdri, wenye walikuja karibu yake aliwaambia:

-Ee Wapadri mumusujudu. Tazama, alikuja Malkia wetu! Mama ya Bwana wetu pamoja na Mwana wake wa pekee pa mikono yake ni mbele yetu! Mumutazame, anasimama yulu yetu.

-Ndugu Vasilie, juu ya ninyi unatwaambie hivi nguvu? Walimuuliza wapadri wengine.

-Wa padri wangu, wakati niliomba mbele ya kanisa, mara moja alikuja kundi moja ya ma shetani, waliyekamata na ma bakora marefu pa mikono yao na walianza kunipika na walisema nguvu hivi: «Unaomba kwa bure, kwa sababu hautaokolewe! Weye uko wetu. Uko mwenye zambi». Hile saa mimi nilianza kumuita Mzazi-Mungu Mama Maria. Hile saa ilishuka ku mbingu mawingu moja meupe iliyejaza na nuru na ilisimama yulu ya kanisa. Ndani ya hii mawingu niliona Mama wa Mungu pamoja na Mwana wake wa pekee ndani ya mikono yake na aliniambia: «Usiogope, kwa sababu kisha ma siku tatu utakuja kwetu». Kisha Kristu alitubariki sisi wote na alirudia pamoja na Mama yake mbinguni. Wa padri wangu, Mzazi-Mungu eko na uwezo mnene kabisa mbele ya Bwana na mbio- mbio anasikia maombi yetu.

-Ndugu Vasilie, alimwaambia padri mkubwa yake, adui (shetani) anakulanda! Epuka akili yako ya hii jambo na sopoka mingi, kwa sababu matego ya shetani ni wingi!

Kisha alisema kwa wapadri wengine:

-Kama, ndugu wetu Vasilios, kisha ma siku tatu ataondoka mbinguni, na sisi tutasadiki ya kama Mzazi-Mungu alimuonyesha hii mambo. Kama hapana, sisi tutajua ya kama shetani alimulanda!

Kisha alisema kwa watawa wengine:

Kisha ma siku tatu, hile saa umoja ndugu mutawa Vasilios Ilie alilala katika Kristu na kusema sala pa midomo yake.

## Ulinzi ya Mzazi-Mungu

Musaidizi ya padri mkubwa mu monasteri Sikhastria ya Rumania alikuwa mutawa Ilarion Ionika (1854-1934). Mbele ya kuwa mutawa alikuwa mufundi ya kufanya ma chombo mu mutoni Bistricha. Usiku moja ya baridi, wakati alirudia nyumbani yake ku kazi yake, walimupika maibwa ya pori. Alikombana na wao ma saa wa wili, lakini hakuna kitumaini ya uzima yake. Alipika magoti na aliomba hivi:

-Mtakatifu kamili Mzazi-Mungu maria, kama utanipatia uzima yangu sasa, nitaacha vitu vyangu vyote na nitafanyika mutawa.

Hile saa alisikia ma sauti ya watu wingi na motokaa moja. Maimbwa ya pori walikimbia na huyu aliokolewa na alirudia mu nyumba na jamaa yake muzima. Kisha ma miezi kidogo aliondoka ya nyumba yake na alienda mu monasteri kutumika kwa Mungu na Mama wake.

Kisha mwaka moja shetani alimuletea majaribu moja mnene. Ilimubamba taabu ya roho na matakio juu ya kutoka ya monasteri yake na aende mu monasteri ingine. Usiku moja alienda mu kanisa, alifanya sala mingi na alitosha machozi. Kisha aliona ya kama toka Picha ya Mzazi-Mungu alitoka mwanamuke moja na nguo meushi ya utawa!  Alimukaribia na alimuuliza:

-Juu ya nini unalia na unaogopa, ndugu Yoano?  (Yoano ilikuwa jina yake ya ubatizo).

-Hapa nilichoka na nilitaka kuondoka mu fasi ingine!

-Juu ya nini unachoka kuikaa ndani ya nyumba yangu?  Ikaa huku na amani na fanya kila kazi yako na mapendo na tangu sasa  na ku mbele utaishi bila kupotesha kitumaini yako!

Kisha huyu Mama wa ajabu alirudia ndani ya Picha yake na asikuonekane. Alikuwa Mzazi-Mungu!

Tangu ile saa ndugu Yoano aliokolewa toka hii majaribu. Kisha wakati kidogo, wakati alikuwa mutawa, alifika mu cheo ya ufazili murefu sana.

Ku mwaka 1933, padri Ilarion alienda mu pori kukata kuni na alifanya kilonda mu muguu yake na shoka. Aliteswa sana na aliomba na machozi:

-Mama Mzazi-Mungu, usiniache. Unihurumie!

Usiku moja, wakati yeye aliomba, aliingia mu chumba yake mwanamuke moja na mabguo meushi sawa mutawa na uso yake ilikuwa uso ya mwanamuke moja munganga ya hile mukini na alimuuliza:

-Juu ya nini unalia, padri Ilarion?

-Mama munganga, nilipata kilonda pa muguu yangu na niniuma sana. Ninasikia ya kama nitakufa na ninalia kwani misikutubu tena.

Mama munganga aliangalia muguu, aliigusu na mukono yake na alimwaambia:

-Usilie tena!  Tangu sasa muguu yako inatunzwa na utaishi tena mwaka moja. Kisha utapumzika kwa milele.

Kisha alikimbia na muzee alilala. Alikuwa Mzazi-Mungu.

Asubui alilamuka muzima, alikuja mu kanisa na alielejea muujiza ya Mama Maria kwa watawa wengine wote.

Basi, aliishi tena mwaka moja na hii siku umoja, ni kusema mu Juma ya Jivine (Tirofagi) mu wakati ya Kwarezima, alitoa nafsi yake pa mikono ya Bwana Yesu na wapadri wote walimusindika mpaka fasi ya  kaburi yake.

## Matulivu matakatifu

Tunajua ya kama Mungu alipatia kwa padri mkubwa ya monasteri ya Mtakatifu Grigorio ya Kilima Takatifu, padri Athanasios mabariki matakatifu.

Watoto wa roho yake walimuuliza nguvu juu ya kusema ma fumbo matakatifu aliishi katikati ya sala yake, lakini yeye hasipende kusema, kwani alikuwa na unyenyekevu mingi.

Wakati moja ndani ya kanisa ya hii Monasteri ilikuwa sala ya usiku (agripnia) na wapadri wengine walimuoona pasri mkubwa yao, mwenye alichofa kidogo ku fasi yake na alianguka chini kusujudu. Wapadri wote walishangaa, kwa sbabau walijua ya kama hile waakti haikukuwe lazima kupika magoti ya kusujudu. Wakati alisimama, waliona ya kama uso yake ilikuwa ya

kuachana. Mambo gani, basi, ilifanyika? Hata mpadri moja hakuna namna kujua, kwa sababu padri ya roho yao hasikusema kintu. Paka ku mwisho ya uzima yake alisema kwa mufwasi padri mkubwa mupya arkhim. p. Visarioni.

-Mtoto wangu, kwa sababu unaniuliza nguvu, nitakufunua fumbo takatifu moja. Bila kusikia, kama nilikuwa ma macho yangu ya kufunga ao ya kufungula, nilitazama sawa ono moja Mtakatifu kamili na ukubwa ya mbingu, Mama Maria, aliyekuwa na utukufu mingi! Mbele ya utukufu na Uso yake nililekea muzima na nilianguka chini juu ya kumusujudu!

Vile, kisha miaka nyingi walisikia wapadri ya hii Monasteri juu ya nini padri mkubwa yao alipika magoti ndani ya Kanisa!

## Wanawake wa wili mu Kilima Takatifu

Hile wakati alikuwa padri mkubwa arkhim. p. Athanasios mu monasteri ya Mt. Grigorio mu Kilima Takatifu, aliishi mutawa moja wa kabaila jina lake Gelasios, aliyekuwa mupole na munyenyekevu. Huyu mutawa alifanya kazi yake na roho muzuri na mapendo. Hakuna uovu na majivuno ndani ya roho yake. Joo vile padri mkubwa alimupenda na alimusifu. Huyu mutawa aliona moja ono ndani ya kanisa.

Ilikuwa saa ya ibada ya asubui. Ibada iliisha kufika mu wimbo ya Tisa, ni kusema hile wimbo tunaimba Mama Mzazi-Mungu: «Uliye wa thamani kuashinda.. . ». Huyu mutawa alikuwa mu fasi ya mbili ya Kanisa inayeitwa mu Kilima Takatifu Liti. Alisimama pale na aliona ono moja wa ajabu. Aliona kutoka ku mulango Bora wanawake wa wili, moja ku mbele na mwingine ku mukongo. Hii mambo ilikuwa wa ajabu, kwa sababu ndani ya Kilima Takatifu inakatazwa kuingia wanawake.. . Walitembea ndani pempeni ya kanisa na walitembea mbele ya wale watawa walikuwa ndani. Hule mwanamuke wa mbili na amri ya mwanamuke wa kwanza alipatia makuta kwa kila mutawa.

Wakati iliisha Liturgia Takatifu na chakula ya asubui, padri Gelasios, alienda mbio-mbio kukutana na padri mkubwa Athanasios.

-Ee Muzee wangu, alimwaambia, wanawake wa nani ni hawa walikuja leo asubui ndani ya kanisa yetu?

Padri Athanasios alisikia mara moja ya kama huyu mutawa alipokelea baraka moja munene wa mbingu na alisema kwa mtoto ya roho yake:

-Namna gani uliwaona? Walikuwa wa ngapi? namna gani ilikuwa mavazi yao?

-Walikuwa wa wili. Hule wa kwanza alikuwa murefu, alivaa nguo nyekunda na alimufunika na kichwa yake na alionekana kama Mfalme mwanamuke. Mwingine wa mbili alikuwa kijana mu kipimo yake, mufupi, mupole na alivaa manguo sawa ragi ya mawingu. Tena huyu wa mbili alikabula makuta kwa kila mutawa, kwani vile alimwaambia hule wa kwanza.

-Mtoto wangu, ono nzuri, Mungu alikutuma! Huyu Mama wa kwanza alikuwa Mtakatifu kamili na mkubwa ya Kilima Takatifu muzima na huler wa mbili alikuwa mtakatifu Anastasia, mulinzi ya Monasteri yetu, kwani tukona mifupa matakatifu yake yote huku.

-Vile, inapashwa kuwa, muzee wangu! Na nafsi yangu vile inaniambia. Lakini misiweze kusikia juu ya nini walikabula makuta kwa kila mutawa?

-Walitaka kutuonyesha ya kama wanafurahi kwa muchoko yetu, kama tunalamuka usiku na tunaenda mu kanisa kwa kumutukuza na kumushukuru Mungu na Watakatifu wake na kila mutawa katika muchoko na kazi yake ya roho eko mustahili kubeba na malipo yake. Unakumbuka tunasoma nini mu Sinaksari ya 1 Mwezi ya Kumi?

-Misiweze kukumbuka.

-Tunasoma uzima ya mtakatifu Yoano Kukuzelis, aliyekuwa mwimbaji mkubwa kabisa wakati yake mu Kilima Takatifu. Huyu mbele ya kuwa mutawa, alikuwa mwimbaji mu nyumba ya Mufalme mu muji Konstantinopoli! Kwa ajili ya mapendo yake mingi mbele ya Mungu

alizarau utukufu ya dunia na muji Konstantinopoli na alikuja mu Kilima Takatifu, mu monasteri ya Lavra Mkubwa.

Wakati moja, ilikuwa Posho, sala ya usiku ya Akathistos ya Mzazi-Mungu, hile wakati aliimba mu kanisa ya monasteri yake, aliisha kuchoka na alilala pa kiti yake. Hile saa alikuja kwake na ndoto yake Mama Mzazi-Mungu na alimwaambia: «Salama, ee Yoano, mtoto wangu. Uniimbe na mimi misitakuache». Na alimuweka kintu kimoja ndani ya mukono yake. Hule alilamuka mara moja na furaha miongi. Aliona na musagao ya kama alikamata kweli ndani ya mukono yake wa kuume makuta moja ya zahabu. Aliweka pa Picha wa miujiza ya Mama Maria. Na hii makuta alifanya miujiza!

Padri Gelasios alisikia na ajabu ma sauti ya padri ya roho yake. Alisikia maana ya kukabula makuta mt. Anastasia. Ndani ya roho yake ilisimama nguvu imani ya kama Watakatifu ni wazima na wanatazama na mapendo michoko ya watawa wote. tangu hile siku alibusu na heshima mingi ma Picha ya Mzazi-Mungu na Mifupa matakatifu ya Mt. Anastasia.

## <u>Ya Kupata kanisa moja</u>

Mutawa moja, mupole na munyenyekevu, jina lake p. Visarioni alisema wakati moja kwa mutawa na ndugu yake ya roho padri Lazaros toka Monasteri ya mt. Dionisios ya Kilima Takatifu jamba moja wa ajabu. Namna gani nikusema alipata kanisa moja huyu p. Visarioni, waakti alikuwa mutumishi mu monasteri moja mudogo, inje ya Kilima Takatifu, iliyekuwa kwa nguvu ya Monasteri ya mt. Dionisios. Hadisi ni hii:

«Monasteri yangi alinituma sawa mujukumu ku mwaka 1916 mu Metokhi (monasteri kidogo) ya fasi Mariana, inje ya Kilima Takatifu. Ndani ya roho yangu nilikuwa na sikitiko, kwa sababu, kila mu Juma misikuweze niende mu Kanisa ya muji Poligiros, kwani niliogopa wivi, wenye walikuja kuiba vitu vyangu.

Ku mwaka 1916, kisha Siku Kuu ya Epifania ya Kristu, ilikuwa mwezi ya mbili, usiku moja nilitumika, kwani nilikuwa mashina ya kutwanga ngano. Niliacha kazi yangu na nilienda pa hile fasi ilikuwa moto ya kivukutu. Ya hile yakona niliona muzee moja na ndevu mweupe! Alikuwa karibu ya moto. Nilishangaa, wakati nilimuona, kwani ilikuwa usiku na misikuona mtu moja aingie nyumbani yangu! Lakini nilimusalima na roho muzuri hivi:

-Wafo wako, ee muzee! Uko ya fasi wapi?

-Na mimi ni toka huku karibu.

Aliniuliza: Namna gani unaishi huku padri Visarioni:

-Utukufu kwa Mungu, nilimujibu. Mambo yote inatembea muzuri (Kwani hile wakati nilikuwa kazi mingi ya kutwaga dego ya ngano). Paka niko na sikitiko moja, kwa sababu hakuna kanisa ndani ya hii nyumba yangu na misiende mu muji Poligiros ya Kanisa kila mu Juma kusikia Liturgia kimungu.

-Muzee alinijibu: Hapa iko kanisa moja, ee Visarioni, na usiseme ya kama hapa hakuna kanisa.

-Muzee wangu, unasema ninyi, mimi misijue? Unajua weye kupita ya mimi?

Muzee aliniambia mara nyingi ya kama kanisa ni hapa. Nilimuangalia muzuri, nilishangaa na niliwaza ya kama huyu muzee eko mumbafu.

-Ee Muzee, mimi niko huku mwaka moja na ninajua ya kama hapa hakuna kanisa. Juu ya nini weye unasema ya kama iko kanisa?

-Sikie, ee padri Visarioni, alinijibu. Karibu metre wa wili mbele ya tanuru (fasi ya kukalanga mukate) ndani ya bulongo ni moja kanisa. Chibula na utaipata.

Wakati nilisikia sauti yake, niliwaza juu ya huyu muzee. Nani eko? Kisha muzee aliniambia:

-Weye Visarioni, usisadiki ma sauti yangu. Lakini sadiki, bila shaka, kwani ni mapenzi ya Mungu hii kanisa kuitosha na yulu yake utajenga ingine mupya. Usishake mu sauti yangu yote.

Kisha mimi nilianza kusadiki na nilimuuliza kama iko na ingine kintu kitakatifu, nikusema vitu vitakatifu, makuta na ingine.. .

-Alinijibu: Juu ya kusadiki tena kuliko, sikia: Kama utapata nguzo (colone) ya Meza takatifu, utasimama kazi ya kuchibula. Utafanya mara tatu alama ya msalaba, kisha utapika magoti mara tatu (metanies) na utaona jambo moja ya ajabu. Hii bulongo ni pa Meza, itaanguka chini hii wa pekee, bila kuisukuma weye.

Wakati nilisikia sauti yake, roho yangu ilijaza na furaha na nilisema kwake:

-Hii usiku utabakia kwangu. Utakula na mimi na utapumzika.

-Hii saa, nitaenda wapi? Paka huku nitabakia.

Wakati tulisuburia hii mambo, nilienda kuangalia kazi yangu namna gani inaenda. Nilirudia juu ya kuendelesha mazungumuzo yetu, lakini hule muzee nitamupata wapi? Alikimbia. Nilimuita musaidizi yangu, mwaminifu moja jina lake Dimosthenis kama aliona muzee moja apite mbele yake na aliondoka. Yeye asikumuone. Mimi nilikuwa na sasa mawazo ya mbali-mbali. Nitafanya nini? Nitaanza kuchibula ao hapana?

Ilipita juma moja, na usiku moja, hile saa nililala, ilikuja kintu kimoja uzito na iliikaa yulu pa kilari yangu. Ilikuwa uzito mpaka 500 kilograme. Hile saa nilikuwa na sikitiko na woga moja munene. Hile saa nilitaabu, nilisikia sauti moja: «Juu ya nini usikufanye sawa vile hule Muzee alikuambia? ». Mimi, wakati nilisikia hii sauti, juu ya kuokolewa, nilisema «kesho» nitafata sauti ya hule Muzee». Kisha sauti aliniambia: «Wakati ilikuja na usichelewe». Vile nilijiuhuru ya hii uzito ilikuwa pa kilari yangu.

Asubui mapema nilichukua piki na nilianza kuchibula mbele ya tanuru na woga na tetemeko kidogo. Alinisikia mwanamuke moja, bibi ya mutumishi yangu. Alishangaa, alikuja kwangu na aliniuliza:

-Ee padri, unafanya nini leo asubui?

Mimi niliendela kazi yangu pasipo kumujibu. Nilimwaambia paka kutoka mbali yangu. Nilichibula mpaka metre moja. Nilipata matafari na kidogo chini nilipata kibabashi ya kanisa. Alikuja na musaidizi yangu Dimosthanis. Pamoja tulichibula. Tulipata hii nguzo. Kisha mimi nilisema kwa mutumishi yangu:

-Sasa utaona muujiza moja! Sasa nitafanya metanies tatu na alama ya msalaba na utaona hii bulongo ni pempeni ya nguzo itaanguka yote chini.

Huyu hasikusadiki. Basi, niliweka metanies tatu, nilifanya alama ya msalaba na, o Muujiza wa ajabu, Brrrrrr, bulongo yote ilianguka chini. Meza Takatifu ilionekana pempeni na nguvu wa Mungu. Kisha mutumishi Dimosthenis alichibula na imani na mapendo. Vile ilionekana hii kanisa».

## Onekano ya Mtakatifu Yoano Mubatizaji

Huyu mutawa padri Visarioni alielejea na onekano moja ya mtakatifu Yoano Mubatizaji, miaka wa wili kisha onekano ya kanisa wa zamani mu Metokhi Mariana ya Kalkidiki, inje ya Kilima Takatifu.

Siku moja watu wa wili ya mukini moja walitengeneza bei juu ya kununua moja punda-nyama ya mwingine. Huyu aliyenunua punda, alienda mu kanisa na alisujudu ma Ikone. Aliacha na mbele ya picha ya mt. Yoano na makuta filani na aliniambia mimi kuwaaka mishumaa moja. Mimi niliwaka mishumaa moja, niliona na makuta hile aliacha. Ilikuwa mbele ya picha ya Mtakaitfu. Mangaribi nilienda kuwaakisha ma Kandili ya watakatifu, lakini hii makuta haikukuwe pale! Nilisikitika sana.. . Shetani alinipatia huzunina kisilani ya roho yangu. Nilienda mbele ya picha ya Mt. Yoano na nilimwaambia:

-Ee Mt. Yoano, usiwe hapa? Juu ya nini unaacha na watu wageni waliingia ndani ya kanisa yako na waliiba makuta? Na mimi tangu leo misitakuwaakisha kandili yako!

Vile niliwaakisha kandili ya Mzazi-Mungu na niliondoka. Ndivyo, lakini ndani roho yangu ilinipika kidogo. Nilienda mu kazi yangu, nilipanda nyumbani yangu ya chakula, lakini niliisha kopotesha amni ya roho yangu. Nilikumbuka ya kama kandili ya Mtakatifu Mulinzi ya Metokhi yangu niliacha ya kuizimisha, lakini shetani hasikuniache. Roho yangu ilikuwa sawa njiwe. Nilisema ndani ya roho yangu: Tutaangalia itakuwa mambo gani. Misitawaakishe kandili hii usiku».

Basi, nilienda kupumzika, lakini nilikuwa makelele ndani ya roho yangu. Wakati nililala katikati ya usiku, nilisikia ya kama moja alinisukuma. Nililamuka na niliona mtu moja munene na murefu na ma nywele yake ilikuwa marefu mukongo ya mabeka yake. Kwa ajili ya woga wangu, nilianza kuogopa na ugumu mingi nilimuuliza:

-Namna gani ulikuja weye huku?

-Huyu alinijibu na namna bila mucheko: Namna gani nilikuja huku, usiniulize, lakini unijibu weye juu ya nini unakataa kuwaakisha kandili yangu?

Mimi niliogopa sana na sauti katika tetemeko na machozi pa ma macho yangu, nilimujibu:

-Unihurumie, ee Mtakatifu. Nilikosa mbele yako.

Nilimuweka metanies tatu (kupika magoti) na nililia mbele ya miguu yake. Nilimuomba anihurumie. Hile saa nilisikia Mtakaitfu Yoano Mubatizaji na namna upole na utamu na aliniambia:

-Mtoto wangu, Visarioni, unasema ya kama mimi misina huku. Lakini, kama mimi misina huku, nani anakulinzi hapa miaka mingi ndani ya hii jangwa ya kila munyanganyi na watu mabaya?

-Mtakatifu wangu, ninakuomba, unihurumie, Misitafanye mara ingine!

-Wende kuwakisha kandili yangu mbele ya picha yangu na utahubiri na kwa watu wengine na kama ma picha ya Watakatifu wanafanya miujiza, kwa sababu ninaona ya kama watu wingin walianza na huku kusema ya kama ma poicha yetu hawafanye miujiza.

Hii ma sauti aliniambia Mtakatifu Yoano na alikimbia. Mimi mara moja, hilesaa, nilienda mu kanisa na, o muujiza wa ajabu, niliona makuta yote ilikuwa mbele ya ikone ya Mtakatifu Yoano!

Mwivi nani, ninawaza, aliteswa kwa ajili ya mt. Yoano na hii usiku, asubui mapema, alirudisha hii makuta aliiba!

## Maombi nguvu mbele ya Mungu

Mtakatifu mutawa Siluanos wa Kilima Takatifu (Athonitis) (1866-1938), aliyemufamia mutakatifu na Kanisa yetu Orthodokse, mu mwaka 1988, waakti aliishi, alipenda kuishi nguvu paka na Mungu! Alimuomba Mungu ya wakati mingi na machozi mengi, lakini hasikupokelewa utulivu moja.

Ilipita wakati ya miezi mengi na huyu kwa ajili ya sala yake mingi, alilekea na alipotesha nguvu ya mwili yake. Alipotesha tena na kitumaini yake na alipaza sauti kusema mbele ya Mungu:

-Ee Mungu, uko mugumu na asiyena mapendo!

Kisha hii ma sauti yake, alisikia sawa ilipasuka kintu kimoja ndani yake. Na hile saa mara moja aliona Bwana Yesu Kristu muzima mbele yake! Alisikia sawa roho yake ilijaza na moto na kama hii ono ilisimama wakati mingi kwa ajili ya hii moto ilikuwa namna yeye akufe! Tangu hile saa hasikuweze yeye kusahabu richo wa mapendo na upole na wa furaha na wa amani ya Bwana Yesu Kristu. Na ma miaka ingine ya uzima yake, alifundisha na aliaandika ya kama Yesu Kristu ni mapendo. Mapendo bila mupaka na yulu na inje ya kila akili ya mtu.

## Mnara na mawimbi

Arkhim. padri Yoakimu Specheris (1858-1935) aliishi mu monasteri ya Mtakatifu Mutawa savas ya inchi Palestina na kisha mu Kilima takatifu, mu Mukini Skiti Mupya (Nea Skiti). Pa hile wakati alitumika sawa muhubiri ma njimbo ya kwachana ndani ya Hellas (Grekia) watu walimusifu sana kwa ajili ya ma fazila na uzima yake takatifu. Alikuwa padri mufazili na mfano muzuri.

Hile nyakati alikuwa muhubiri mu Mitropolia ya Khalkida na Karistia ya Grekia, alisikia ya kama alifariki katika Kristu padri mujukumu ya Kanisa Orthodokse mu muji Masialia ya Franza. Waliomba wa padri wingi hii fasi. Watu wale walimufamia p. Yoakimu walimusukuma aende mu hile fasi kuwa padri ya wa greki, wenye waliishi mu inchi Franza. Aliaandikla na yeye karatasi ya kuomba hii fasi na alituma mu makutano ya Kanisa ya Grekia. Lakini juu ya moja kuchakula, alipotesha hii kiti na fasi! Basi, alitaabu mingi na sikitiko yake alisema na mbele ya Mzazi-Mungu.

Hile wakati alitumika mbele ya Mama Maria, ilikuja musingizi. Hile saa aliona ndoto hii:

«Niliona ya kama nilikuwa ndani ya mnara moya murefu. Pa chogo yake ilikuwa chumba moja na mimi niliikaa pale wa pekee. Nilishangaa, kwani nilionaka ya kama nilifungwa ndani ya hii chumba pahali ilikuwa ma dirisha wa inne. Kila dirisha ilikuwa pa fasi moja-moja ya mashariki, mangaribi, kaskazini na kusini. Chini ya mnara ilikuwa bahari munene na mawimbi walipika na nguvu mingi pa kibabashi ya hii mnara. Mimi, basi, misikujue kufanya nini, nilikuwa tayari kuanguka inje na ndani ya bahari. Niliogopa mingi, na nilisikia mara moja mukono moja ile ilinibamba ku manguo yangu na alinikokota ku mukongo. Nilipindula mkongo kuona nani ananikokota na niliona, o muujiza wa ajabu, Malkia wa dunia Mzazi-Mungu mama Maria aliyenikamata nguvu na aliniambia:

-Unataka kukuacha kuanguka ndani ya hii bahari wa mawimbi? Hauone mawimbi mengi? Rudia mkongo ndani ya mnara.

Kisha ma sauti ya Mtakatifu kamili wetu, nililamuka na nilisikia ni nani ilikuwa bahari na ni nini maana ya mnara na hatari nini nitapata kama nitapanda pa cheo ya yulu, sawa hivi nilipenda».

## <u>Jua moja ndani ya chumba ya mutawa moja</u>

Mutawa padri Lazaro toka Monasteri ya mt. Dionisios ya Kilima takatifu alipata wakati asikie jambo moja wa ajabu iliyefanyika mu tarehe 11 mwezi ya mbili ya mwaka 1958. Ndugu ya roho yake, mutawa Yerotheos alimwaambia:

-Padri Lazaro, jambo moja wa ajabu ilifanyika kwangu hii ma siku!

-Sema, padri Yerothee, ninakusikia.. .

-Ndugu wangu, ninakuwaambia hii jambo wa ajabu, kwa sababu ninajua ya kama usiseme kintu mbele ya watawa wengine. Misiweze kusema kwa mutawa mwingine. Atawaza ya kama niko mazimu.. .

-Ukona haki, ndugu wangu! Uniambie, basi, kusikia na mimi misitaseme kintu kwa mutu mwingine.

-Hii masiku, kisha kifungo ya mu Juma ya Jivini, inakuja mu Kazi tatu na sisi, kisha kifungo ya ma siku tatu, tutapewa Mwili na Damu ya Kristu katika desturi ya Monasteri yetu. Mimi, kwani nilipenda kutayarisha kidogo kupita muzuri hali ya roho yangu, nilisukuma maungo yangu. Nilifanya kifungo mingi, nilifanya sala mingi na metanies. Mbele usiku ya kulala nilifanya sala ma saa 3-4 na kisha metanies. Ma siku wa wili mbele ya Juma ya Jivini, hile wakati usiku niliomba kwa Mungu, niliona chumba yangu ilijaza na nuru! Nuru wa ajabu, sawa jua meupe kabisa! Na ilionekana ya kama ilitokea ku Picha ya Mzazi-Mungu.

-Wakati uliona hii nuru, uliogopa? Ulishangaa?

-Hapana, misikuogope, lakini nilifurahi mingi. Nilisikia furaha munene na nilianza kusema Wimbo ya Akathiste ya mzazi-Mungu na wimbo ingine nilijua, sawa: «Niliajibu kweli.. . », »Uliye wa thamani.. . » na ingine.. . Niliimba na furaha munene na shangilio.

-Ma saa ma ngapi ilisimama ndani ya chumba yako nuru?

-Ninazania mpaka tatu ao wa inne saa na kisha ilipotea.

Mukusikia hii jambo wa ajabu padri Lazaro alishangaa na alitukuza wema ukubwa ya Bwana Yesu Kristu, aliyeshukisha neema Wake kwa watumihsi wake wenye ya bure na unyenyekevu.

## Mama Mkubwa ya Kilima Takatifu

Arkhim. p. Andreas wa Monasteri ya Mt. Paulo (1904-1987) alikuwa padri mkubwa mara wa wili mu Monasteri yake (1960-62) na (1964-1974). Alifata kabisa ma kazi ya uzima utawa wake na alistahiliwa kuona na Mzazi-Mungu.

Kisha wakati wa kwanza alikuwa padri mkubwa ya Monasteri yake, aliondoka na alienda mu jangwa, shamba ya monasteri yake iliyeitwa Monoksilitis. Wakati moja bahari ilikuwa makali sana. Padri Andreas alikamapa mpango aende mpaka kikavu kuangalia kama bahari ilitosha kuni ile inakuja ya ma fasi ingine ya mbali-mbali juu ya nyumba yake ao kama ilifanyika musiba fulani ndani ya bahari na chombo moja na mtu fulani alikuwa ulazimisho ya saidio.

Basi, alienda mu kikavu na alianza kulokota kuni. Hile saa alilokota alienda ku mbali mtu moja aliyeikaa pa njiwe moja. Aliwaza ya kama alikuwa mutu moja aliyeokolewa kisha musiba ndani ya bahari, ni kusema chombo yake iliharabika na yeye aliokolewa.. Alikaribia sana na aliona na musangao mutawa moja mwanamuke! Huyu alikamata pa mukono yake kitabu moja wazi na aliaandika. Alishituka sana na alimuuliza:

-Ee Mama wangu, unataka nini weye hapa? Unataka saidio moja?

-Hapana, misiombe saidio moja. Mimi ni Mama mkubwa ya hii Fasi Takatifu na ninafanya hii kazi kuangalia na kuaandika uzima ya wale watawa wanaishi hapa.

Padri mkubwa Andreas asikusikie, mambo gani ilikuwa na alimuuliza:

-Hii kitabu unaikamata ni nini?

-Ni kitabu ya kuingia, ya kubakia na ya kutoka ya Wapadri ya Kilima Takatifu. Hapa ni ma jina ya wale watawa wanaishi na wanakufa ndani ya Kilima Takatifu.. .

Hata hii ma sauti yake hasikusikie padri Andreas na, kwani aliwaza ya kama alikuwa mutu moja aliyeokolewa kwa ajili ya musiba moja ndani ya bahari, alirudia nyumbani yake mu fasi Monoksilitis.

Pale alianza kuwaza mara ingine hii jambo. Aliangalia Picha ya Mzazi-Mungu na alimufamia ya kama Hule Mutawa alikuwa Mzazi-Mungu Mama Maria, mkubwa ya Kilima Takatifu!

Alisimamisha Ibada ya Magaribi (Njioni) na alienda mbio karibu ya kikavu, pa hile fasi aliona ono wa ajabu, kwani alitaka kumutaguria na kumuona Mzazi-Mungu.

Alifika mu kikavu mukutosha jashu mingi. Lakini alisikitika sana, kwa sababu hile njiwe ilikuwa wazi! Alitaabu sana. Aliwaza ya kama juu ya zambi yake hasikustahiliwa kuangalia hii ono wa mbingu. Alikaribia njiwe na alipumuzi harufu moja nzuri sana. Mzazi-Mungu Mama Maria alimuonyesha ya kama na hii namna ya kutosha harufu yake alikuwa Huyu na alimufurahisha sana.

# ZAWADI YA MIUJIZA

Muujiza ni kazi kimoja kimungu yenye ni kupita yulu ya sheria ya hii dunia. Ni tendo wa ajabu moja iliyetoka ya Mungu, bila kuharabisha ma sheria ya dunia na inchi yetu. Muujiza ni jambo yulu ya akili yetu na inatuletea ajabu na musagao.

Kila tendo wa zawadi ya Mungu ni moja jambo wa ajabu. Bwana Yesu Kristu alitwaambia: «Kweli, kweli ninawaambia ninyi, Yeye anayeniamini mimi, kazi ninazofanya yeye atazifanya vilevile; na atafanya kazi kubwa kuliko hizi;» (Yoano 14, 12). Tena alitukikisha hivi: «Kwa maana ninawaambia ninyi, Mukiwa na imani kama mbegu ya haradali, mutamwambia mulima huu: Ondoka hapa uende kule, na utaondoka; wala halitakuwa neno lisilowezekana kwenu» (Matayo 17, 20).

Basi, zawadi ya miujiza Mungu anaipatia kwa wale watu wekona imani nguvu. Ni kweli ya kama miujiza hawafanye watu, lakini Mungu katika yao. Mkubwa Antonios anatufundisha: «Uwezo ya kufanya matendo wa ajabu haina yetu, lakini ni tendo ya Mwokozi wetu».

Kila mwaminifu orthodokse, kwani alibeba na Ubatizo yake neema ya Roho Mtakatifu, kama atatakaswa iko namna Mungu asikie maombi yake na atafanya miujiza. Lakini kuliko muujiza munene ni uzalio wa pili katika roho, waakti mtu moja anaondoka ya uzima wa zambi ao uzima ya wapagano na anafata uzima takatifu na mupya mu Kanisa Orthodokse. Mutawa moja wa jangwa alisema hivi: «Misipende kufukuza ma shetani ao kutunza wagonjwa, lakini ninataka kumuomba Mungu anichunge roho yangu hapana kuingia shetani na tena juu ya kusafisha maungo yangu ku kila uwazo mubaya na, tazama, niko mkubwa. Kama mtu moja atamaliza hii tendo wa ajabu, huyu atakuwa pa cheo moja na wale wanafanya miujiza na atastahiliwa aingie mu Ufalme mbinguni.

Na ma shetani wanaweza wafanye «miujiza» wa uwongo, wala hawa wala watumishi wao, nikusema mafumu na milozi. Lakini miujiza ya Mungu inaonekana teketeke, kwa sababu miujiza ya Mungu haifanyikwa juu ya utukufu na majivuno ya watu wa dunia. Kazi yao ni juu ya kusaidia watu kwa kitubio, kwa mapendo na uzima takatifu katika unyenyekevu.

## Ukavu ya miaka tatu

Mwanafunzi ya Mt. Mkubwa Antonios, jina lake Ilarioni (+371), aliitwa na yeye mkubwa, kwa sababu alipeleka uzima ya utawa kutoka Misiri mu inchi Palestina.

Wakati ingine alirudia mu fasi Thivaida ya Misiri, pahali aliishi mwalimu ya roho yake, mt. Antonio. Kule watu waliishi bila kitumaini.. . ya wakati miaka tatu hakuna kunesha nvula! Ilianja njaa moja munene. Mayani yote waliisha kukauka juu ya jua na ma nyama walianza kufa juu ya njaa!

Wakati watu wa Thivaida walipata tangazo ya ufikisho ya padri mkubwa Ilarioni, walisanyikwa pamoja na wabibi na watoto wao na walikuja amukutana naye. Mahaganyiko yao ilikuwa munene juu ya njaa. Walianguka ya kupika magoti mbele yake na walimuomba hivi:

-Utuonyesha wema wako! Utusaidie pa hii mateso na sikitiko yetu! Umuombe kwa Bwana Yesu ya kushusha hasira Yake na atupatie nvula, kwani inchi yetu itaharabika yote.

Mtakatifu mutawa Ilarioni mukuona watu wote ya kukonda sana, aliomboleza mbele ya Mungu. Aminyanyua mbinguni ma macho yake, alinyanyua mikono yake na aliomba na moto ya roho yake kwa Mungu aonyesha wema wake kwa watumwa wake na awapatie nvula.

Mbele ya kuisha maombi yake, ilianza kunesha nvula!

Hii ufazili na baraka munene ya Mungu ilimufwata majaribu moja munene. Kama ilisimama nvula iliyeleta uzima mu hile fasi, walionekana ma nyoka mengi wa sumu na walianza kulumiza watu. Hile saa watu wingi walianguka chini bila nguvu, karibu ya kufa. Mukuona hii jambo mutawa Ilarioni alibeba mafuta, aliomba saidio kwa Jina ya Baba na Mwana na ya Roho Mtakaitfu na alipakaa na hii mafuta vilonda ya wale watu waliteswa chini. Tunzo ilikuwa mara moja! Watu wote walimutukuza Mungu na walimushukuru mutumishi wake, padri mt. Ilarioni.

## Bahari wa mawimbi makali

Hile waakti mutawa mt. Ilarioni alikuwa mu muji Epidavros ya Dalmatia ya Servia, ilifanyika tetemeko moja munene! Ilitetemeka njimbo hile yote. Tena na bahari ilitosha pofu sawa chakula inatosha pofu pa moto na ilitoka ma metre mengi mbali ya kikavu. Vile ilionekana fasi moja munene pa hile fasi maji ya bahari ilikimbia mbali.

Pepo moja nguvu ilikamata ma chombo na iliwatupa mbali pa njiwe na walipasuka. Wakaa ya muji Epidavros mukuona bahari kuwa na tetemeko waliogopa. Waliogopa ya kama inchi itapasuka na wote watakufa ndani ya bahari. Walianza kulia na walimuomba padri Ilarioni awasaidie. Walimwaambia:

--Upendwa wanadamu ya Mungu ilikuletea hapa juu ya kutusaidia pa hii hatari.

Basi, walimupeleka pa kikavu na walimusimamisha aone mawimbi ya bahari. Hule mukusadiki ma sauti ya Bwana Yesu: «Kwa maana ninawaambia ninyi, Mukiwa na imani kama mbegu ya haradali, mutamwambia mulima huu: Ondoka hapa uende kule, na utaondoka; wala halitakuwa neno lisilowezekana kwenu» (Matayo 17, 20). Alifanya nini? Alifanya na buchanga chini, karibu ya kikavu, alama ya msalaba. Kisha alipindula pa fasi ya mashariki, alinyanyua mikono yake mbinguni na alimuomba Mungu aonyeshe wema Wake mbele ya watu wake na katika amri yake asimamishe mawimbo ya bahari na hii bahari arudie pa mipaka yake.

Hile saa padri aliomba, bahari ilinyanyuliwa yulu sana na watu waliogopa ya kama itaharabisha hile njimbo yao yote. Lakini sala yake ilinyanyuliwa kuliko yulu, ilitambuka mbingu na ilifika kwa Mungu mupenda-wanadamu. Pole-pole bahari ilisimama, ilishuka na amani ilirudia pa mipaka yake wa kwanza!

Wakaa ya mji Epidavros kwa kijazi ya kizazi ya miaka mingi walichunga ndani ya akili yao hii muujiza wa ajabu ya hule padri mt. Ilarioni.

## Mutembeo ya wanyanganyi

Mtakatifu mutawa Ilarioni, kwani alichukia utukufu ya dunia, kisha hii muujiza alifanya na mambo ya bahari, alibeba wanafunzi wake na aliondoka mu fasi ingine mbali. Kutoka Dalmatia iliondoka chombo ya Kisanga Kipros. Huyu na kundi yake waliingia waende mu Kipros. Na chombo walifika pa fasi moja, pahali ilikuwa ndani ya bahari ma njiwe. Watumishi ya chombo hawakuweze kutumia na kasia ya chombo na walisukuma chombo na mishale yao. Pa hile fasi, lakini, wa hatari, walifuchama wanyanganyi, wenye, wakati walisikia ya kama ilikuja kwao chombo waliwapika na mikuki yao.

Mu chombo ilifanyika funjo munene! Watumishi ya chombo walivaa ma silaha yao juu ya kukombana wa adui. Watu wenye kusafiri waliomboleza juu ya bahati yao. Tena na wanafunzi ya mt. Ilarioni walimwaambia ya kama hali ya uzima yao ni wa hatari. Hule padti aliwaambia na amani:

-Juu ya nini munaogopa na munasikitika?

Hile saa ilikaribia chombo wa kwanza ya wa adui, mtakatifu Ilarioni alichukua njiwe moja na aliitupa katikati ya ma chombo wa wili na alipaza sauti aseme mbele ya wa adui:

-Musimame mpaka hile fasi ilianguka ndani ya bahari njiwe! Musikaribie kuliko karibu.

Wale hawakusimame pa hile alama. Lakini ilifanyika ninyi? Wa adui walikombana kukaribia chombo ya mt. Ilarioni, lakini ma chombo yao walirudia ku mukongo! Kisha makangamano mengi, walisimama nvita na waliondoka. Hile chombo ilipeleka mutawa Ilarioni iliokolewa ya uharibifu, ilitambuka hile fasi wa ahatari na ilifika mu kikavu ya Pipros bila mambo!

## Kisima isiyona maji

Mutawa Pior wa Misiri alionyesha uvumilia kabaila mu uzima yake. Pa hile jangwa aliishi, alichibula na alipata maji, lakini ilikuwa na chumvi mingi. lakini alibakia pale mpaka lufu yake

na alipima maji ya chumvi!  Watawa wengine wingi walipima kumufwata uzima yake, lakini hata moja hasikuweze abakie kule, pa hile fasi wa matata, kuliko yulu ya mwaka moja.

Wakati fulani mu monasteri moja watawa wenye walikuwa makumi mnane, walichibula kisima moja murefu, lakini, bahati mbaya, hawakupate maji!  Na taabu mingi waliwaza wasimamishe kazi yao. Hile saa waliona ya kama alikuja kwao toka jangwa ndani ya kivukutu ya muda, padri Pior. Aliwakaribia, aliwasalimia na aliwaambia:

-Ee wenye wasiyoimani nguvu, juu ya ninyi mulipotesha imani yenu?  Tangu jana ninamiangalia ku mbali na ninamiona ya kama mulipotesha kitumaini yenu.

Huyu alishuka ndani ya kisima na alimuomba kwa Mungu. Kisha alichukua jembe moja, alipika mara tatu na alisema:

-Mungu wa patriarkhi wa Abrahamu, Isaaka na Yakobo, usiharabishe muchoko ya hawa watumishi yako; uwatumie maji kwani wekona yo lazima kabisa.

Mara moja ilitoka maji na iliwalobana yote!  Mtakatifu Pior, aliomba mara ingine na alilamuka kwa kuondoka. Watawa walimuomba asimame kula pamoja wote. Hule, halafu, hasikupende. Aliondoka mukusema:

-Niliisha hii kazi Mungu alinituma. Hasinitume Mungu ya kula pa meza na mweye.

## Huyu aliyelokota mayani ya ngano

Mtakatifu Makarios na kundi ya wanafunzi wake walivuna shamba ya mtu moja na waliona mwanamuke moja aliyewafata, alilia bila kusimama na alilokota hile mayani ya ngano ilibakia mukongo yao. Hile saa alimuita padri Makarios mkubwa ya shamba na alimuuliza:

-Ya mambo gani eko hapa huyu mama na analia?

-Hule alimujibu:  Mtu moja alimupatia kwa bwana ya huyu mwanamuke makuta mingi ya kuichunga, lakini bwana yake alikufa, pasipo kusema kwa bibi yake fasi wapi alifuchika makuta ya hule mugeni. Sasa huyu mugeni anataka kubeba huyu mama na watoto wake sawa watumwa.

Mtakatifu Makarios alimuwaambia:

-Umuwaambie akuje kwetu kusuburia na sisi, hile saa kati ya muchana tutasimama kazi.

Wakati huyu balaka alikuja, mt. Makarios alimwaambia:

-Juu ya nini unalia vile bila kusimama?

-Kwa sbaabu mtu moja aliacha kwa bwana wangu makuta ya kuichunga, lakini bwana yangu alikufa na hasikuniambie alifuchika wapi hii makuta.

-Twende kutuonyesha fasi wapi ulizika bwana yako. Mtakatifu alibeba na wanafunzi wake na wote walimufata huyu mama. Alisimama mbele ya kaburi yake, alimuomba kwa Mungu nguvu na alimwaambia:

--Uliweka wapi makuta hile mutu moja alikupatia aichunge?

Na hule mufu alimujibu:  Ni ndani ya nyumba yangu, chini ya muguu ya kitanda yangu.

Kisha Mtakatifu alimwaambia:  Endelea kulala mpaka hile saa ya ufufuo yako.

Wanafunzi wake walioshangaa. Walianguka mbele ya miguu yake na walimusususdu. Lakini huyu aliwaambia:

-Hii muujiza haikukuwe toka mimi!  Mimi ni mutu wa bure. Mungu alifanya muujiza Yake kwa huyu mama balaka na watoto wa yatima. Mungu anataka tusifanye sisi zambi na kila kintu tunamuomba, yeye anatuipatia.

Vile huyu mama alipata jibu makuta aliweka wapi bwana mufu yake na aliokoa maungo na watoto yake ku utumwa.

## Binti ya askofu

Mtakatifu Spiridon alikuwa na binti moja mufazili aliyeitwa Irini (Amani). Mutu moja, rafiki yao alimupatia kwa Irini pambo moja nzuri sana. Hule binti, juu ya kuichunga muzuri,

aliifuchika ndani ya bulongo ya inchi. Lakini kisha ma siku madogo alikufa. Kisha muda kidogo huyu mugeni, aliyemupatia pambo yake, alikuja nyumbani ya baba yake, mt. Spiridon na aliomba pambo, lakini binti yake aliisha kufa na baba yake asikujue iko wapi. baba yake, alipata sikitiko juu ya hii hasara ya hule mutu mugeni. Alienda mu kaburi ya mtoto yake na alimuomba Mungu amuulize binti yake aliweka wapi hii pambo.

Na kweli, kitumaini yake ilifanya muujiza. Binti yake alifufuka na alisimama mbele ya baba yake. Alimwaambia aliweka wapi pambo na kisha mara moja alilala.

Mt. Spiridon alipata pambo na alirudisha kwa hule mtu mugeni.

## **Kitubio wa uwongo**

Nyakati moja al;ienda mtu moja pamoja na mtoto mwanaume wake kwa padri mutawa Sisoi aliyeishi mu Kilima ya Mt. Antonios. lakini mu njia mtoto wake alifariki! Baba yake, kwani alikuwa kitumaini kwa utakaso yamkubwa Sisois aliweka mtoto wake pa mabeka yake na aliipeleka mbele ya miguu ya Mtakatifu. Alipika magtoti mbele yake na aliomba baraka yake. Kisdha alienda inje. Mtakatifu Sisois alisema kwa mtoto-mufu:

-Juu ya nini unasimama hapa? Simama na uende kwa baba yako.

Mtoto alifufuka! Alitoka inje na alienda kwa baba yake. Baba yake na furaha na machozi pa macho yake aliingia mara moja ndani, alibusu miguu ya mutawa na alimushukuru sana.

Mutawa Sisois, kwani alikuwa munyenyekevu na hasipende kusikia watu wengine hii muujiza, alimuhamuru baba yake mpaka mwisho ya uzima yake aipashwe kusema sauti moja juu ya hii muujiza.

## **Sikilizano ya mamukini wa wili**

Binti moja aliyeitwa Piamun, aliishi sawa mutawa ya jangwa mu Misri pamoja na mama yake. Alikula mara moja kila ma siku wa wili na alifanya mitunga.

Hile wakati mutoni ya Misri inaitwa Nilos ilijaza na maji na wakaa ya ma mukini wa wili kule walikombana moja ingine juu ya mambo ya kukabula maji. Kwani funjo yao ilikuwa yulu, walikombanishwa katikati yao na wengine walikufa! Pa hile hali, mukini moja alikombana hii mukini aliikaa na Piamun. Watu wingi na ma silaha yao, mikuki na mbau waliondoka waende kupika wakaa ya mukini ya mama mutawa Piamun. Huyu Piamun aliita wakubwa ya mukini yake na aliwashauria hivi:

-Mwende kutoka inje ya kukutana wakaa ya mukini ingine, wenye walikuja kwenu kwa komikombana. Mwende kupatana na wao na kusikilizana kwa sababu, kama hawa wataingia ndani ya mukini yetu, wataharabisha yoyote. Lakini wale waliogopa na walimwaambia aende huyu juu ya kusuburia na hawa. Walimwaambia hivi:

-Sisi tusiweze kuwakutana na hawa, kwa sababu watatupika na mukuki yao. Lakini, kama unapenda mukini yetu na nyumba yako, uende weye mumoja na uwaambie. Watakuheshimiwa weye.

Mutawa Piamun hasikuichike na sauti yao. Lakini alipanda nyumbani yake na usiku muzima alimuomba kwa Mungu:

-Ee Bwana, Wewe unayehukumu dunia muzima na usipende matendo isiyona haki, utubariki sisi na utuokoe toka hii hatari, hii ni mbele ya ma macho yetu. Uwezo yako iwe sawa kibabashi juu ya kusimamisha wa adui, wenye wanakuja kupingana sisi.

Asubui mapema, hile nyakati wa adui walikuwa 5 kilometre mbali ya mukini, walisimama pa hile fasi na hawakuweze kutengwa. Wakati kisha saa kidogo walitangazwa mambo nini iliwafanyika juu ya maombi ya mama mutawa Piamun, walituma tangazo mu mukini yake na waliomba na namna muzuri sikilizano pamoja na wakaa yake. Kisha, walikuwa wahuru ya hii fungu na walitembea na walisikilizana mambo yao.

# Uharibifu ya Armazi

Chini ya inchi munene Rusia ni inchi moja inayeitwa Georgia ao Iviria. Kule alihubiri imani ya Kristu mara ya kwanza Mtume Andreas. Lakini taifa muzima alifata imani mupya ya Kristu mu milele wa inne, hile wakati alikuwa mfalme ya Konstantinopoli Konstantinos Mkubwa (312-337) na mfalme ya Iviria Miriani. Mtume ya Kristu alikuwa mtakatifu mwanamuke Nina.

Mt. Nina, mu kipimo udogo yake, wakati aliishi mu muji Yerusalema, alisikia ku mwalimu mweshimiwa mama Niofora mapokeo moja wa zamani ya kama nguo ya Bwana Yesu Kristu ilikuwa mu inchi ya Iviria. Hile saa iliwaka ndani ya roho yake matakio aende kule juu ya kuisujudu nguo ya Kristu na kuhubiri imani Yake pa hile inchi.

Kisha ma hatari mengi alifika mu muji wa zamani Urbinisi ya inchi Iviria na walimupokelea watu wa Ebrania, wenye waliishi kule. Kule alisikia juu ya kutim na uzima na lugha ya huu taifa.

Kisha mwezi moja, alisikia siku moja ya kama wakaa ya muji hii na ma mukini wa pempeni walitayarisha vitu vyao waende mu muji kubwa ya inchi iliyeitwa Mucketa juu ya kusujudu miungu wao wa uwongo. Pamoja na wao aliendа na mtakatifu Nina. Walikaribia muji na walienda kundi ya wafalme bwana na bibi yake na kundi yao, wenye walienda pa chogo ya mulima moja juu ya kusujudu sanamu iliyeitwa Armazi

Mpaka kati ya muchana ya hile siku muda ilikuwa muzuri na safi. Hii siku itakuwa wa mwisho ya kusujudu watu sanamu moja. Pamoja na watu wote na Mt. Nina aliendа mu chogo ya mulima, pahali ilikuwa hekalu ya sanamu. Alipata fasi moja nzuri na ku hile fasi aliona sanamu. Ilifanana sawa mtu moja mkubwa. Mu kilari yake ilikuwa sawa nguo ya zahabu na kofya wa zahabu pa kichwa yake. Ndani ya ma amcho yake waliisha kuweka ma njiwe mazuri ya mbali-mbali. Pa fasi ya kuhume ya hii sanamu ilikuwa sanamu ingine mudogo wa zahabu, iliyeitwa Gachi, lakini pa fasi ya kushoto ilikuwa ingine na jina Gaimi.

Mufalme na hasira ya watu wote walisimama na heshima na woga mbele ya ma sanamu yao. Waliogopa kukaribia juu ya woga, kwani walisadiki, ya kama watakufa, kwa sababau sanamu Armazi alikamata mu mukono yake na mukuki moja murefu. Walikombana kukumbuka kama walifanya kosa moja, ao walisikitika ma kundi ya wa Kristiani ao ya Waebrania. Walitetemeka ya kama Armazi ilikuwa namna kuwapika na mukuki yake, kama walifanya kosa moja.

Hile wakati mapadri yao walitayarisha masadaka mbele ya ma sanamu. Wakati ubani ilipanda yulu na dami ya ma nyama ilianguka chini watumishi wengine walipika baragumu na goma. Hile saa mufalme na taifa muzima walianguka na uso yao chini. Roho ya Mtakatgifu Nina ilikungua sawa roho ya Nabii Ilie juu ya mapendo ya Mungu na wokovu ya wa ndugu wake! Aliomboleza nguvu, alinyanyua ma macho yake kwa kutosha machozi mbele ya Mungu na alianza sala:

-Ee Mungu Mwenyezi! Katika hasira ya rehema yako ongoza huyu taifa yako mu imani wa kweli. Zambalisha ma sanamu yake, sawa vile pepo inaza, balisha vumbi na maivi. Penda taifa yako, uliyemuumba na mukono wako wa kuhume na ulimusifu katika Sura yako kimungu! Wewe, Bwana na Rabi, ulipenda muumba yako mingi na ulituma duniani Mwana wako wa pekee juu ya wokovu yake. Basi, uhuru hawa ma nafsi ku mamlaka ya mkubwa ya ngiza. Ee Bwana, unibariki kuona na mimi uharibifu muzima ya hii ma sanamu wanaikaa na majivuno huku. Fayna, taifa huu yako na kila taifa ya hii dunia wapate njia ya wokovu na watu wote wasujudu Wewe Mungu Mwenyezi, kwani Kwako ni sifa wa milele na utukufu».

Bado kuisha sala yake mt. Nina na mara moja mawingu walionekana toka magaribi. Mufalme na taifa muzima walisikia hatari na walikimbia mbio-mbio, lakini Mwenye heri mt. Nina alifuchama ndani ya tundu ya njiwe moja. Mawingu walikaribia hile fasi ya sanamu kubwa. Walianguka umeme na pepo nguvu kabisa na nvula. Ma sanamu walianguka chini na

walifanyika vipande-vipande na ma kibabashi ya hekalu ilibomoa chini! Nvula ilinesha sawa mutoni na yoyote matafari na maibwe ilikokota mbali. Kisha saa kidogo hakuna hekalu na ma sanamu!

Mtakatifu Nina alikuwa ndani ya njiwe moja na aliangalia hii kazi ya Mungu wa ajabu. Kisha ilitoka jua na ilikuja kivukutu. Hii uharibifu ilifanyika mu siku ya Shangilio ya Mageuzo Sura ya Bwana Yesu kristu, mu tarehe 6 Mwezi ya Mnane. Tangu hile siku nuru wa mulima Tabori iliangaza mara ya kwanza na taifa ya Iviria na ilizambalisha ngiza ya dini wa sanamu.

## Taji wa moto

Mutawa mtakatifu Theognios, kwani alipenda uzima ya jangwa alikuja na aliikaa karibu ya Monasteri ya mtakatifu Theodosios, iliyekuwa katikati ya muji Bethlehem na Monasteri ya Mtakatifu Savvas.

Ndani ya pango moja ya jangwa aliishi wakati kidogo na kisha, kwani alifanyika hekalu ya Roho Mtakatifu na alivaa silaha ya Mungu, alianza kutunza na neema ya Mungu magonjwa na alifanya miujiza mengi.

Tangazo ya uzima takatifu yake ilizambalala ma fasi mengi. Alijenga monasteri mu fasi moja muzuri. Kisha alifanyika padri na askofu ya muji Vitilio ku askofu mkubwa ya Yerusalema jina lake Ilie. Hii muji ilikuwa muji kidogo 130 kilometre mbali ya muji takatifu, Yerusalema. Mt. Theognios, bila mapenzi yake, aliichika kuwa askofu ya hii muji na alienda mu njimbo yake.

Hile wakati, basi, aliishi kule, bahari muda moja, ilinyanyua yulu, iliingia pa inchi na ma shamba na ilipika muji yake. Ninazania, Mungu alitengeneza hii mambo ya hatari juu ya kufundisha watu, wenye walifanya uzima wa zambi na tena alipenda Mungu kuonyesha neema hiule ilikuwa ndani ya mutumishi wake askofu Theognios. Wakaa ya kumuona mawimbi ya bahari kunyanyua juu, waliogopa na walikimbia. Walienda kwa askofu yao na walimuomba na sala yake asimamishe bahari.

Mushindani mkubwa ya fazila askofu Theognios aliichika, kisha maombi mengi ya watotot ya roho yake. Alishuka mu kikavu, aliweka msalaba moja kule, pa hile fasi ilikuwa mupaka ya bahari na alisema hii ma sauti ya Madiko Takatifu: «Vile anasema Bwana, mpaka hii alama utakuja na usitembee kuliko mbali; na mawimbo yako sasa kusimamishwa».

kama aliweka pale msalaba moja, alirudia kwake. Bahari mara moja alirudia pa mupaka yake na mustari yake wa zamani. Tangu hile siku, wakati mawimbi ilinyanyua yulu, ilifika mpaka pa Msalaba na alirudia mukongo.

## «Jangwa ilitosha maua»

Wakati moja, mt. askofu Yoano wa jangwa alichukua tunda moja ya kukauka na alisema kwa wanafunzi wake jina yao Theodoros na Yoano:

-Munisikie, watoto wangu. Kama upenda wanadamu ya Mungu italeta neema kwa hii tunda na nguvu kwa hii njiwe juu ya kutosha tunda, hii ni alama ya kama Mungu alinipatia ufalme mbinguni.

Kisha hii ma sauti yake aliweka hii tunda ya kukauka pa njiwe moja. Na mUngu, aliyehamuru bakora ya Nabii Musa kutosha maua, Huyu na sassa alihamuru hii njiwe juu ya kutosha mayani mubichi. Alifanya hivi Mungu juu ya kuonyesha kwa watu wengine neema ngapi alikuwa mu roho yake mutumishi wake padri Yoano wa Jangwa.

Mt. askofu Yoano, wakati aliona muti mubichi pa njiwe, alimushukuru Mungu na machozi. Hii mayani ndani ya mwaka moja alitosha matunda tatu! Mtakatifu alibeba hii matunda tatu na machozi, aliibusu mara mengi. Kisha aliwakula mukushukuru Mungu, kwani alimutumia hii tangazo na alikabula kidogo-kidogo kwa wanafunzi wake.

Wakati mwandishi yake padri Kirillos wa Skithopolitis, mwenye aliaandika uzima na matendo ya uzima yake, alienda karibu mu njiwe juu ya kuona muzuri namna gani ilipanda na namna gani iliota pa njiwe muti moja, alishangaa sana, kwa sababu hasikupate hata mizizi, hata tundu moja ya kuingia mizizi. Alipaza sauti kusema na ajabu: «O, hii ni fumbo ya hekima na ufamio ya Mungu; Matendo ya Mungu ni sawa njia na sisi tusiweze kujua! »

## Chakula ya wenye jangwa

Ku mwaka 524, kisha uzalio ya Kristu mutawa mt. Kiryakos wa jangwa aliondoko ku monasteri ya mtakatifu Eftimio na alienda mu jangwa moja pamoja na mtoto moja ya roho yake.

Lakini kule mu jangwa haikuote mayani hata moja juu ya boka yao. Padri Kiryakos alimuomba Mungu amusaidie na kuotesha hata mayani moja juu ya kula. Kule ilikuwa na ilikomea mayani moja sawa matungulu, lakini ilikuwa uchunga sana. Padri alimuomba Mungu ya kugeuza ushungu yake mu utamu. Alisema kwa mtoto ya roho yake:

-Mtoto wangu, uende mu jangwa, lokota na weka pa moto ya kupika hii mayani ni buchungu. Alifanya hivi mtoto yake. Aliweka pa meza ya kula pamoja na chumvi kidogo. Mara moja hii mayani iliyeitwa Skila, iligeuzwa na ilkuwa utamu! Kule waliishi miaka inne na walikula paka hii mayani.

## Mkubwa ya chombo mweshimiwa

Musaidizi moja ya mufalme wa Konstantinopoli aliondoka pamoja na bibi yake aende kutembelea ma Fasi Matakatifu ya Yerusalema, pahali aliishi Yesu Kristu.

Hile wakati walisafiri, huyu na watu ya kundi yake waliharabisha sana hii maji ilikuwa ndani ya chombo. Wakati walifika katikati ya safari yao, maji iliisha na wenye safari walipata mambo munene, bila maji. Watoto wadogo na wanawake wenye walikuwa ya kukonda walianguka chini juu ya hakuna maji!

Kisha ma siku tatu hali ilikuwa mubaya kabisa. Hakuna kitumaini, kwani wlaikuwa kati ya bahari. Lufu yao ilikuwa wa kweli.

Hile saa huyu musaidizi ya mufalme, aliyekuwa mukosefu juu ya hii mateso, alitosha kisu yake juu ya kuua mkubwa ya chombo na watumishi yake. Lakini mtu mwingine alimubamba.

-Usifanye uwaji isiyo haki. Omba na weye mbele ya Mungu wetu Yesu kristu atusaidie.

Siku wa inne, huyu mkubwa ya chombo mwaaminifu aliyefanya sala pamoja na kifungo ya chakula, alipaza sauti alisema:

-Utukufu kwako, ee Kristu Mungu wetu!

Watu wote walishangaa. Lakini huyu alihamuru watumishi wa chombo:

-Mufungule ma hema ya chombo.

Watumishi wake walifungula na walizambalisha pa chombo, mara moja ilikuja mawingu moja meushi yulu ya chombo na ilianza kunesha nvula! Ma hema ya chombo walilokota hii maji ya nvula na walijaza ma jerekani na ma tuku yao yote.

Vile chombo iliweza endelee safari yake mpaka palestina.

## Wokovu ya ndugu moja

Siku moja, mtakatifu mutawa Venediktos alikuwa na ukimya mu chumba yake na mwanafunzi wake mutawa Plakidas alienda mu kiziwa moja juu ya kushota maji. Lakini kule ilianguka ka mikono yake birika yake na ilipotea ndani ya maji. Alikangamana huyu ndugu ya kuibamba, lakini alitelemuka na yeye ndani ya maji. Hile saa mutumishi ya Mungu Venediktos,

aliyekuwa nyumbani yake, alipata tangazo mambo gani ilifanyika. Aliita mara moja mwanafunzi wake mwingine, jina lake Mavros, na alimwaambia:

-Ndugu Mavros, kimbia mbio ku kiziwa, kwa sababu ndugu Plakidas alianguka ndani ya maji.

Na hile saa ilifanyika muujiza moja, sawa hile muujiza ilifanyika na Mtume Petro mu kiziwa ya Galilaya.

Mutawa Mavros na amri ya padri mkubwa yake, aliemnda mbio ku kiziwa. Alitembea pa maji na aliendelea kukimbnia pa maji mpaka alifika pa hile fasi alikuwa mutawa Plakidas! Alimubamba ku ma nywele na alirudia mbio ku mukongo. Wakati alifika pa inchi, paka hile saa alisikia ya kama aliisha kutembea pa maji ya kiziwa! Alishangaa na alirudia kwa padri ya roho yake na alimuelejea hii mambo wa ajabu.

Mtakatifu Venediktos alimwaambia ya kama hii muujiza alifanya Mungu kwa ajili ya utii ya mtoto ya roho yake. Lakini mutawa Mavros alimusema ya kama sababu ya hii muujiza ilikuwa amri ya padri mkubwa yake.

Katikati ya hii mazungumuzo yao aliingia na mutawa Plakidas, aliyeokolewa na alisema:

-Hile saa maji ilinikokota ndani na kati ya kiziba, nilisikia ya kama yulu yangu ilikuwa nguo ya padri ya roho yangu na tena nilisikia ya kama huyu atanitosha ku maji.

## Mtu moja na jina lake Tzalas wa inchi Gotthia

Alikuwa mtu moja wa inchi wa zamani Gotthia aliyeitwa Tzalas. Huyu alikuwa mukristu, lakini alifata imani ya uwongo. Huyu, hile wakati alikuwa mfalme ya Gotthia Totila, alichukia wapadri wakubwa ya Kanisa yetu Orthodokse. Vile, kama alikuta padri moja ao mutawa, alimupika na kisu yake na alimuua.

Siku moja alikuta mtu moja wa mukini na alianza kumupika nguvu. Huyu mtu wa mukini, kwa sababu hule munyanganyi alimuomba makuta, alimwaambia ya kama makuta yake anaichunga padri mkubwa mt. Venediktos.

Basi, Tzalas, alisimama kumupika, alimufunga mikono yake mukongo, alimuweka mbele ya punda yake, alimusukuma juu ya kumupeleka kwa padri Venediktos. Huyu mtu wa mukini alimupeleka hule mtu mubaya mu monasteri ya mt. Benediktos. Pale walimutafuta padri, aliyeikaa mbele ya nyumba yake na alisoma kitabu moja. Mtu wa mukini alipindula kwa mtu mubaya na alimwaambia:

-Tazama, huyu ni padri Venediktos.

Munyanganyi alimuangalia na richo ukali mt. Venediktos, kwa sababu alizania, ya kama atamuogopesha. Alipaza sauti alimusema:

-Simama mara moja na leta makuta ya huyu mtu wa mukini.

Hiule saa padri alinyanyua ma macho yake ya kitabu, alimuangalia munyanganyi na kisha mtu mwingine wa mukini, aliyekuwa ya kufungwa na kamba mikono yake mukongo yake. Na o, muujiza wa ajabu! Wakati alimuona padri Venediktos huyu mtu wa mukini, mara moja monyororo ilifunguliwa na ilianguka chini!

Mukuona hule munyanganyi mtu wa mukini kusimama bila monyororo, alimubabmba tetemeko na woga; alianguka chini, alipika magoti mbele ya Mtakatifu na alimuomba baraka yake.

Mtakatifu hasikusimame hata kidogo ya somo yake, lakini aliita wa ndugu wake na aliwaambia kutayarisha chakula kukula huyu munyanganyi. Na huyu mtu mubaya alisikia kosa yake, alisikia shauria ya mt. Venediktos na aliondoka ya monasteri bila kuomba makuta ya hule mtu wa mukini.

## Maombi ya dada moja

Mt. Venediktos alikuwa na dada moja katika mwili, aliyeitwa Skolastiki. Na huyu alifata uzima ya utawa tangu kipimo kidogo yake. Tena mara moja kila mwaka alizombelea aende kuona na mkubwa ndugu yake na huyu padri Venediktos aliendа amukute mu nyumba moja, inje na karibu ya monasteri yake.

Siku moja alifika Mtakatifu, katika zoezo yake karibu ya dada yake pamoja na wanafunzi wake. Siku muzima walipita pamoja naye, walisoma vitabu ya roho, walisoma Madiko Takatifu, ilikuja magaribi na waliikaa wakule. Hile saa walikula na waliendelea zungumuzo ya roho, dada yake alimuomba:

-Usiniache, ndugu wangu, hii usiku kuwa huku mimi mwenyewe. Ninapenda kusuburia mpaka asubui juu ya mafundisho ya roho na uzima wa milele.

Mwenye heri ndugu mkubwa yake alimujibu:

-Sauti nini unasema sasa?  Misiweze mimi kulala inje ya chumba yangu.

Inje muda ilikuwa safi na ukimya na pepo hakuna. Huyu mtakatifu dada yake, kwani mkubwa yake alikataa kuikaa pale usiku muzima, aliweka mikono yake pa meza, alinamisha juu yao kichwa yake na alimuomba kwa Mungu.. .  Wakati alinyanyua kichwa yake ku meza, ilianza inje pepo nguvu na nvula na umeme munene kabisa. Padri Venediktos na wa ndugu wake hakuna namna kutoka ya hii nyumba.

Mukuona hii mambo Mtakatifu, ya kama hakuna namna kurudia kwake, alitaabu na alisema kwa dada yake:

-Mungu akuhurumie. Ulifanya nini sasa weye na sala yako?

Na hule alimujibu:  Tazama, nilikuwaambia kuikaa kwangu na ulikataa. Nilimuomba kwa Mungu, basi, na Bwana wangu, alinisika. Sasa, kama unaweza, toka inje.

Hule hasikutake ambakie, lakini na hasikuweze atoke. Hivi alibakia karibu yake. Walipita pamoja usiku moja na walijaza ma roho yao na mafundisho ya Mungu.

## Uwili isiyozala watoto

Mtakatifu askofu Theodoros wa Sikeotis (+613) alimutembelea patriarki mkubwa ya muji Konstantinopoli. Pale alikuwa shemasi moja aliyeitwa Sergios. Huyu alikuwa na binti moja tasa. Alimuchukua huyu na bwana wake na aliwaweka chini ya mugazi ya nyumba ya patriarkhie, Tena alisema kwa shemasi ya mt. Theodoros, jina lake Yoano, hile saa ataondoka Mtakatifu, amuwaambie ashuke paka na hii mugazi.

Na vile ilifanyikwa. Shemasi Sergios alileta uwili wa tasa mbele ya mt. Theodoros. Walianguka mbele yake na walimuomba awapatia baraka yake juu ya kuzala mtoto. Halafu hule aliwaambia:

-Hapana kwangu, lakini mukimbilie kwa Mungu na Huyu atamitimiza maombi yenu.

Lakini, kwa sababu walikataa kusimama na kuondoka, Mtakatifu alibeba misipi yao wa wili. Aliiweka ma fasi ya kuachana, alipika magoti katikati yao na aliwabariki na kisha aliwapatia afungu mwili yao. Na neema ya Mungu kisha miezi tisa walizala mtoto moja mwanaume.

## Mutoni wa uharibifu

Mawingu moja kila nyakati ilikujaka pa mukini Skudri ya Asia Kidogo na ilinesha maimbwe mengi pempeni ya milima yote. Tunda ya hii mambo ilikuwa ya kama mutoni moja ilijaza na maji na kila wakati ilikuwa hatari kuharabisha manyumba ya watu na ma shamba yake.

Muda moja ilinesha maimbwe mengi kuliko ya nyakati iongine. Hivi hii mutoni ilijaza na maji na ilianguka pa mukini!  Pa njia yake ilikokota ma nyumba kipande moja ya mukini pamoja na wanaume, wanawake na watoto na watoto wadogo!  Tena ma nyama mengi walitembea pa

maji. Ilikuwa onekano moja matata na wa sikitiko nyingi!  Mtoni ilitelemusha hii vitu vyote na iliwapeleka ndani ya mutoni ingine munene jina lake Sagaris, pasipo hata kitumaini.

Basi, wakati ilisimama hii mateso, wale watu waliishi, walienda na machozi kwa mtaaktifu Theodoros wa Sikeotis na walimuomba aende pa hile fasi mawingu ilinesha maibwe kila wakati.

Mtakatifu alimuomba kwa Mungu na aliweka msalaba moja pa hile fasi ilinesha maimbwe. Tangu hile siku haikufike hata mawingu moja pa hii njimbo!  Kama, kila waakti, ilinesha nvula ao teluji, mutoni haikujaze hata na hakuna hasara moja mu mukini.

## Mupito ya Yordani

Mtakatifu mutawa Maria wa Misri, mbele ya mwisho yake alielejea uzima yake kwa mutawa Mt. Zosimas. Ku mwisho ya sauti yake alimuomba hivi:

-Padri Zosima, kila sauti nilikuwaambia sasa usitaseme mpaka lufu yangu. Uende sasa na mwaka kesho usipite mutoni Yordani, katika zoezo yako. Mbakia mu monasteri yako, kwani, kama utataka kutoka, hautaweze. Kama itakuja Mu Kazi Inee Mkubwa, chukua ma Fumbo Matakatifu, pita mtoni Yordani na uniongojee pale, kwa sababu, tangu hile wakati niliingia mu jangwa (mbele ya miaka 40) misikupewa Mwili na Damu ya Kristu!

Hivi alisema Mutawa Maria na alikimbia mu jangwa. Mtakatifu Zosimas alishituka juu ya zawadi ya kujua Mt. Maria matendo mbele ya kutimizwa. Kisha alipika magoti, alibusu hii fasi aliisha kusimama Mt. Maria na alirudia mu monasteri yake.

Mwaka kesho alitaka atoke inje ku monasteri yake padri Zosimas, lakini kwa ajili ya ugonjwa moja, asikutoke mu jangwa ya ma siku makumi inne hile wakati ya Kwarezima, katika zoezo yake. Alikumbuka ma sauti ya mt. Maria. Na mu Kazi Inee Mkubwa alibeba Kikombe Takatifu na Mwili na Damu ya Kristu, matunda madogo, mahalaki na alikaribia mutoni Yordani.

Saa ilitembea mbio na Mtakatifu Maria bado kuonekana. «Lakini namna gani atapita mutoni?  Vile aliuliza maungo yake padri Zosimas, kwa sababu hakuna mutubwi. Vile aliwaza na kwa rafla alimuona akuje mt. Maria!  Ilikuwa usiku lakini nuru ya mwezi ilikuwa nguvu. Mt. Maria alifanya alama ya Msalaba na mara moja alikuwa pa ngambo ingine ya mutoni!  Mt. Zosimas alishituka. Alinamisha kichwa yake juu ya kumusujudu.

-Padri, Zosima, alimwaambia Mtakatifu Maria, unafanya nini sasa?  Unakamata pa mikono yako VItu Vitakatifu, Mwili na Damu ya Kristu, na unataka kupika magoti yako mbele yangu? Weye unibariki.

Kisha alimuomba kusema:   «Baba yetu uliye mbinguni.. .  » na «Nasadiki Mungu moja.. . » na alikomunika. Kisha alifanya  sala kidogo, hii:  «Sasa umuacha mutumishi wako, ee Rabi.. . ». Kisha alipindula kwa mt. Zosima na alimuomba hivi:

-Ee Padri, kama ni ubarikiwa, uende sasa mu monasteri yako na mwaka kesho kuja kunikuta pa hile fasi uliniona mara ya kwanza.

-Mutumishi wa Mungu, alimujibu padri Zosimas, mi si ninakuwa mustahili kukufata. Lakini beba hii chakula nilikuletea.

Hile saa Mtr. Maria alifungula mukono yakena alibeba ma begu tatu ya mahalaki, alifanya alama ya Msalaba na alipita mtoni Yordani, sawa alifanya ku mkongo!  Padri Zosimas alimuona na musagao na aliondoka na yeye arudie mu monasteri yake.

## Chetezo moja mupya

Mtakatifu askofu ya Argos, muji ya Grekia, jina lake Petros, alitaka kumufukuza mutawa mt. Theodosios, kwa sababu aliisha kusadiki ma sauti mabaya na wa uwongo kupingana yake!

Usiku moja alikuja kwa ndoto ya askofu mt. Theodosios na alimwaambia ya kama ni musiyekosa. Mt. askofu Petros, alitubu na aliondoka juu ya kumukuta. Alitaka kuomba hurumia,

kwa sababu watu wabaya walimuchukia mt. Theodosios na walisema ma sauti ya uwongo kwa askofu ya hii njimbo.

Mt. Theodosios alijua ufikisho yake, mbele ya kuja mt. Petros! Aliweka makala ya moto ndani ya nguo ya kofya yake (kukuli), alibeba ubani na alitoka inje juu ya kumupokelea askofu Petros.

Wakati hule askofu alimukaribia, mt. Theodosios aliweka ubani pa makala ya moto. Nguo meushi ya kofya yake, haikulungua hata kidogo! Na hii chetezo wa ajabu alimufukiza mt. Theodosios askofu Petros. Na ma fasi pempeni ilizambalishwa harufu muzuri.

Askofu mukuona hii muujiza wa ajabu, alishuka ya punda yake na alikaribia mt. Theodosios. Huyu aliacha kukuli na alimuweka metania (kupika magoti mbele yake). Mt. Petros alimubusu, alimuomba hurumia juu ya hii mawazo mabaya alikuwa na ndani ya akili na kupingana yake.

## Kazi wa muujiza ya kulopola samaki

Mu kikavu ya muji Kalkidona, muji ile ni karibu ya Konstantinopoli wakati moja mu milele wa tisa walikuwa wavuvi na walilopola samaki. Pa hile fasi aliishi na mutawa Lukas wa Nguzo (879-980). Wavuvi walichoka ma siku mengi, bila lakini kutosha hata kintu. Walirudia ma nyumbani yao na sikitiko, bila samaki ya ma siku mengi.

Mtakatifu siku moja aliita mkubwa yao muvuvi na alionyesha ya kama asijue mateso yao. Basi, alimuuliza:

-Juu ya nini ya wakati mingi mpaka sasa usikunileteе hata samaki moja?

Hule alimujibu na malako ya kama wanakombana ma siku mengi na hawabambe kintu na wanasikitika kwani hakuna na mukate yao.

-Usipotee nguvu na kitumaini yako, alimushauria mt. Lukas. Mbio-mbio Kristu ataleta hasira ya ma samaki mengi ndani ya makila yenu.

Kisha alibeba chupa moja na maji, aliibariki na alimupatia kwa hule muvuvi. Tena alimupatia na nguo moja na hile alisafisha mikono yake. Alimuhamuru kumimiya na maji ma makila yao na watafunga hii nguo mueupe mu fasi ya kona yao. Ku mwisho alimuhamuru amuletee samaki 1/10 kwake. Alimupatia na unabii ya kama watamuletea karibu ma samaki makumi tatu (30).

Sauti yake ilitimizwa kabisa! Wakati walimimiya makila na walifunga hii nguo meupe ya kona yao kundi moja ya ma samaki karibu 300 walibambwa pa makila. katika amri yake walimupatia 30 samaki.

Kisha mt. Lukas aliwaambia na mara ingine: Mwende mu kazi yenu. Ndani ya makila yenu mutapate na ma samaki ingine. Mutaniletea kwangu 1/10. Walienda hwa mbio na furaha nyingi waliisha kubamba mpaka ma samaki 400. Lakini walikataa amuletee 1/10, nikusema ma samaki makumi inne. Walimuletea paka 15 ma samaki. Hile saa mt. Lukas aliwafokea na namna ukali:

-Mimi nilimiambia muniletea kwangu 1/10, lakini mweye muliniletea paka 1/30. Kwa hivi leo, sawa na zamani, hamutabambe ma samaki ingine! Basi, sasa mutaenda kuuzisha hii samaki mulibamba na kisha mutaenda huku nyumbani yangu na mutakula hii samaki mulinipatia. Na mutamushukuru Mungu, aliyemupatia hii baraka ma jamaa yenu.

Tangu hile wakati wavuvi, kama walikuwa na ugumu mu kazi ya kulopola samaki, walienda kwa mt. Lukas na imani. Na hule aliwapatia waakti ingine maji ubarikiwa na waakti ingine mukate ubarikiwa na wale waliiweka katikati ya makila yao sawa kintu ya chakula yao na vile walikuwa na baraka munene.

## Wokovu ya mtoto mudogo

Baba moja na taabu mingi alikuja nyakati moja kwa mt. Mutawa Luka wa Stilitis (wa nguzo) na alimuelejea teso yake:

-Tulilala pa kitanda yetu na tulikuwa na mtoto yetu katikati. Lakini, wakati tulilamuka, mtoto alikuwa pa kitanda pasipo kupumuzi. Tulisikitika sana na tulikuja kwako kuomba saidio yako.

Na huyu mupendwa wanadamu mtakatifu, alifata mapendo ya Kristu. Aliwamuru kuikaa na kukula pamoja pa meza moja. Hile saa hawa uwili walikula, mt. Luka alifanya sala kwa Bwana ya uzima na lufu.

Wakati Mungu alimutangaza ya kama alisikia sala yake, aliwaita na aliwaambia:

-Mwende na furaha na shangilio nyumbani yenu. Musiwe hata shaka moja juu ya wokovu ya mtoto yenu na musiteswe hata na sikitiko moja.

Walisadiki ma sauti ya mt. Lukas na walienda mbio mbio kabisa nyumbani yao, pahali walipata mtoto yao muzima na alicheza wa furaha.

Walirudia mukongo kwa Mtakatifu juu ya kumushukuru na kumutukuza pamoja Mungu juu ya hii muujiza yake.

## Namna gani ilitoka maji takatifu

Wakati mutawa Mt. Athanasios wa Kilima Takatifu (Athonitis) alianza kujenga Monasteri yake Lavra ukubwa, aliona ya kama makuta, vitu ya vyakula na vitu ya majengo ilikuwa karibu ya mwisho. Hakuna makuta juu ya kuripa wajengaji. Hakuna kintu ya kupika chakula. Alipotesha kitumaini yake. Alisimamisha kazi na aliondoka kuenda mu muji Karies ya Kilima Takatifu.

Kisha mwendo mu njia ya ma saa wa wili, alionekana pa njia mwanamuke moja mkubwa, aliyemwambia na namna ukali:

-Ee padri Athanasios, unaenda wapi? Juu ya nini uliacha hii kazi ulianza? Rudia mukongo kuendela kazi takatifu na kimungu yako.

Mtakatifu Athanasios alishituka juu ya onekano ya mwanamuke moja ndani ya Kilima Takatifu *(Inapashwa kujua sisi ya kama inakatazwa kuingia hata mwanamuke moja ndani ya Kilima Takatifu, pahali wanaishi watawa wa Orthodoksi karibu 2000).* Na alimuuliza na mustari yake:

-Nani uko weye? Namna gani unamifamia? Namna gani unajua jina yangu na unanihamuru nirudie kwangu? Na ma vitu ma nani na namna gani nitaendelesha kazi yangu, kwani vitu vyote iliisha kuisha?

Hile saa Hule Mama alimwaambia ya kama ni Mama ya Bwana Yesu kristu na inapashwa arudie kwake kuisha kazi ya kujenga monasteri yake. Atapata ma nyumba yote ya kujaza namafuta na ma chakula ya kuachana na fasi ya makuta itakuwa mengi na kila kintu eko na lazima ataipata, kama atarudia mu monasteri yake.

Mtakatifu Athanasios juu ya kukikisha ya kama ma sauti yake ni wa kweli, alimuomba ya Mzazi-Mungu alama moja wa ajabu. Hile saa Mama Maria alimwaambia apike na bvakora yake njiwe moja na mara moja itatoka maji. Na kweli, waakti mt. Athanasios alipika njiwe moja, ilitoka maji utamu na inatunza wagonjwa wingi! Hii maji mpaka leo inaitwa «Maji Takatifu ya Mtakatifu Athanasios» na watu wingi wanakunywa na wanasikia muzuri sana.

Mtakatifu alisadiki ma sauti ya Mzazi-Mungu, alirudia mukongo na kweli alipata ma birika na ma sanduku ya kujaza na makuta na vitu ya kazi na chakula na kila kintu juu ya kuendelesha kazi yake.

## Kinywaji ubarikiwa

Mu milele wa kumi na moja (11) mu Rusia aliishi mkubwa ya ufalme moja aliyeitwa Izaslavos. Huyu alimupenda na alimuheshimiwa sana mt. Mutawa Theodosios wa Kievon. Mara

mengi alikujaka nyumbani yake juu ya kusikia ma neno na mafundisho yake ile ilikuwa sawa asali. Siku moja walichelewa na walisuburia mpaka magaribi. Huyu mkubwa, kwani ilikuja saa ya sala ya Njioni, aliingia mu Misa asikie Ibada. kwa rafla ilinesha nvula moja munene, katika mapenzi ya Mungu. Basi, mt. Theodosios alimuwaambia musaidizi yake atayarishe chakula ya usiku juu ya huyu mkubwa. Lakini huyu alimwaambia ya kama iliisha kuisha sali+ maji na hakuna kintu amupatie. Hii sali na maji pamoja walimupatia pa fasi ya vinyo, kwa sababu hile wakati hakuna vinyo.

-Mtakatifu alimuuliza:  Hakuna hata kidogo?

-Hapana, alimujibu mujukumu ya nyumba ya vitu ya chakula.

-Angalia mara ingine kama ilibakia hata kidogo.

-Unisadiki, padri wangu, ya kama hii tuku ilikuwa ya kupindula. Na ndani hakuna kintu.

-Uende na kwa jina ya Bwana Yesu Kristu, utapata, alimwaambia na kitumaini mingi padri Theodosios.

Wakati aliend pale huyu mutawa alipata tuku ya kusimama na ilikuwa ya kujaza na asali na maji!  Alishituka na hii muujiza an aliend amuwaambie hii jambo kwa mt. Theodosios.

-Mtoto wangu, funga kinywa yako na usisema kintu kwa watu wnegine. Tengeneza sasa meza na weka hii kinywaji na kwa ndugu wote, kwa sababu ni baraka ya Mungu.

Kisha saa kidogo nvula ilisimama na hule mkubwa aliweza atoke nyumbani yake. Hii kinywaji ubarikiwa ilikuwa ya wakati mingi mu monasteri yake na ndugu  wote waliipima mara nyingi.

## Mufalme mt. Simeoni mwenye kutosha manukato

Muyengeji ya monasteri Khilandarion ile ni mu Kilima Takatifu ni mufalme moja aliyekuwa mu inchi Serbia mu wakati (1114-1200). Huyu alicha cheo na kiti kwa mtoto mudogo yake na alimufwata mtoto mkubwa yake, jina lake Savvas na alikuja mu Mulima Takatifu kukuwa mutawa na kipimo yake miaka 55.

Kisha lufu takatifu yake alionekana na ono moja kwa mtoto yake mt. Savvas na utuklufu na eema mingi, kwani Mungu alimutukuza mbinguni!  Mt. Savvas alitaka na wengine wa ndugu yake ya inchi Serbia kutangaza utakaso ya baba yake na kwa hivi alimuomba Mungu mwili ya baba yake atoshe manukato!  Huyu mt. Savvas alikuwa na uwezo mingi mbele ye ya Kristu na aliomba kila kintu, bila shaka.

Basi, kwa ukumbusho ya baba yake aliita na mkubwa ya Mulima Takatifu (Protepistatis) na wakubwa wapdri ya ma Monasteri ingine na wapadri wengine. Kwa ajili ya hii makumbusho yake walikuja mu monasteri ya Khilandarion waaminifu wingi. Kanisa na kaburi yake walikuwa ya mapambo mazuri. Tangu magaribi waliimba pa kaburi yake wimbo ya makumbusho yake. Kisha chakula ya usiku, mt. Savvas aliend kwa mkubwa ya Kilima Takatifu na alimwambia waende mu Misa. Kule alimwaambia:

-Ee Padri mtakatifu, mimi pamoja na waaminifu wenye inchi yangu Serbia, nitaenda mu mnara ya monasteri, pahali ni kanisa kidogo juu ya kufanya mu lugha yetu slavona ibada ya asubui kesho. Lakini mweye wa aminifu wa inchi Grekia (Hellas) mutambakia ndani ya hii kanisa munene na mutafanya Ibada ya asubui mu lugha yenu na kisha ibada ya wafu juu ya baba wangu. Mumuombe kwa Mungu, apumuzike na baba yangu. Wakati Mungu atatukuza mutumishi wake, (mt. Simeoni) mutaniita na mimi na nitakuja mbio.

Waliondoka inje ya kanisa. Alifunga kanisa na alipatia funguo kwa mkubwa ya Kilima Takatifu. Mkubwa ya Kilima Takatifu hasikusikie sauti ya mt. Savvas na alimujibu:  «Mapenzi ya Mungu uje». Kisha aliend mu chumba yake kupumuzika. Mt. Savvas alianza tangu usiku ibada ndani ya kanisa kidogo ya mnara. Aliomba na machozi toka Mungu ufanyike hivi mapenzi yake:

-Ee Bwana Wema kamili, unisikie mimi mwenye zambi, ninakuomba mara ingine. Patie neema mingi kwa mifupa takatifu ya baba wangu, iliyeteswa na ilijikauka na kifungo juu ya mapendo yako. Uijaze hii Mifupa na manukato yako juu ya kubeba sisi wote barako yako na kukutukuza kwa kuona rehema yako. Vile tutapatra fundisho ya kama unatukuza hawa watu waliacha vitu vyote vya dunia na walikufata na walikuwa na kitumaini na mapendo kwako. Amina.

Asubui, hile saa ya ibada ya Asubui watawa wa greki pamoja na muklubwa ya Mulima takatifu walifanya sala yao na walimukumbusha na mutawa Simeoni, kwa rafla kanisa yote ilijaza na manukato ya neema ya Roho Mtakatifu! Ma nafsi yao yote ilijaza na furaha, amani, utamu na waliuliza namna gani ilikuja hii manukato?

Ninyi wote walikuwa karibu ya kaburi ya mt. Simeoni walisikia sawa bikelele moja kutoka ya ndani. Waliangalia muzuri na waliona njiwe hile wa yulu ya kaburi iliisha kujaza na manukato! Walishangaa sana! Walisimama Ibada na walkiimba: «Bwana hurumia»!

Hile saa mkubwa ya Mulima Takatifu alikumbuka sauti ya padri Savvas, hivi: «Wakati Mungu atatukuza baba wangu, mutaniita na mimi», na mara moja alimuita ashuke ya mnara. Mt. Savvas a;ishuka na furaha toka mnara na waakti aliona hii jambo ya ajabu alimutukuza Mungu. Alibatia kaaburi ya baba yake na alimubusu sawa alibusu mwili ya baba yake na alimuwangisa na machozi yake!

Mkubwa ya Mulima alibeba manukato na alimimiya ya kwanza mtr. Savvas, mtoto ya mt. Simeoni na kisha watawa wote. Wale wagonjwa waliteswa na magonjwa ya kuachana, walitunzwa, hile waakti waliwamimiya na manukato ya mt. Simeoni. Manukato ilitokea hapana toka kaburi yake, lakini na toka Picha yake iliyekuwa yulu na pempeni ya kaburi ya mt. Simeoni.

Mt. Savaas kisha aliweka manukato ndani ya chupa moja na aliituma mu mudogo ndugu yake, aliyekuwa mufalme ya inchi yao Serbia, jina lake Stefanos, sawa baraka ya padri yao.

## Majengo ya Monasteri ya Simonopetra mu Kilima Takatifu

Mtakatrifu Mutawa Simon wa Mirovlitis (wa kutosha manukato) aliishi mu (milele 14) na aliisha ndani ya pango moja mu pori. Pale alikombana shetani na umaskini na mateso mengi. Kwa hivi na Mungu alimupatia zawadi ya hekima na ufafanusho ya Madiko Takatifu. watu wingi walikujaka kwake juu ya faida ya roho. Hule, basi, kwani matembeleo ya watu walimuuzi, aliwaza kutoka mbali na ndani ya jangwa.

Lakini Mungu, aliyetengeneza faida ya watu, hasikumuache atoke jangwani. usiku moja, hile saa alimuomba kwa Mungu, pango yake ilijaza na nuru kimungu! Mt. Simoni alisikia na shangilio wa roho na harufu. Alisikia na sauti moja ilimwaambia:

-Ee Simoni, Simoni, rafiki muzuri na mutumishi wa Mwana wangu, usitoke! Nilikuweka huku juu ya kuwa weye nuru ukubwa na utatukuza hii fasi.

Simoni munyenyekevu, hasikusadiki ma sauti ya Mzazi-Mungu Mama Maria. Aliogopa ya kama ilikuwa mutego ya adui shetani, mwenye, katika Agano Jipya, anaonekana sawa «malaika ya nuru». Kwa hii neno, aliendelea kupenda atoke jangwani. Halafu usiku moja aliona ono moja wa ajabu: Aliona ya kama ilishuka toka mbingu nyota moja na ilisimama pale ni sasa monasteri yake Simonopetra. Hii ono aliona na ma usiku ingine. Lakini juu ya woga yake hasipende kusadiki ya kama ilikuwa ono ya Mungu, kwani alizania ya kama ilikuwa mutego ya shetani.

Usiku ya Siku Kuu ya kuzaliwa Kristu, hasikuone paka nyota ushuke na ushimame pa njiwe moja murefu, lakini alisikia na sauti kimungu mara tatu:

-Ee Simoni, Simoni, huku unapashwa kujenga monasteri yako kusudi kuokoa nafsi yao! Mimi nitakuwa musaidizi yako. Sopoka, lakini, usishake, kwa sababu utapata kintu kibaya kinene.

Mtakatifu Mutawa Simoni alisikia woga na furaha. Aliwaza ya kama ilikuwa mu Bethlehem, ya kama aliona wachungaji pempeni ya Mtoto Mtakatifu Yesu Kristu, Mzazi-Mungu

Mama Maria na Yosefu mwenye haki.. . alizania ya kama alisikia na shangilio wimbo ya malaika: Utukufu kwa Mungu juu pia.. . . »

Kisaha ma siku wa wili tatu walifika vijana wa tatu na walimuomba kumbaki kwake na wafate uzima ya utawa. Mt. Simoni ku mwanzo alikataa. Kwa sababu, lakini, wale walimuomba bila kutoka, aliichika na aliwaweka ndani ya kundi ya watawa wake. Kisha wakati ingine aliwafufunusha ono yake takatifu sawa aliona mara ingine uzalio ya Bwana yesu Kristu. Aliwaambia:

-Watoto wangu, ninasadiki ya kama huku alimituma Mungu, hapana paka kusudi kupata wokovu yenu, lakini juu ya kusaidia tujenge sisi monasteri yetu. Basi, mwende kupata wajengaji.

wakati wa ndugu walipata wajengaji na mt. Simoni aliwaambia hiole fasi kusudi kujenga monasteri, wale walikataa, kusema hivi:

-Ee Padri, unasema nini? Unasema kweli ao kwa bure? Hii fasi ni wa hatari na sisi na kila mtu ataikaa huku iko mambo ya kuanguka chini na akufe.

Mtakatifu Simoni alisikia ya kama paka na ma sauti yake hakuna namna kuanza kazi yao. Ilikuwa lazima na moja tendo kitakatifu.. . .

Alisema kwa wanafunji wake kutayarisha meza juu ya kula wote pamoja. Lakini mutawa moja, hile saa alipitisha pempeni ya watawa wengine awakabula vinyo, alipotesha nguvu yake na alianguka kutoka chogo ya njiwe chini. Hile saa alikamata chupa ya vinyo pa mukono ya kuume na kopo pa mukono ya kushoto.

-Unaona? walisema wajengaji kwa padri Simoni. Weye sasa ulikua sababu na mutawa moja alikufa! Lakini, kama sisi tutaanza kazi ya kujenga, unawaza wa ngapi watu watakufa?

Mt. Simoni aliomba kwa siri. Alimuomba kwa Mzazi-Mungu awasaidie. Watawa wengine walienda chini kutafuta hule mutawa aliyeisha kuanguka chini. Walizania ya kama watapata vipande vipande ya mwili yake. Kwa rafla, walimupata arudie kwao na kukamata pa mikono yake chupa ya vinyo na kopo, bila hata kilonda moja! .. .

Wakati waliona hii muujiza wajengaji walishituka na walianguka mbele ya miguu ya mt. Simoni na waliomba hurumia. Kisha bila shaka walianza kujenmga monasteri inayeitwa toka jina ya mt. Simoni Simonopetra, ni kusema Monasteri pa njiwe ya mt. Simoni.

## **Ndege ya mbingu**

Mtakatifu mutawa Maksimos wa Kafsokalivis alijaza na ma zawadi ya Roho Mtakatifu. tena alikuwa na zawadi ingine, na hii haiko na watakatifu wengine. Huyu aliluka pa pepo! Hasikukuwe paka ndege ya Mungu kwa ajili ya uzima takatifu, umaskini na kifungo na sala mingi, lakini kweli aliluka pa pepo! Aliluka kutoka fasi moja kwa mwingine! Miili sawa mwili yake, kwani wekona neema ya Mungu mingi, ni mapepeo, sawa kuwa bila nyama na haina lazima ya mabawa. Mabawa yao ni Neema takatifu na Hii ni ribawa kimungu, wa malaika!

Mutangazi ya hii jambo wa ajabu alikuwa mwandishi ya uzima wake, aliyekuwa askofu, jina lake Theofanis. Huyu aliandika hivi:

«Siku moja niliondoka toka Monasteri ya Vatopedion na ndugu mwingine kusudi twende nyumbani ya hule Mutawa Maksimos wa Kafsokalivis. Lakini, bahati kibaya, misikumupate kule. Nilitaabu na nilitafuta kule pempeni kusudu kumupata. Nilirudia mara ingine mu nyumbani yake na hile saa niliangalia njia ya bwana Isaya, tazama, nilimuona mbali ya 3, 5 kilometre. Nilimuona kuluka pa pepo, sawa ndege! Aliluka sawa kwazi kibeba kuku yulu ya pori na ma njiwe na alikuja kwangu!

Hile saa niliogopa na nilipaza sauti niseme: Ee Bwana uwe Mkubwa.. . » na juu ya woga wangu nilichofa kidogo mukongo. Huyu kisha dakika moja alifika kwangu na aliimba wimbo moja. Aliimba nini, misikuisikie, kwani nilikuwa na ushituko ya hii jambo ukubwa!

Nilianguka mbele ya miguu yake, nilimuweka metania. Hule aliniuliza ya kuendelea:

-Ma saa ma ngapi uko huku?

Kisha alinikamata mukono yangu na mapendo sawa baba ya roho na aliniweka ndani ya nyumba yake. Pale alinifundisha, alinishauria na ku mwisho aliniambia:

-Sopoka, usiseme hata kintu kimoja kwa mtu mwingine mpaka mwisho ya uzima yangu. tena sikia na weye ya kama siku moja utakuwa padri mkubwa ya monasteri na kisha askofu ya njimbo Akxrida! Mbele ya mwendo yako itakufwata mateso na majaribu mengi. Lakini fanya uvumilia na fata uzima ya Bwana Yesu Kristu, aliyesulubiwa pa Msalaba. Huyu atakuwa musaidizi yako pa majaribu, ma taabu na mashindani yako wa magumu.

Na kweli hii ma nabii yote aliniambia ilitimizwa wote, sawa huyu aliniambia».

## Ufufuo ya mtoto

Ma fasi pempeni ya monasteri Lavra ya Utatu Mtakatifu, mu muji Zagorski ya inchi Rusia aliishi mtu moja aliyechunga ndani ya roho heshima na mapendo mbele ya mujengaji ya hii monasteri, kwa mt. Sergios wa Rantonezi. Mtoto wa pekee ya hule mtu aliteswa na ugonjwa moja, wa bila tunzo. Kwani alitumainia tunzo ya mtoto yake alienda kwa mt. Sergio pamoja na mtoto mugonjwa wake. Lakini kwa ajili ya muchoko ya mtoto yake pa njia, huyu alikufa! Baba yake alipotesha kila kitumaini na alianza kulia. Alisema kwa mtakatifu:

-Ole kwangu! Nilikuja huku na ukikisho ya kama utanisaidia, lakini mtoto wangu wa pekee alifariki pa njia.

Baba yake na machozi mengi na maombolezi alienda alete sanduku na manguo juu ya Kiliyo ya mtoto wake. Mtakatifu alimutaabu. Alifanya sala mingi na alimufufusha mtoto wake! Wakati baba ya mtoto alirudia toka muji, pahali alienda kununua vintujuu ya kiliyo, mtakatifu alimwaambia:

-Usichoke na usiomboleze bila haki. Mtoto yako hasikufe, lakini anaishi!

Baba, mwenye alijua ya kama kweli mtoto yake alikufa, hasikuweze kusadiki ma sauti ya mt. Sergios. Halafu, alikaribia, alisadiki na furaha mingi alimushukuru Mtakatifu.

-Usilande akili yako, alimwambia hule. Kwa ajili ya baridi mingi huyku, mtoto yako alionekana sawa mufu, lakini hapa ni kivukutu na mtoto yako ni muzima.

Baba yake hasisadiki hii uwazo ya Mtakatifu Sergios. Alisadiki ya kama kweli mtoto yake alikufa na mt. Sergios alimufufusha katika sala yake. Mt. Sergios alimuwaambia na namna ukali juu ya kufuchika fazila na unyenyekevu yake:

-Simama kusema kwa watu wengine ya kama mimi nilifufusha mtoto yako. Usiseme hivi, kwa sababu utapotesha mtoto yako!

Baba yake alirudia nyumbani mukutukuza Mungu na mtumishi wake padri Sergios. Kisha nyakati ingine alielejea hii muujiza kwa mwanafunji moja ya mt. Sergios na huyu kisha aliilejea kwa watu wengine.

## Zahabu wa uwongo

Shetani alioyechukia kila kazi kizuri, alipima kuangusha mtakatifu Matrona wa Kisanga Khios (+1462) kwa hii majaribu: Hile wakati walifungula wajengaji masingi ya kujenga kanisa moja, kwa rafla walipata zahabu moja munene!

Iko namna shetani muovu alitaka kuangusha mt. Matrona mu jaribu ao ya upenda-feza ao mu majivuno, nikusema, ilikuwa namna kuwaza na kusadiki ya kama alifika mu cheo yulu ya fazila na kwea hivi Mungu alimutuma hii zahabu.

Halafu, Mtakatifu hasikufurahi na hii zahabu, lakini aliomba kwa Mungu na machozi na moto ya roho yake:

-Ee Bwana Yesu Kristu, kama hii zahabu ni ya Kwako, uniambie hivi. Lakini kama hii inatokea ya shetani, mara moja, ninataka kukimbia na kutoka.

Vile alisema na hii zahabu, mara moja ilifanyika makala meushi!

Hii muujiza ilipatia nguvu kwa Mtakatifu kusudi aendelea kujenga Kanisa.

## Muchele ya mkubwa wa Turkie

Mtakatifu Yoano wa inchi Rusia (1690-1730) alijibamba mutumwa mu nvita katikati ya Rusia na Turkie mu mwaka 1711 na alijiuzisha kwa mkubwa moja wa inchi Turkia aliyekuwa toka muji Prokopion ya Azia Kidogo (Turkie).

Mkubwa yake, aliyekuwa muslimani, alimupenda Yoano, mutumwa wake. Siku moja alikamata mpango aende mu muji «takatifu» yako Meka, hile ni mu inchi Arabia juu ya kubusu njiwe moja, hile wanasadiki mataifa ya dini wa umuslimani ya kama hii njiwe ilianguka toka mbingu.

Kisha ondoko toka nyumba yake, bibi yake alifanya muchele nyumbani yake na aliita wale aliwafamia na ma rafiki wake wakule pamoja juu ya kufurahi na kutakia kwa kurudia ku mukongo muzuri bwana yake, kisha safari yake mu muji Meka ya Arabia. Pempeni ya ma chakula ya mbali-mbali bibi yake alipika na muchele, hile wanaipenda sana watu wa mashariki. Alikumbuka bwana yake, kwa mwenye muchele inamupendeza sana na alisema kwa musaidizi yake Yoano:

-Yoano, kama mkubwa yako atakuwa huku, ataweza kula hii muchele na ataweza kusikia furaha mingi!

Hile saa hule aliomba ya mkubwa mama yake sahani moja na muchele na alimuwaambia ya kama huyu ataituma kwa mkubwa yake mu muji Meka! Kwa hii sauti yake wale walikuwa pa meza walicheka sana, kwani walizania ya kama huyu mutumwa alitaka akule yeye wa pekee hii muchele ao, alitaka aipatia kwa jamaa moja umaskini sawa vile alifanya na chakula yake kila siku. Mama mkubwa alisema kwa musaidizi mwanamuke amupatie sahani moja na muchele nyeye (Yoano) atafanye hile kintu yeye aliipenda.

Mtakatifu Yoano alichukua sahani, alishuka nyumbani ya ma nyama ya mkubwa yake na, katika zoezo yake, alianza kuomba kwa Mungu juu ya kuituma kwa mkubwa yake mu muji Meka. Aliacha, halafu na sahani, pale karibu na alianza sala kwa kusimama pa nyasi ya kukauka. Mungu, mwenye anasikia sala ya wale watu wa upole na unyenyekevu, hasikuzarau na sala ya mutumishi wake kijana Yoano. Mt. Yoano aliomba afanye Mungu hii muujiza juu ya kuonekana utukufu ya Im, ani Orthodokse mbele ya wale walifata dini ya umuslimani, dini ya uwongo kabisa. Aliomba kutukuzwa Kristu na hapana yeye mwenyewe! Hii maombi inafanyika na roho unyenyekevu na kusudi kimungu, Mungu anaisikia na anamaliza mapenzi ya watumihsi wake, kweani anataka kusaidia wokovu ya watu wingi.

Kisha sala ya mt. Yoano, sahani na muchele ilipotea mbele ya ma macho yake! Kijana Yoano, alifurahi na alimushukuru Mungu. Alirudia pa meza na alisema kwa mama mkubwa yake ya kama alituma muchele kwa mkubwa bwana wake! Mukusikia hii ma sauti yake wale walikuwa pa meza walianza kucheka mara moja. Hata moja hasikusadiki ma sauti yake, na walizania ya kama huyu alikula hii muchele.

Kisha ma siku madogo walishangaa hawa watu. namna gani walishagaa? Alirudia huyu mkubwa toka Meka na aliwaambia ya kama alichukua ndani ya nyumba yake sahani yake na muchele. Hivi alisema:

-Mu tarehe siku fulani ya hii mwezi, aliwaambia, na ilikuwa siku ya chakula yao mu nyumba yake, nilirudia toka tzamia (hekalu) mu chumba yangu ya muji Meka. Wakati nilifungula mulago ya hile nyumba, niliona na musagano pa meza yangu sahani moja na muchele ya kivukutu. Nilifokea kwa Mungu: Ee Alah, Alah, nani alileta hii muchele ndani ya nyumba yangu, lakini mlango ilikuwa ya kufungwa? Nilikaribia kuiangalia muzuri sahani na nilishituka sana! Nilifokea kwa Mungu: Ee Alah, Alah, hii sahani ni toka nyumba yangu ya mukini Prokopi ya Turkie, kwani iliandikwa na jina yangu pempeni yake! Niliikaa na nilikula hii

muchele, bila kufafanusha hii jambo ya ajabu. Kwa kurudia nilibeba na hii sahani juu ya kumionyesha hii jambo na mweye mutanielejea namna gani ilifika mu muji Meka.

Wakati walisikia sauti ya mkubwa yao, walishituka na waliangalia moja mwingine bila kusema neno moja. Hile saa bibi yake alimuelejea:

-Musaidizi yetu Yoano, aliomba hile saa ya meza yetu, sahani moja na muchele juu ya kuituma kwako mu muji Meka. Sisi tulimupatia na mucheko. Hakuna namna kusadiki ya kama yeye ataweza kuituma kwako na saidio ya Mungu wake!

## Safari wa ajabu

Mujengaji ya monasteri Mzazi-Mungu wa Onekano (faneromeni) ya Kisanga Salamina ya inchi Grekia (Hellas) alikuwa mtakatifu mutawa Lavrentios (+1770). Mbele ya kuwa mutawa aliitwa Lambros, alikuwa mulimanji na aliishi mu muji Megara pamoja na bibi yake Vasiliki, aliyekuwa kisha mutawa na jina Vasiani, na pamoja na watoto wao wa wili.

Hile wakati alikuwa tena mukristu laice, alipokelea ono moja toka Mzazi-Mungu, aliyemwaambia ajenge kanisa yake, iliyekuwa mu fasi moja ya Kisanga Salamina na iliisha kuharabika. Lakini huyu, kwani alikuwa munyenyekvu na mwenye akili, hasikusadiki hii Ono yake. Basi, Mzazi-Mungu Maria alionekana kwake na mara mbili na tatu na mara wa inne alimufokea ya kama, kama atakataa kujenga kanisa yake atamufanyisia kintu kimoja kibaya.

Basi, mukristu Lambros aliondoka ya nyumba yake, alishuka mu kikavu na aliona ya kama ilikuwa mawimbi, zoruba na tufani mingi mu bahari. Hakuna na chombo kusudi aende mu Kisanga salamini, ile ilikuwa mu ngambo ingine.

Hile saa aliikaa pa kikavu na aliwaza atafanya nini, alisikia kwa rafla sauti kimoja kimungu:

-Tupa gochi yako pa maji ya bahari, panda juu yake na utafika bila shaka mu Kisanga!

Na imani bila shaka Mukristu Lambros alifungula gochi yake, alipanda juu yake na alitelemuka ndani ya bahari na alifika muzima na bila mambo mu Kisanga Salamina!

## Sala wa pepo

Mtoto ya mfalme Ekaterini S. alikuwa na mwipwa moja aliyeteswa kwani alikonda, na hasikuweze kutembea. Basi, alimupeleka na kitanda moja mu nyumba ya mt. Serafimi wa Sarofi. Hile saa padri alisimama inje ya mulango ya nyumba yake sawa alimuongojea huyu mugonjwa. Waliingia ndani na alimusema:

-Furaha wangu, tutafanya pamoja sala na weye na mimi. Lakini sopoka! Utakuwa ya kularia pa kitanda na hautapindule mwili yako mu fasi ingine.

Huyu kijana alimbakia pa hile fasi mpaka ilipotesha uvumilia yake na alipenda kupindula pa hile fasi alikuwa mt. Serafim na alifanya sala. Basi, alipindula kichwa yake na alimuona mt. Serafdim, aliyeomba kwa Mungu, lakini mwili yake ilikuwa pa pepo! Hii onekano aliiona alishituka na alianza kupaza sauti.

Padri Serafim aliisha sala yake, alimukaribia mugonjwa na alimwaambia:

-Sasa, basi, utasema mbele ya watu wote ya kama Serafim ni moja mtakatifu na anaomba pa pepo! Sopoka, ninakuomba! Mpaka nitakufa hautaseme hata sauti moja. Kama utasema, utakuwa mugonjwa mara ingine.

Huyu kijana alilamuka ku kitanda yake. Walimusaidia na watu wengine. Alitoka inje ya nyumba ya padri. Wakati alifika pa hile fasi walikuwa waaminifu wote, mu hoteli ya Monasteri, walimukaribia watu wingi na walimuuliza:

-Padri Serafim, alikusema nini, alikufanyisia nini?

Watu wote walisikitika kwa sababu hawakupate hata jibu moja. Mu muji Petrupolis alifika na afya muzuri! Kisha, waakti alisikia ya kama padri Serafim alikufa, alisema hii muujiza yake.

# Wokovu ya Monasteri Chernika ya Rumania

Taifa ya inchi wa Rumania walifanya nvita kupigana ya Turkie mu mwaka 1821, kwani waliteswa kwa ajili yao. Wakaa wingi ya muji kubwa Vukuresti walikmilia mu monasteri ya kiziwa Chernika, ni mbali karibu 12 kilometre ya Bukuresti. Hile wakati padri mkubwa Kalinikos (1787-1868) aliwakaribisha wote mu Kisanga ya Mt. Nikolaos, ndani ya ma chumba ya watawa, lakini watawa wote aliwapelekea mu kisanga ya Mt. Georgios.

Hii ma siku magumu wakaa ya muji walipata utulivu na saidio mingi ku padri mkubwa Kalinikos. Aliwafundisha, aliwashauria na aliwapatia chakula ya monasteri bila malipo.

Hii mwaka, wakati askari wa Turkie walitangazwa ya kama ndani ya ma kisanga walifuchama watu wingi, waliweka ma bunduki makubwa pempeni ya monasteri juu ya kuibomoa. wa askari wengine walienda ma kisanga ingine juu ya kuuwa waaminifu na visu vyao. Hile saa mt. Kalinikos alisanyika taifa muzima na watawa ndani ya Kanisa, aliwashauria kusimama nguvu na walifanya sala ya usiku (agripnia). Siku wa mbili alituma mutawa moja kwa mkubwa ya wa Turki na alimwaambia ma taabu na masikitiko yao kwa ajili yao. Hivi katika maombi ya padri mkubwa Kalinikos, machozi ya watu na saidio ya mt. Nikolaos watu wote waliokolewa ku lufu.

Wakati iliisha ma chakuka yote ya monasteri, watawa na waaminifu waliteswa juu ya njaa. Hile saa alipika magoti yake mt. Kalinikos mbele ya Picha ya Mzazi-Mungu na mt. Nikolaos na aliwaomba saidio. Mara moja maombi yake ilisikiwa ya watakatifu! Wakati alisimama kisha sala yake, mt. Kalinikos, alifika inje ya mulango ya monasteri yake watu tano wenye walikokota motogari moja ya kujaza mukate. Hii mukate alituma mkubwa ya wamuslimane jemadari toka kundi yao ya ngambo ingine.

Tena mu mwaka umoja 1821, mkubwa jemadari mwingine aliyekuwa kundi ya askari yake mu mukini Penteleimon, alikamata mutawa mwanamuke moja ya monasteri pasarea sawa mutumwa. Lakini mt. Kalinikos hasikupende kuwa mutawa moja mwanamuke pa mikono ya mkubwa moja muslimani. Alituma barua kwa mkubwa mwingine ya waturki juu ya kumuacha mutawa muhuru. Hule mkubwa aliyemubamba mutawa mwanamuke, alisirika na usiku pamoja na ma bunduki makubwa yake alikamata mpango kupigana monasteri ya mt. Kalinikos, kwa kuiba vitu vyote vyake na kukuua padri Kalinikos. Padri, kwa kusikia mawazo na matendo yao, alifanya sala usiku pamoja na watawa wake wote. Na mara ingine aliokolewa na namna wa ajabu toka hii hatari. Kwa sababu hile usiku mkubwa jemadari alikuwa tayari kubomoa na kuharabisha monasteri, mutumihsi yake moja, alipima kumuua na bunduki yake. Lakini mashasi ilipita inje ya mwili ya mwili yake na hivi jemadari muslimani aliokoa uzima yake. kwa ajili ya hii muujiza aliogopa na alituma hii mavazi yake sawa ukumbusho ya hii mambo mu monasteri ya Chernika. Na amri ya padri mkubwa Kalinikow, aliinunua na hii makuta walichibula kisima moja inje ya monasteri. Hii kisima inaitwa mpaka sasa: «Kisima ya wa turkie».

# Wokovu ya watumishi ya chombo

Pepo ilipepula nguvu kati ya usiku moja wa baridi mu bahari Egeon, karibu ya inchi Grekia na chombo moja ilikuwa hatari kupasuka na kupotea! Chombo sawa bego ya tunda ilipanda na ilianguka na iliingia ndani ya maji ya bahari.

Mu monasteri ya mt. Markos watawa walifanya sala ya usiku (agripnia). Watumishi ya chombo walipata hatari mnene na walikuwa na warafiki ya wale watawa waliishi mu monasteri ya mt. mutawa Parthenios ya Kisanga Khios (1815-1883).

Mkubwa wa chombo jina lake Zanaras ya mukini Brondado, aliyemufamia mutawa Parthenios, alisema na huzuni ya roho:

-Ee Mungu wangu, utuokoe katika sala ya mutawa Parthenios na vile vitu ni ndani ya chombo tutaipeleka mu monasteri yake!

Mutawa parthenios hile saa alisoma sala yake. Mara moja alimbakia bila kutengwa! Alinyanyua ma macho yake pa Picha ya Kristu, alinyanyua mikono yake juu ya kuanza sala. Watawa walimuona, bila wamuulize ao kusuburia naye. Paka waliandika hile siku na saa ya sala yake. Hile saa mkubwa Zanaras alisema sala yake kwa Mungu, kwa rafla mutawa moja alikuja na alikamata volan ya chombo. Aliwaangalia na mucheko wa kitumaini

-Watumihsi wote walisema na sauti yao nguvu: Parthenios, Parthenios. Ni Padri mkubwa ya Monasteri ya mt. Marko!

Hatari ya chombo ilishuka sana. Pepo ilisimama kupepula. Ilikuja utulivu mu bahari. Kisha mt. mutawa Parthenios alikimbia. Asikuonekane!

Kisha ma siku madogo chombo ilitembea pamoja na watumihshi yake yote mu monasteri ya mt. markos. Sawa vile waliisha kumupatia malako walifika karibu. Walitosha vitu vya vyote ya chombo na walipeleka mu monasteri. Ya kwanza walimushukuru Mungu na mutumishi wake padri Parthenios na kisha walirudia ma nyumba yao.

wale waliokolewa walielejea hii muujiza kwa watawa wote na woga na shukrani kwa Mungu. Watawa waliangalia hile siku padri ya roho yao alisimama somo ya sala yake na alinyanyua mikono na alifanya sala na walisikia ya kama hile saa huyu alifanya sala juu ya wokovu ya chombo yao!

## <u>Ndugu wa wili</u>

Mu muji Argostolio ya Kisanga Kefalinia aliishi jamaa moja na walikuwa na watoto wanawume wa wili. Hile wakati aliishi kule na mutawa na padri Maisios Mbashas (1801-1888).

Hawa watu walikuwa waaminifu, kupita mama ya watoto, mnwenye alisaidia watu na maskini na vitu vyake.

Nyakati moja alikufa bwana yake! Mama balaka pamoja na watoto wake wa wili aliendelea uzima yao na aliendelea kusaidia na maskini. Alitembelea wagonjwa na wenye kifungo na aliwaongoza mu imani ya Kristu.

Usiku moja, mtoto wa kwanza, na kipimo yake miaka 21, hile saa aliika karibu ya meza ya nyumba yao, alifanya kivukutu na alianguka pa kitanda! Mama yake aliita munganga. Huyu aliangalia mtoto na alisema ya kama mambo ya mtoto ni ya hatari na alisema kwa mama yake ya kama mtoto atakufa. Hile saa mama yake alienda mbele ya ma Picha ya Watakatifu nyumbani yake na aliwaomba hile usiku muzima, kabisa Mzazi-Mungu, kwa kusaidia mtoto yake.

Lakini, bahati mubaya, mtoto yake, asubui alifariki! Mama yake alilia, alisikitika, lakini saidio kwa watu wagonjwa na maskini aliendelea kufanya, sawa na zamani.

Mbele ya kupitisha mwaka moja, aligonjwa na mtoto mwingine. Munganga alihamakia mtoto na alisema ya kama, hakuna namna kuishi. Ugonjwa yake ni nguvu. Mama yake alikimbilia mara ingine kwa Watakatifu na aliwaomba na machozi na mbele ya Mzazi-Mungu Maria na kwa Mt. Gerasimos juu ya kumusaidia.

-Munisaidie kwa ajili ya hii buruma na saidio ninafanya. Muokoe mtoto wangu wa pekee.

Siku ingine asubui na huyu mtoto alikufa. Hile saa mama yake aligeuza mfano yake na alikuwa sawa nyama mukali ya pori! Alianza kuchabula Mungu na Watakatifu wote.. . Nyumbani yake hasikupokelee hata mtu moja. Alipatia ma picha ya watoto wake wa wili kwa mtu moja mwenye kufatula juu yeye kufanya ma picha makubwa. Mama yao alibeba ma picha ya watoto wake na aliweka pa kibabashi ndani ya nyumba yake. Picha moja pa kibabashi moja na picha ingine mu ngambo ingine pa kibabashi. Aliweka pa picha yake nguo moja teketeke, aliweka chini yao mushumaa moja-moja ya kuwaakisha. Kila siku aliwaakisha ma mushumaa, aliangalia watoto wake na alisuburia na wao.

Siku moja mt. Mutawa Paisios Mbashas aliingia ndani ya chombo moja na kutoka ya muji Liksuri alikuja mu muji Argostolio. Aliondoka na bakora yake aende nyumbani ya hule mama balaka. Wakati alikokola mlango, hule mama alikuja inje ya dirisha. Wakati alimuona huyu padri, kwani hasikumufamie, alisirika na alianza kumuchekelea na alisema matusi na ma neno mabaya! Hule padri alimuwaambia mara wa mbili na wa tatu amufungule mulango ya nyumba yake, kwa sababu alikuwa na sauti moja amuwaambie. Lakini huyu mama alimuchabula mubaya.

-Ao utanifungulia mulango yako ao nitaingia mimi mwenyewe ndani, alimuwaambia padri. Hile saa alisukuma na bakora yake mulango na mara moja aliingia ndani.

Mama alishituka! Mtakatifu Paisios alipanda mugazi ndani ya nyumba na alienda mu chumba munene. Alimufwata na huyu mama. Wakati walisimama pa hile chumba ilikuwa ma picha ya watoto wake alimuwaambia padri:

-Ikaa mu fasi moja ya kona na utaangalia jambo moja na utashangaa!

Padri alifanya sala kidogo. Ma nguo iliyekuwa mbele ya ma uso yao, ilianguka chini na watoto wa wili walionekana katikati ya hii chumba! Hile saa walitosha bunduki yake kila mtoto walipika mashashi na walikufa yote wa wili. Kisha hii jambo wa ajabu walirudia watoto mara ingine ndani ya ma picha yao.

Mama yao aliangalia hii jambo wa ajabu na woga na ushituko mingi. Padri alimuelejea:

-Mama wangu, Mungu anakupenda! Alibeba, basi, watoto wako na namna muzuri, kwa sababu, kama waliishi, ilikuwa namna kuona hii jambo uliona hapa sasa. Watoto wako wa wili walipenda paka mwanamuke mumoja na walikuwa na tamaa nani atabeba huhu mwanamuke ya bibi yake. pa hile fasi alibeba watoto yako, kwa sababu ilikuwa namna wakufe wa wili. Basi, tubu mbele ya Mungu. Omba hurumia. Umushukuru Mungu na endelea kazi yako juu ya kusaidia wa maskini, sawa ulifanya na zamani.

Kweli, huyu mama mkubwa ya muji Argostolion alitubu na aliendelesha kazi wa buruma yake, mpaka mwisho ya uzima yake.

## <u>Nvula isiyosimamishwa</u>

Mtakatifu Nektarios, askofu wa Pentapolis ya Misri (1846-192) alitembelea mara ya kwanza Kisanga Egina ya Grekia ku mwaka 1904. waakti alienda mu hii Kisanga aliponyesha mtu moja waliyekuwa ndani yake pepo buchafu na mwanamuke moja aliyetosha damu yake.

Ya kwanza mu Kisanga alitafuta hile fasi alipenda kujenga Monasteri yake. Kisha alirudia pa kikavu na aliongojea chombo juu ya kurudia mu Athina, muji kubwa ya Grekia. Mbele yake ilikuja kundi moja ya watu wa hii Kisanga na katikati yao alikuwa na mkubwa ya muji.

-Mweshimiwa.. . .

-Ndivyo. Ninamisikia.. .

-Mutuhurumie, kwa sababu tunataka tumiuzi kidogo. hapa ni na wa ndugu ya Kisanga yetu, wenye wanataka kusema sauti moja.

Askofu aliangalia moja moja uso yao na namna wa upadri. Wale watu walivaa manguo mabaya.

-Sisi hapa, Mweshimiwa tukona mu Kisanga yetu mulinzi, mt. Dionisios. Neema yake kwa sisi nu kubwa. Lakini, kwa ajili ya zambi zetu, huyu Mulinzi yetu anakataa kutusaidia. Hapa ya wakati miaka tatu na kipanda hakuna nvula. Kisanga yetu itakauka.. . Tunamiomba, ee Mweshimiwa, kwa kutusaidia.

Askofu alicheka na huruma.

-Watakatifu wetu, ndugu wangu, aliwajibu, ni yulu mu Kanisa wa mbinguni na wanaomba mbele ya Kiti ya Yesu Kristu. Wanaomba kwa sisi. Na hawatutume mafigo.

-Lakini mumuombe na mweye. Mumuombe na Mungu atatusaidia. Jana tulipata tangazo ya kama muliponyesha watu wa wili.. .

-Mimi nilifanya miuujiza? Hapana. Munafanya kosa. Misikufanye mimi tendo moja wa ajabu. Kama munaweza juu ya hule kijana aliyekuwa pepo buchafu, mutasoma Madiko Takatifu na mutapata fundisho nzuri. Kila padri, wa ndugu wapenzi wangu, ni mutumishi ya Mungu kila siku.. . Huyu inapashwa kumaliza mapenzi Yake. Lakini, mu Juma ingine nitakuja huku mu kanisa yenu kubwa na pamoja tutafanya sala juu ya mambo yenu. Nitatumainia ya kama Mungu mwenye ni Mwema atatuma nvula pa Kisanga yenu.

-Aksanti, Aksanti, Mweshimiwa. Miaka yenu iwe wingi. Hii saa iwe ubarikiwa. Safari yenu iwe muzuri.

Mt. askofu Nektarios alichunga malako yake. Mungu alimubariki na alirudia kisha juma moja mu Kisanga Egina. Alifanya Liturgia mu Kanisa yao kubwa kwa jina ya Kulala Mzazi-Mungu. Askofu, ku mwisho ya Liturgia, aliwaambia waaminifu wote wapike magoti yao chini na yeye alisoma ma sala juu ya kunesha Mungu nvula. Waaminifu wote walijibu: «Bwana hurumia».

Kisha Liturgia aliendа pa hile fasi aliisha kuchakula juu ya kujenga Monasteri yake. Bahati kizuri, kwa sababu alirudia na chombo mu muji Athina na haraka. Mbingu ilijaza na mawingu. Kisha saa kidogo ilianza kunesha nvula. Ilinesha nvula bila usimamisho!

Watu wote walisema: Utukufu kwako, ee Mungu, utukufu kwako!

Kisha ma siku filani, mu tarehe 19 Mwezi ya Kumi 1904, mwenye kufungula masomo ya wapadri, pahali alikuwa mkubwa askofu Nektarios, alikuja kwake na alimwaambia ya kama walikuja amutembele kundi moja ya waamnifu wa Kisanga Egina. Alisema: Uwaambie aingie ndani.

-Waliingia mu fasi ya kazi yake watu tano-sita. walimufamia tangu zamani, wakati askofu alikuja mu Kisanga yao mara ya kwanza.

-Mweshimiwa, walimusema, tulikuja tuseme kwenu ya kama sasa tukona mambo ingine munene! .. .

-Nikusema?

-Inanesha nvula, bila usimamisho! Inasimama mbingi ma saa wa wili na inaanza mara ingine. Mitoni yote ilijaza, bahari iliharabika ragi yake na ma nyumba madogo ya watu walianza kujaza na maji. Tunaogopa ya kama tutakufa juu ya maji mingi.. .

-Hakuna namna, aliwaambia.

Alicheka na aliwaambia hapana kusikitika.

-Musiogope! Itasimama.

-Mufanye, Mweshimiwa maombi yenu. Tunaomba nvula, lakini hapana hivi.. . Tutakufa.. .

Haina lazima nifanye mimi maombi. Mungu anajua anafanya nini. Muko na kipwa ya wakati miaka tatu na kipande, namna gani munataka kujaza na ma kisima na ma chemchem yenu na kumwangisha na ma shamba yenu? Basi, musiogope. Mungu anajua anafanya nini.

Aliwaambia waikaa chini. Aliwapatia kafe na kintu ya utamu na aliwaacha waende na utulivu.

## Makila

Hile wakati mt. askofu Nektarios alijenga monasteri yake mu Kisanga Egina, kila wakati, alikujaka muvuvi moja kutoka kisanga Poros. Aliitwa bwana Theodoros na alimufamia mt. askofu Nektarios.

Wakati aliweka makila yake karibu ya Egine huyu Theodoros, kisha alipanda mu monasteri na alimupatia kwa askofu samaki ya kula. Hivi na askofu aliomba kwa Mungu juu ya huyu Theodoros na bibi na watoto wake.

Siku moja, mu tarehe ku mwanzo ya 1914, alikuja mu monasteri Theodoros na machozi na manguo mabaya na bila samaki.. .

-Juu ya nini unalia, baba-Theodore? Alikufa mtu moja katikati ya jamaa yako?

-hapana, Mweshimiwa, lakini nilipata ingine kintu kibaya kupita. Walikuja masamaki makubwa kati ya makila yetu na wanaiharabisha. Ninatumika, kila siku na muchoko mingi na misiweze kutosha hata samaki moja. Jamaa yangu atakufa. Watoto wangu sasa ya ma siku wa ine wanalala bila chakula! Ninasikia haya kutoka inje ya soko na nitaomba huruma.

Alianza mara ingine kulia.

-Usilie. Ikaa kukula kidogo chakula na sisi tutakusaidia na kila namna, kama tunaweza.

-Iko wapi mutrubwi na vitu vya kazi vyako?

-Ni chini mu kikavu.

-Utaweza kunilete makila huku kwangu?

-Ndivyo, baba wangu. Mungu anakusaidia weye.

-Weye anakusaidia kupita, alimujibu Mt. Nektarios.

Baba Theodoros aliende na alimuletea makila mara moja.

Askofu al;iichukua na aliipeleka ndani ya Kanisa. Alifanya sala, aliibariki, Na sisha alimurudiswa mukusema:

-Kamata, baba Theodore makila yako, Nitamumainia ya kama ma samaki makubwa watakimbia.

Kisha ma juma wa wili alirudia baba Theodoros na furaha mingi mu monasteri. Alimupatias kwa Mtakatifu na ma samaki wa wili makubwa.

-Padri wangu, padri wangu, nilitupa makila ndani ya bahari na sasa misi na na wakati ya kutosha ma samaki mengi. Mikono yao iwe mabarikiwa.

-Mungu, mupendwa wangu Theodore, ni Mwema kupita ya sisi.. . Ninakushukuru juu ya hii samaki ulinileteа. Kuja tuingie mu Misa wa wili kwa kumushukuru Mungu.. .

## Wakubwa wa wili ya Musulmani

Wakati moja wakubwa wa wili ya Misulmani, waliyekuwa na wafumu, walienda kwa mt. Arsenio wa Kapadokis (184)-1924).

Mtakaitfu aliwapokelea na mapendo na aliwapatia kafe. Wakubwa walianza zungumuzo moja kwa bure na akili ya mt. Arsenios iliuma. Aliwaambia:

-Misiweze kumisikia, kwani inauma akili yangu.

Wale hawakusikie na walimusema:

-Ee padri, sisi tunaweza tukufanye kintu kimoja kizuri (lawa ya shetani) na akili yako itasimama!

Mt. Arsenios aliwajibu na namna ukali:

-Mimi niko na nguvu kupita kubwa ya nguvu yenu na ninaweza na uwezo ya Mungu kumisimamisha hapa ndani na hamutaweze kutengwa.

Aliwaacha na alienda mu chumba yake ingine. Wakati waliisha kunywa kafe yao wakubwa wafumu walitaka kuondoka, lakini hakuna namna kusimama na kutembea. Waliisha kufungwa na minyororo isiyoonekana! Basi, walimuita padri Arsenios juu ya kuwafungula. Hule alienda kwao, lakini hasikuwaambie kintu. Paka na alama ya ma macho yake aliwaambie watoke na vile waliondoka.

Wakubwa wamuslimani walisikia kosa yao na waliomba hurumia:

-Ee Padri mkubwa, utuhurumie. Uwezo yako ni kubwa, kwa sababu ilitoka ya imani nguvu yako! Sisi tunatumika pamoja na shetani.

## Wamisulmani wa ine

Wanaume wamisulmani wa inne walienda siku moja kuiba mt. Padri Arsenios wa Kapadokis. Mtakatifu hile saa alisoma kitabu moja. Aliona wivi wenye walifungula mlango yake

na walianza kutafuta ma fasi yote ya kuume na kushoto vitu filani. Mt. Arsenios aliwaangalia, lakini hasikuwaambie hata sauti moja.

Kwani hawakupate makuta na vitu vingine wivi walikuwa tayari ya kuondoka. Paka walipata manguo ya kitanda mbili na mwivi moja aliikamata. Hii ilikuwa mali yote ya mt. Arsenios. Lakini walipata mambo gani? Hile wakati walitaka kuondoka, hawakuweze kutafuta mulango, sawa waliisha kuwa vipofu! Walitembea pempeni ndani ya nyumba ya padri na hawakuona mulango ilikuwa wapi! Hile saa padri alibamba musulmano moja na alimusema:

-Tazama mulango, pahali wanapita wivi na wanaenda mu gehena!

Paka hivi waliweza kutoka inje! Halafu, walitubu na waliomba hurumia. Mt. Arsenios aliwasamehe na wale walikimbia. Kisha walielejea mambo yao kwa wandugu wao wengine.

-Ole, ole wetu! Musiende kuiba huyu padri Arsenios, kwa sababu, kama mutaingia ndani ya nyumba yake, hamutaweze kutoka inje.

## Malipo ya wenye kufungwa

Wanyanganyi wingi waliyekuwa Misulmani toka Kapadokia ya inchi Azia Kidogo, waliingia kunyanganya ndani ya mukini Farasa watajiri kumi na mbili. Waliwatangaza ma jamaa yao, ao watawapatia 500 lire wa zahabu ao watawauwa. Tena waliwaambia ya kama haipashwe kufanya bukomvi kupigana yao, kwa sababu, wale watumwa wandugu wao, wekona ndani ya buloko, watawauua yote.

Wakaa ndani ya mukini Farasa walisikitika sana; watu wengine walienda kusimamisha vijana yao, wenye walitaka kuwapika wamisulmani, na watu wengine walienda mbio kwa padri Arsenios, aliyekuwa kitumaini yao umoja sana. Tena mambo ilikuwa munene, kwani na kundi ya misuylmani waliisha kutayarisha vity vya ya kufanya nvita.

Mtakatifu Arsenios, wakati alisikia hii mambo, alienda mu Kanisa na alisema kwa watumihsi ya kanisa kwa wamupatie makuta hile ilikuwa ndani. Hii makuta ilikuwa karibu 50 lire wa zahabu.

Basi alibeba hii makuta na pamoja na watu wazee wa wili alipanda pa hile fasi ilikuwa kundi ya askari yao na mkubwa yao. Mkubwa alikuja na furaha, kwa sababu alizania ya kama huyu padri atamuletea makuta. Wakati alimuona mkubwa padri Arsenios alianza kumufokea hivi:

-Usiogope weye Mungu? Usisikie haya? Namna gani watapata hii makuta zahabu hawa watu wamaskini na munasema ya kama mutakata vichwa vyao, kama hawatamiletea hii makuta?

Kisha alichukua mufuko na hii makuta ya kanisa, aliitupa mbele ya miguu yao na aliwaambia:

-Mubebe hii makuta juu ya hii muchoko mulifanya na munileteа huku waaminifu wangu, wenye mukona waliwabamba na munakamta sawa watumwa pa mikono yenu. Kama munakataa, mimi nitamikata sawa ma njiwe hapa sasa.

Wakati alisema padri: «Mitamikata sawa ma njiwe» wa askari misulmani walisimama pa fasi yao bila kuwaza ya kutenga. Walisimama sawa ma sanamu! Kisha aliwaambia:

-Mbio, munileteе huku watu wangu na mutokeni mbio. Paka hile saa waliweza kutengwa na walikimbia. walifungula watumwa wa kumi na mbili waliyekuwa toka mukini Farasa ya Kapadokia na walikimbia na woga mingi. Walikimbia bila kunamisha mikono yao juu ya kubeba hii makuta, iliyekuwa chini yao! Mt. Arsenios alisema kwa wenye kufungwa:

-Mulokote hii makuta ya kanisa na tuende.

Kisha saa kidogo walirudia wote wa furaha mu mukini yao.

## Safari kwa pepo

Mutawa Isaaka ya monasteri ya mt. Dionisios ya Kilima Takatifu (1850-1937) alikuwa kijana na alitumika  sawa musaidizi mu nyumba ya monasteri mu muji karies karibu ya mkubwa mutawa muzee Gelasios.

Siku moja wa baridi, ku mwezi Februarie (mwezi ya mbili) ilionekana mambo moja na ilikuwa lazima padri Gelasios kusuburia na wakubwa ya monasteri juu ya mambo moja. Hile wakati haikukuwe telefon. Ilipaswa mtu moja aende mu monasteri na miguu yake, hata kama muda ilikuwa mubaya. Basi, aliita musaidizi yake mutawa Isaaka na alimutuma na barua moja aipatie kwa padri mkubwa ya monasteri yao. HUle aliomba baraka yake, alibeba bakora na barua na alianza kutembea katikati ya milima na miguu ku monasteri.

Hii njia kutoka Karies mpaka monasteri ya Mt. Dionisos kati ya Milima ni ma saa wa tano.

Padri Isaaka aliondoka toka Karies na utii, lakini mbingu ilianza kujaza na mawingu na ilionekana ya kama itaanza kunesha teluji. Alitembea karibu saa moja, aliingia ndani ya pori, pahali ni miti marefu na mara moija alipata mambo munene. Ilianza kunesha teluji!  Ma fasi yoite ilijaza na teluji. Alikombana kutembea lakini hakuna namna. Kipimo ya teluji ilifika karibu metre moja. Alisimama katikati ya pori. Ma fasi yote ya kufunika na teluji. Pepo ilikuwa nguvu. Alipotesha njia, baridi ilikuwa nguvu kabisa. saidio ya mtu fulani, hakuna namna. Hata nyumba moja haikukuwe kuingia ndani. Ilifika magaribi. Hakuna wokovu ya padri Isaaka. Hile usiku ilikuwa wa mwisho kwake.

Wakati, basi, alipotesha kila kitumaini, alinyanyua mikono yake juu pia mbinguni na imani nguvu alimuita Mungu:

-Ee Bwana yesu Kristu, Mungu wangu katika sala ya padri mkubwa wangu uniokoe. Ww Mt. Yoano Mutangulizi, unistahili nifike mu Monasteri yetu.

Na tazama!  Hile saa nguvu moja isiyoonekane alimukamata na alimupeleka inje ya monasteri yake. Saa ilikuwa 4, 30 magaribi. Watawa ya monasteri hile saa waliisha kumaliza meza ya chakula. Mujukumu ya Mulango ya monasteri, wakati alimuona padri Isaaka, inje alishituka na alimuuliza:

-Unakuja ya wapi, padri?  Namna gani ulikuja ndani ya hii hali ya muda?

Tena alishangaa, kwa sababu mukongo  yake hasikuone mwendo na alama ya bilato yake! Hii musagao yake mkubwa ya mulango alisema na kwa watu wengine. Padri Isaaka, hasikupende kuwaambia namna gani alifika. Alitaka kufuchika muujiza. Lakini aliwaambia hivi na ma sauti madogo:

-Na saidio ya mt. Yoano Mutangulizi na Mulinzi yetu, nilifika huku bila hatari na aliwaonyesha Picha yake.

## Saidio ya Malaika Mkubwa

Mu juma asubui ya tarehe, 20 Oktovrie (Mwezi ya kumi) 1945 kundi moja ya askari walikombana kumubamba padri Dimitrios Gagastathis, aliyekuwa padri mu parokie ya mukini moja kati ya Grekia. Na hile siku alitembea mu mukini Vasiliki ya njimbo Trikala ya Grekia.

Alituwaambia huyu padri:  «Walinitafuta, walinichabula na walinipika na mashasi, Lakini hawakuweze kuniua!  Mashashi walinipika, lakini walipita paka na ma raso (manguo meushi) yangu, na hata moja rishashi haikunipike!

Walinikaribia na walikuja pempeni yangu karibu metre makumi tano. Mimi, hile saa nilikuwa mu hatari, nilinyanyua mikono yangu yulu mbinguni na nilimuita na yote nafsi yangu:

-Ee Malaika Mikaeli mkubwa, uniokoe, niko ndani ya hatari munene!

Na, o muujiza wa ajabu!  Sawa umeme alionekana Malaika Mikaeli kwa mkubwa ya wa askari adui yangu. Malaika alikata musipi  hile ilichunga hile kintu ilikuwa pa punda na mkubwa aliikaa juu yake. Mara moja hule mkubwa wa askari alianguka chini na alipasuka kifuno yake. Wa askari wengie wa kumi walisimama bila kutengwa. Waaminifu ya parokie ya mukini

Vasiliki, walisikia mashashi na walikimbia pa milima na waliangalia mambo yangu itakuwa namna gani.

Hile saa mimi nilisikia sauti moja. Ilikuwa sauti ya mkubwa ya wa askari:

-Padri wangu, utuhurumie na wende muzuri. Ukona milinzi wakubwa. Inapaswa kuishi tena. Vile ni mapenzi ya Mungu!

-Aksanti, nilimujibu.

Niliwasamehe na niliendelesha safari yangu. Niliwatakia Mungu awangaze kwa kutubu na kufanyika watu wazuri.

## Epuko ya uharibifu

Kati ya muchana ya mu kazi inee mu tarehe 7 ya Yuni (mwezi ya sita) 1956 ilianza kuonekana mawingu mu mukini Platanos ya Trikala ya Grekia. Pale padri ya parokie alikuwa padri Dimitrios Gagastathis.

Ilionekana kintu kibaya kinene, kama hii mawingu ilikuja kwetu, mu mukini yetu. Wakati mawingu ilikuja karibu ya njimbo yetu, nilienda mu kanisa ya malaika wakubwa, nilipika magoti na niliwaomba kuchofesha mawingu mbali kwa sababu itaharabisha ma shamba yetu yote. Na, o muujiza wa ajabu na wa haraka! Malaika walisikia maombi yangu na mara moja mawingu walikimbia mbali.

Mawingu moja ilienda ma mukini iongine pahali hile fasi ilijaza na maimbwe meupe munene na mawingu ingine ilienda ma mikini ingine na ya ma siku wa wili iliharabisa ma shamba yao yote!

Mukini yetu iliokolewa kwa ajili ya ulinzi ya malaika wakubwa milinzi wetu.

## Mahalaki yenye kufigwa

Mutawa wa monasteri ya mt. Dionisios ya Mulima Takatifu padri Anthimos alielejea kwa ndugu ya roho wake, padri Lazaro muujiza moja. Ilikuwa hii ifwatayo:

Hile wakati nilikuwa mupisi mu monasteri yetu (1951-1952), ilikuwa mu Juma na tulikuwa na sala ya usiku. Nilibeba mahalaki ya mutawa mujukumu juu yan kuipika na kukula watawa mu Juma, kisha Liturgie. Niliiweka pa chungu ma saa tatu, lakini hakuna namna kuipikwa. Saa ilipita. Sikitiko yangu ilikuwa mingi. Hakuna utulivcu kwangu. Kisha sla ya usiku, Wapadri watabakia na njaa?

Nilitaabu mingi. Nilishuka mu kanisa mudogo ya Malaika Watakatifu. Niliwaakisha ma kandili yao. Nilipika magoti mbele ya picha yao, nilibusu ma uso yao. Nilibeba komboskini na nilianza kufanya sala. Kisha sala, nilisikia sauti moja kutoka ya ndani yangu:

-Beba mafuta kidogo ya kandili na uitupe ndani ya mahalaki.

Nilifanya hivi na imani. Niliimba na wimbo ya malaika na kisha ma dakika kumi na tano (15), hile mahalaki ilikuwa ya kukauka na hakuna namna kuipikwa. walipikwa mara moja. Niliona hii muujiza na niliwashukuru wa malaika Wakubwa, wenye walinitosha ku hii taabu na sikitiko! Wakati walikula watawa, walifurahi na waliniambia:

-Ee padri Anthimos, Mungu akusamehe. Ulitufurahisha mingi. Hii chakula yako ilikuwa na utamu sana.

Lakini mimi nilishukura na nilitukuza Mungu na Wa malaika wakubwa na maombezi yao sisi tukona kitumaini kuokolewa. Amina.

## Ufazili kwa mufazili

Padri arkhim. Venediktos Petrakis alikufa mu tarehe 8 Septembrie (Mwezi ya Tisa) 1961 alitumika muzuri kabisa sawa muhubiri mu njimbo ya Etolokarnania ya Grekia na kabisa mu mji Agrinio. Watu wakubwa ya hii njimbo walikuwa watoto wa roho yake na walikuwa matunda ya kazi ya roho yake, kwa sababu alitumika nguvu juu ya kupenda Mungu na watu.

Wakati huyu muhubiri alikuwa kijana na alifunda mafundisho ya Theologia alim, usaidia mama moja, jina lake Melpomeni Bulbasaku toka muji Patra ya Grekia.

Wakati alikuwa arkhimandritis na alitumika mu njimbo yake, walimwaambia ya kama mufazili na musaidizi yake, huyu mama ni ku mwisho ya uzima yake na alimuita amupatia takatifu Komonyo. Mara moja padri Venediktos alibeba motogari moja na al;ienda mu mji patra, nyumbani yake. Kwa kufika kwake alikuta shemasi moja, aliyekuenda kwake amupatia Komonyo.

-Alimuuliza; Ulimukomunika?

-Misikupate wakati, pater. Alifariki! .. .

Waliingia pamoja nyumbani ya huyu mufu. Ilikuwa ya kujaza na waaminifu. Alisema padri Venediktos:

-Mupika magoti mweye yote na mumuombe kwa Mungu!

Alipika magoti na huyu.. . Kisha na mukono yake wa kuume alikamata mukono ya mufu na mukono yake wa kushoto aligusu uso yake na alimuita:

-Ee melpomeni.. . . Melpomeni.. . Mimi ni Benediktos. Nilikuja kukupatia Komonyo Takatifu.

Na o Muujiza wa ajabu! .. . Alifufuka Melpomeni. Alirudia mu hii uzima! Alifungula kidogo kinywa yake, alikamata Mwili na Damu ya Kristu. Kisha padri alimupatia vinyo akunywe na alimwaambia:

-Kunywa hii.

Aliikunywa.. . Kisha alikunywa na maji kidogo. Kisha alimwaambia:

-Sasa lala na mapatano muzuri mu ufalme ya mbingu.

Kisha alisema kwa shemasi:

-Ee ndugu, mimi misikukuseme ya kama bado kufa huyu mama?

Kisha alisema mbele ya watu waliyekuwa pale:

-Musiseme hata sauti moja ya hii matendo wa ajabu muliona leo, mpaka mwisho ya uzima yangu.

# ZAWADI YA MWISHO WA HERI

Ni tendo wa ajabu na wa furaha, hile wakati ya mwisho ya wale waaminifu, hapana paka Watakatifu, lakini na waaminifu wa upole, wenye walikuwa na mwisho moja kabaila wa ajabu.

Hii fasi ya mwisho ya watu ni onyesho moja namna gani aliishi huyu mtu mu uzima yake na alimufurahi Mungu na tena mwisho yake ni onyesho moja ya kama ataingia mu Ufalme mbinguni.

Mwsiho wa amani na baraka ya Mungu inajiungana na zawadi na maono mazuri. Tunafamia waaminifu, wenye walisema saa ya lufu yao, mbele ya kuifika ao walipokelea matulivu matakatifu ya malaika, Watakatifu filani na maono ya Paradizo.

Onyesho ya lufu wa heri ni onyesha ya kama Mungu alifurahi juu ya mwaaminifu moja. Lakini na waaminifu wengine walikufa bila kuona ao kupokelea maono ya paradizo ao matembeleo ya malaika ao Watakatifu. Hii haina onyesho ya kama hawa waaminifu hawakuokolewa. Hii maono na matendo wa ajabu ni kwa mapenzi ya Mungu.

## Mtakatifu Mutawa Sisois

Wakati walisikia watawa wa jangwa ya Mulima ya Mt. Antonio ya kama Mutawa mkubwa Sisois ni ku mwisho ya uzima yake, alisanyika nyumbani yake juu ya kuomba baraka yake. Walimusifu sana. Walimuita «Alimasi ya jangwa» na kwa haki. Uzima yake yote ilikuwa ushindani moja juu ya utakaso na sasa mbele ya lufu yake utakaso iliangaziwa zaidi.

Pa uso yake uheshimiwa iliisha kuonekana furaha wa heri.

Watawa, watoto wa roho yake, wlaikuwa pempeni yake na walipenda kusikia sauti yake wa mwisho. Lakini padri Sisois aliisha kupanda na akili yake mbinguni.

-Anakuja padri mkubwa wangu, walimusika kusema na sauti wa chini. Watawa wenye walikuwa karibu yake na ma macho ya akili yao, waliona akuje kwake padri mt. Antonio juu ya kuchukua nafsi ya mtoto ya roho yake, padri Sisois.

-Tazama, kundi ya Mitume na ma Nabii anakuja!

Uso ya mutawa Sisois ilijaza na nuru wa mbingu. Midomo yake walisuburia chini, bila kusikia wale walikuwa pempeni yake.

-Unasuburia na mtu gani, ee padri? Walimuuliza wazee ndugu wake.

Malaika watakatifu wanataka wanibebe na mimi ninawaambia waniache tena juu ya kutubu, alisema na muchoko na machozi wa weili walianguka chini.. .

-Usina na weye tena lazima ya kitubio, mwenye heri Sisois! Weye ulitubu mu uzima yako yote, walimujibu watawa wengine na walishangaa juu ya unyenyekevu wake.

-Misijue, wa ndugu wangu, kama niliweka tena mwanzo ya kutubu.

Hile saa lisema hii ma sauti kwa rafla uso yake ilijaza na mwangaza. Wenye karibu walishangaa na musagao munene pamoja na woga.

-Bwana wangu na Mungu wangu, utukufu kwako!

Hii ilikuwa ma sauti yake wa mwisho. Hivi nafsi yake ililuka mbinguni. Aliisha kuona Yesu Kristu? hatujue. Lakini hii nuru kimungu ilijaza uso yake, harufu hiule ilijaza nyumba yake wanatwaambia ya kama Mufalme wa mbingu alimutembelea.

## Mtakatifu mutawa Ilarioni

Mt. Mutawa Ilarioni miaka tano wa mwisho yake alipitisha mu Kisanga Kipros.

Alifika mu kipimo miaka yake makumi mane (80) na alisikia na kama inakaribia saa ya ondoko yake mbinguni. Kwa sababu alilofa hii ma siku mutoto ya roho yake, mutawa mt. Isikhios, aliandika barua moja sawa agano. Alimwacha Evangelio moja, raso (nguo meushi) moja, mupila urefu moja na kukuli mojo (nguo ya kofya). Hii yote ilikuwa mali yake.

Kwa wale wa ndugu walikuja kwake amusalimia alisema:

-Ninajiuhuru ya monyororo ya mwili yangu na ninaenda karibu ya Mungu!

Kisha aliwashauria mambo ya maziko yake na aliongeza hii sauti:

-Mutanizika paka na hii manguo ninavaa sasa. Wala mutaongeza nguo moja, wala mutatosha hata moja!

Ma saa ya mwisho alisema kwa maungo yake:

-Nafsi yangu, juu ya nini unaogopa? Toka inje na tembea mbele. Uende kwa Bwana wako! Juu ya nini unaogopa? Toka ya mwili yako. Ulitumika kwa Bwana wako miaka makumi saba (70) na sasa unaogopa lufu? Kristu anakuita! Anakuita kuenda karibu Yake. Basi, kuja, na furaha karibu yake!

Hii ma sauti alisema mutawa Ilarioni, alifanya alama ya Msalaba, na aliishi uzima yake. Ndugu wake walimuzika pa hile fasi yeye aliisha kuitayarisha.

## Mtume mwanamuke Nina

Uhubiri ya mt. Nina mu muji Kakheti ya Georgia ao Iviria, chini ya Rusia, ilikuwa kazi yake wa mwisho. Nikusema mbele alifanya kila tendo ya mapendo ya watu na kisha aliwaahubiri

imani ya Kristu. Lakini sasa ilikuja mwisho yake. Mungu alimufunusha ukaribisho ya mwisho yake. Basi, mtume Nina aliandika barua moja kwa mfalme ya inchi Miryani:

-«Ninatakia ufalme wako kuwa na baraka daima ya Mungu na Mzazi-Mungu na ulinzi ya uwezo ya Msalaba Mweshimiwa! Mimi, sawa mugeni, ninaondoka ku hii dunia. Ninakuomba sana, unituma askofu Yoano juu ya kunitayarisha ya safari yangu wa mwisho, kwa sababu siku ya lufu yangu ni karibu»

Hii barua aliipatia kwa bibi ya mfalme, jina lake Sonje na hule aliipatia kwa bwana wake. Wakati aliisoma mfalme Miryani aliondoka na haraka na wakubwa wake na wapadri kwa kumukuta. Watu wingi waliisha kuwa pempeni ya kitanda yake na walitosha machozi juu ya mapendo yao. Wagonjwa wingi, wakati waligusu kitanda wake, walitunzwa!

Wanafunzi wanawake wake walimukaribia na walimuuliza awaaambia juu ya uzima wake ku mwanzo yake. Mama Salomi, mfalme yua Utzarmi aliandika ma sauti yake.

-Alisema kwao mwenye heri Nina: Iko nzuri kuandika uzima yangu uzaifu na umaskini, juu ya kuifamia na watoto wenu. Muandike uzima yangu juu ya kujua na wafwasi wenu na imani na mapendo ngapi mweye mulinipokelea, tena muandike na ma alama wa ajabu ya Mungu muliona mu uzima yangu.

Kisha aliwaambia juu ya uzima wa milele. Alikukomunika Mwili na Damu ya Kristu ku mikono ya askofu. Ku mwisho aliwaambia amuzike mu nyumba yake, pahali alikuwa hii saa. Vile, kisha miaka mengi ya utume wake mu Kanisa ya Kristu, alijitoa kwa mikono Yake.

Mufalme, askofu na taifa muzima waliomboleza juu ya lkufu yake, mkubwa mutume ya imani yao ya Kristu. Walipima kupeleka maiti yake mu Kanisa kubwa ya muji yao Mtisketa, lakini hakuna namna. hakuna namna kutengwa ya fasi yake! Basi, walimuzika pale ndani ya nyumba umaskini yake, mu mukini Bondbe.

Kisha wakati kidogo, ku mwaka 342, kisha uzalio ya Kristu, mufalme Miryani alijenga pa kaburi yake Kanisa moja kw ajina ya mt. Mushahidi mkubwa Georgios, aliyekuwa ndugu ya mtume Nina. Hii kanisa aliitimiza na aliisha yote mtoto yake jina lake Mbakari (342-364). Hii kanisa iko mpaka sasa! Waliitengeneza mara mengi, lakini hata mara moja haikubomowa. Wakati ingine pa hile fasi walijenga monasteri kwa jina ya Mtume Nina. Karibu ya kanisa ilijengwa Nyumba ya askofu (Mitropolis) ya mukini Bondbe.

Mungu Mwema alitukuza Mtakatifu Mtume Nina, kwa sababu mwili yake ilibakia muzima, bila uharibifu! Pa kaburi yake mpaka sasa inafanyika miujiza ya wagonjwa mengi! Kwa ajili ya hii miujiza, lakini kabisi juu ya uzima wa malaika wake na michoko ya utume yake, Kanisa alimufamia Mtume mkubwa ya inchi Georgia. Ukumbusho yake inashangiliwa mu tarehe 14 Yanuario (Mwezi ya kwanza), pahli hile siku alikufa katika Kristu.

## **Mtakatifu Markos mutawa wa jangwa**

Wakati moja aliondoka Mutawa Serapioni toka jangwa ya Misri juu ya kumukuta mutawa mt. Markos wa muji Athina, aliyeishi mu mulima Thraki ya inchi Abisinia ya Afrika.

Kisha michoko na ma hatari mengi alifika mu pango yake. Alimusika aseme ma Zaburi na kisha alisema kwa maungo yake:

-Ee Marko, mwili yako iwe wa heri, kwa sababu haikuanguke ma zambi ya usharati. Nafsi yako iwe wa heri, kwa sababu haikutalie matakio mabaya ya mwili na ma furaha mabaya. Tena ma macho yako iwe wa heri, kwani haikuone ma uso mabaya. Masikio yako iwe wa heri, kwa sababu haikusikie mawimbo ya zambi. Mikono yako iwe wa heri, kwa sababu hikufanye zambi. Miguu yako iwe wa heri, kwani haikutembee njia ya zambi.. . .

Kisha padri Markos alitoka inje na pasipo kumuona wakati ingine huyu padri Serapioni, alimuita na jina lake:

-Wafo wako, mtoto wangu Serapioni. Kuja karibu yangu.

Hile saa yeye alimukaribia, alimubatia na alimubusu mukusema kwake:

-Ninakutakia Bwana Yesu akupatie malipo yako, hile siku ya mwisho yako, kwa hii muchoko ulifanya kufika kwangu kuniona mimi, mtu moja mwenye zambi, sasa mu mwisho ya uzima yangu! Niko huku miaka makumi tisa na tano (95) na misikuone mtu mwingine. Ninakushukuru kwa sababu ulifanya hii muchoko.

Kisha walifanya pamoja sala. Walikula chakula na walim, ushukuru Mungu, kwani alibariki hii mapatano yao. Kisha alianza kusema juu ya uzima yake:

-Ya wakati miaka makumi tatu (30) nilikuwa huku na misikuweze kutafuta hata mayani moja ya kula, hata mizizi, hata kintu kimoja. Kwa ajili ya njaa, nilikula bulongo ya inchi na nilikunywa maji ya bahari! Manguo yangu iliharabika na niliishi mutupu na bila bilato. kwa ajili ya kivukutu mingi ao baridi mu nyakati yake, ilitoka ngozi ya mwili yangu. Nilianguka chini sawa mufu! Ma shetani usiku na muchana walinikombana na walinikokota inje na walikankamana kunifukuza ya huku. Pa hii fasi niliishi misikuone hata mtu, hata nyama mukali ya pori, hata nyma ingine. Mungu, vile ilionekana, ya kama aliisha kuniacha! .. . Lakini kama iliisha nyakati ya miaka makumi tatu, ilianza kuja matulivu matakatifu. Waliota, sawa vile na weye unaniona, pa mwili yangu manyonya na walinifunika! Tangu hile wakati mpaka leo, nikusema ya miaka makumi sita na tano (65) ma shetani hawakufike kunikaribia! Kila siku Mungu ananionyesha mapendo na saidio Yake. Hakuna hatari juu ya kivukutu ao baridi mu uzima yangu! .. . Lakini, na weye Bwana alikutuma leo huku juu ya kuzika mwili yangu unyenyekevu.. .

Wakati alisikia hii ma sauti yake padri Serapioni alianza kulia. Mt. Markos alimwaambia:

-Usilie, mtoto wangu, leo ni siku wa furaha juu yangu.. . Mungu, aliyekutuma huku, Huyu atakutulivu.. . . Leo ni siku wa furaha ya uzima yangu. Mwili yangu itapumzika ku michoko yake mingi na nafsi yangu itajaza na furaha wa uzima wa milele.

Mara moja pango yake ilijaza na nuru na pa hile fasi ilizambalishwa harufu. Mt. markos aliendelea kusema:

-Salamu, pango wangu ubarikiwa! Ndani yako nilifuraisha Hule aliyeniongoza mimi huku kuishi hii miaka mengi.. Pumuzika mwili yangu wa muchoko. Tangu leo anakuchukua Bwana wangu na atakupatia malipo yako. Kwa hii utupu ulipima miaka huku mengi na ulivulimia, sasa utavaa mavazi wa isiyoharabika hile siku ya Uhukumu! Ee ma macho yangu, tangu leo mutapumzika, kwa sababu mulichoka kila siku na usiku kwa kuangalia na kuongojea neema ya Mungu. Na mweye miguu yangu, mutapumzika, kwa sababu mulichoka kila usiku kufanya sala kwa kusimama.. .

Kisha hii ma sauti yake alimwaambia kwa padri Serapioni:

-Ee ndugu wangu Serapioni, zika mwili yangu unyenyekevu huku mu pango yangu na funga na maimbwe kinywa ya pango yangu na rudia mu Misri na amani. Usitake kuikaa huku.

Kisha hii ma sauti yake ilikuja sauti moja ku mbingu:

-Munileteе karibu yangu hii nafsi ufazili ya jangwa! Munileteе kwangu, huyu mutumihsi ya ma fazila na mutumishi wangu wa kweli. Kuja, ee Marko, kupumuzika mu inchi ya shangilia wa milele.

Mtakatifu mutawa Marko alipika magoti yake. Alipika magoti na mutawa Serapioni na aliendela kulia. Kisha saa kidogo alinyanyua ma macho yake yulu na aliona malaika wenye walikamata nafsi ya Marko na waliipeleka mbinguni. Mufuniko ya pango ilifunguliwa na walionekana ma kundi ya ma shetani. Walikuwa ma kundi ya Duani! Nafsi yake ilihamakiwa ya ma shetani karibu saa moja! Kisha iliendeleshwa maingio yake mbinguni, mu Kiti ya Bwana Yesu Kristu.

## <u>Mtakatifu Efremi wa inchi Siria</u>

Hile wakati mt. Mutawa Efremi wa inchi Siria aliacha hii dunia juu ya kupanda nafsi yake mu uzima wa milele, alitakaza wa ndugu wake amusifu na amutukuze mwili na maziko yake. Alikataza hata kumusoma sala ya Kiliyo ao kusoma mahubiri!

-Musiimbe wimbo juu ya mimi, mskini Efremi. Musiseme ma sauti ya utukufu, Musinizike na manguo mazuri. Musichibule kaburi juu ya mimi, kwa sababu niliisha kusema kwa Bwana Yesu ya kama ninataka kuniweka mu kaburi ya wageni. Kwani na mimi ni mugeni na ya kupitisha huku wakati kidogo.

Kama, alisema, mtu moja alitayarisha manguo mapya juu ya maziko yangu, misitake. Ninataka paka kukabula hii manguo ya watu wamaskini.

Mwaamnifu moja, aliyeisha kutayarisha nguo moja wa kabaila juu ya maziko yake, wakati alisikia hii sauti yake alisikitika na aliwaza hapana kuipatia hii nguo kwa watu maskini, lakini atawapatia makuta. Hii saa mara moja alipata ugonjwa na pepo buchafu! Alianza kufokea na kulia mbele ya kitanda ya Efremi na alitosha ma pofu ya kinywa zake. Mutawa Efremi mupendwa wa Mungu, alimuuliza:

-Uzulumu gani ulifanya na ilikufata hii mateso?

Kwa hii ulizo ya Mtakaitfu yuhu mtu aliyekuwa na shetani ndani yake, alisimama na alisema hii uwazo aliichunga kwa siri ndani ya akili yake, ya kama aliwaza kwa maskini wapatie makuta na hapana hii manguo alitayarisha ya maziko ya mt. Efremi. Kwani aliungama, mt. Efremi alumutunza mara moja!

Kisha hii muujiza alifanya na ma sauti ya shauria aliwapatia, alifika ku mwisho ya uzima yake na aliingia mu kikavu ya ufalme wa milele.

## Mt. mutawa mwanamuke Makrina

Mt. askofu Grigorios alitembelea mu monasteri ya mt. mutawa Makrina, aliyekuwa dada yake katika mwili. Huyu alikufa mu tarehe 379. Vile aliandika ndugu mkubwa yake juu ya lufu ya Makrina, dada yake:

«Makrina aliteswa na kivukutu. Alikuwa hapana pa kitanda, lakini pa mbau moja! Mbau ingine ilikuwa pempeni juu ya kuchunga kichwa yake.

Wakati aliniangalia na nilikaribia mlango, alisimama kidogo. Juu ya kuja karibu yangu hasikuweze, kwa sababu kivukutu yake iliisha kupita.

Huyu mutawa Makrina alinyanyua mikono yake kwa Mungu na alisema:

-Ee Mungu wangu, na hii matakio yangu uliitimiza, juu ya kuleta karibu yangu ndugu mkubwa yangu na mutumihsi wako!

Pamoja naye tulisuburia ma fumbu takatifu juu ya uzima ubinadamu na mapendo ya Mungu mu uzima yetu.

Kisha huyu alifanya hii sala kwa Mungu:

-Weye Bwana, ulitosha ya ndani yangu woga ya lufu. Ulifanya mwisho ya hii uzima mwanzo ya uzima wa milele. Unapumzika wakati kidogo miili yetu na mara ingine utaifufusha na baragumu mu Ufikisho Yako wa Mbili. Unaweka mwili yetu ya wakati kidogo ndani ya bulongo na kisha utaifufusha katika mwangaza na bila uharibifu. Ulituokoa toka laana na zambi, kwa sababu Weye ulijipokelea na ulikuwa laana kusudi wokovu wetu. Ulitupatia alama ya Msalaba juu ya kushinda shetani na hivi kuchunga nzuri uzima yetu. Kwako nilijitoa tangu hile siku nilizaliwa. Weye roho yangu ilikupenda na kwako nilitoa mwili na nafsi yangu tangu kipimo kidogo yangu mpaka sasa. Wewe, Bwana, weka na sasa pa ribeka yangu malaika wa mwangaza juu ya kuniongoza mu fasi ya pumziko, mu kumbatano ya Wapadri watakatifu. Weye uliyeleta mu paradizo munyanganyi, aliyesulumbiwa na weye pamoja, kumbuka na mimi katika ufalme wako. Kwa sababu na mimi nilisulubiwa pamoja na weye, kwa sababu juu ya woga wako takatifu nilizimisha kila matakio mabaya ya mwili yangu na mapenzi yake wa zamabi. Ee

Bwana, unihurumie kusudi kupumzika na kuwa mbele Yako, bila uchafu ao kosa. Pokea kwa mikono yako nafsi yangu isiyozambi na uchafu, sawa ubani wa harufu mbele yako.

Kama alisema hii ma sauti yake, alifunga kinywa yake na aliweka alama ya msalaba pa ma macho yake, pa masikio yake, pa roho yake. Ulimi yake pole-pole haikuweze kusema sauti, Sauti yake ilipote na paka alifungula na alifunga midomo yake bila kusikia sisi ma sauti yake. Kisha alibeba pumuzi moja nguvu na pamoja na sala yake aliisha na uzima yake.. .

Watoto wa roho wake wanawake wote, kisha lufu yake, walianza kuliya sana. Na mimi misikuweze kusimamisha machozi yangu. Watawa wengine, watoto wake waliomboleza na walimwaambia na machozi:

-Ilizimishwa taa (kandili) ya ma macho yetu! Ilipote hii nuru iliyeongoza ma nafsi yetu. Huyu alikuwa ulinzi ya uzima yetu, alama ya isiyoharibifu yetu, maungano ya mapendo na amani yetu. Ilivunjikwa ulinzi ya wasiyonguvu, ilipotea tunzo ya wagonjwa.. . Wakati alikuwa katikati yetu na usiku ilijaza na nuru kwa ajili ya nuru ya uzima yake takaitfu. Sasa nma siku ilijaza kwa sisi na ngiza.. .

Kisha sisi pamoja na kundi ya watawa wanawake tulifanya ibada ya usiku, walikuja na watu na watawa wa inje na toka monasteri ingine. Asubui alikuja na askofu ya hile njimbo, jina lake Araksios pamoja na wapadri wake. Tuliondoka juu ya kiliyo. Mimi nililamusha kitanda na maiti juu yake pamoja na askofu na mukongo yetu walikuwa wpadri wa wili wengine. Kisha mna saa madogo tulifika pa hile fasi ilikuwa kaburi yake, mu kanisa ya Washahidi watakatifu, pahali walikuwa pale na miili ya wazazi wetu mu kaburi yao. Ndani ya kaburi yao na sisi sasa tunaweka maiti ya dada wangu mutawa Mtakatifu Makrina, sawa vile na huyu hivi aliisha kuniambia.

## Mutawa muzee Anthimos

Mu monasteri ya mt. Savvas, mu inchi Palestini aliishi mutawa moja aliyepitisha uzima wa utawa wake na matendo mazuri na makubwa sana. Alikuwa toka Vithinia, fasi ya Turkia wa zamani na aliitwa Anthimos. Alijenga chumba yake mu ngambo ingine ya mutoni, mu fasi ya mashariki, ngambo ingine ya mnara ya mtakatifu Savvas. Alibakia ndani ya hii chumba miaka makumi tatu.

Wakati alizeka, aligonjwa na alianguka pa kitanda. Mwenye heri Savvas, mukuona ya kama aliisha kuanguka ma nguvu ya mwili yake, alimushauria abebe nyumba karibu ya kanisa juu ya amusaidie mtu moja. Lakini muzee alikataa.

-Ninasadiki, alisema, ya kama Mungu atachukua nafsi yangu toka hii chumba, pahali tangu mwanzo alionistahili nibakie.

Usiku moja alilamuka mt. Savvas, mbele ya saa ya Ibada ya Asubui na alisikia ma sauti, sawa walikuja toka watu wingi. Alizania ya kama watawa walianza ibada ya asubui saa ingine ya mukongo na alishangaa, kwani walifanya hivi bila wamuulize. Basi, alishuka mbio mu kanisa, lakini alipata mulango ya kufungwa! Kisha alirudia pa mnara na alisikia mara ingine ma sauti mengi ya kundi moja na waliimba na wimbo utamu kabisa. waliimba wimbo ya zaburi:

«Nitapita katika fasi wa ajabu
mpaka hekalu ya Mungu
katika sauti ya shangilio
na maungamo katika sauti wa shangilio».

Wakati alisikia toka fasi wapi ilikujaka hii wimbo, alilamusha mbio musaidizi ya kanisa na alimwaambia kupika kengele na yeye atakuja na ubani na mishumaa mu chumba ya mutawa Anthimos. Alienda nyumbani yake, lakini hasikupate hata mtu moja. Alipata paka mutawa Anthimos, aliyeisha kuisha uzima yake katika Kristu!

Walishangaa watawa wote, wenye walikuja karibu yake. Walitayarisha maiti yake na waliimba mu kanisa Ibada ya Kiliyo. Kisha walimuzika mu kaburi moja mukutukuza Mungu, aliyemutukuza watakatifu wake.

## Mutawa  mkubwa Mikaeli

karibu ya njimbo ya Arselau, karibu ya monasteri ya Mt. Ekaterina ya Mulima Sinaya aliishi mutawa Mikaeliwa inchi Iviria. Aliishi pamoja na mwanafunzi moja aliyeitwa Efstathios. Wakati aligonjwa sana huyu muzee, mtoto ya roho alisimama karibu yake kwa kumusaidia. Fasi hile waliwazika wapadri ilikuwa kule chini na njia kwake ni wa hatari na ugumu sana. Basi, alisema Muzee kwa mtoto ya roho yake:

-Mtoto wangu Efstathio, uniletee maji kunawa na kukomunika Mwili na Damu ya Kristu.

Wakati alifanya hivi mtoto wake, mara ingine alimwaambia padri Mikaeli:

-Mtoto wangu, unajua nzuri ya kama njia kwa kwenda mu fasi ya maziko ni wa hatari na ya kutelemuka na, wakati nitakufa, namna gani utanipeleka paka weye wa pekee?  Ninaogopa ya kama utatelemusha na utakufa. Kwa hivi, basi, tuende pamoja pole-pole.

Wakati walishuka, aliomba Muzee Mikaeli, alimubusu ndugu, mtoto ya roho yake na alimutakia hivi:

-Amani ya Mungu akufunike!  Omba juu yangu.. .

Alilamuka ndani ya kaburi na furaha na shangilio mingi na alitoka kwa Bwana.

## Mt. mutawa mwanamuke Melani

Mushahidi ya roho mutawa mwanamuke Melani, (383-439) mbele ya saa ya lufu yake, aliifamia na alianza kuongojea na furaha saa gani atakuja Bwana-Arusi wake, ni kusema Yesu Kristu amubebe na amupeleke karibu Yake. Alifanana sawa mushindi moja aliyefanya ushindi yake na sasa anaongojea taji yake!

Aligonjwa na haraka na alianguka pa kitanda. Hile saa alisanyika watawa wanawake wote ya hii monasteri yake na aliwaambia:

-Mimi, wa dada wangu, kisha saa kidogo nitaondoka katika mwili yangu na misitakuwe karibu yenu, lakini Mungu atakuwa daima karibu yenu!  Huyu anajua kila dada na roho yenu! Basi, mutumike na muishi katika mapendo na uzima safi mpaka mwisho ya uzima yenu.. . Munajua ya kama sisi wote tutasimama ku mbele ya Mwendo matata ya Muhukumu Yesu Kristu na kila dada atapokelea malipo juu ya michoko wake ao uhukumu juu ya makosa na zambi zake.. .

Watawa wanawake walianza kulia na kuomboleza, kwa sababu walisikia ya kama ilifika nyakati ya kutoka mama  na mwongozi ya roho yao njiani ya fazila.

Hule Mama yao aliomba na roho nguvu, hivi:

-Ee Rabi Mungu, weye unajua matendo vyote, mbele ya kutimizwa. Weye unajua namna ngapi nilikupenda na roho yangu muzima na niliishi na woga yako. Kwako, uliyeniumba mu tumbo ya mama yangu, nilitoa nafsi na mwili yangu tangu kipimo uajana. Weye ulinichunga ku mukono wangu wa kuume na uliniongoze kwa mapenzi yako. Kwani na mimi ni mutu wa zambi, nilikoa mbele yako mara mengi katika maneno na matendo. Basi, pokea sasa maombi yangu, ili ninakutoa na machozi yangu. Unisafishe mimi mutumihsi wako juu ya hapana kukuta mazibirio, hile saa nitakuja karibu yako. Misipende ma shetani waovu kuninyanganya, lakini ninataka kufika kwako bila kuniuzi, katika ongoza ya malaika watakatifu wako. Ninapenda kusikia sauti yako ubarikiwa:  «Kujeni, ninyi muliobarikiwa na Baba yangu, muriti ufalme muliotengenezewa tangu kuumbwa kwa ulimwengu». (Matayo 25, 34).

Kisha saa kidogo aliita padri ya monasteri na mbele yake alisema kwa wanawake, wa dada wake:

-Ninamiomba kuomba kwa mimi sasa, kwa sababu misikuwaze kintu kimoja kibaya ya mweye. Kama nilimifokea na sauti ukali kila wakati, niliifanya juu ya mapendo wa roho. Ninamiomba kuishi ingine waakti ya uzima yenu na ubikira na hivi Bwana-Arusi yenu, Yesu

krisu atamipenda na mutasimama na furaha mbele Yake, hile siku ya uhukumu. Ninamitoa kwa Mungu aliyekuwa na nguvu achungu ma nafsi na miili yenu. Ninamitoa kwa padri ya roho yenu na ninamiomba musimusikitishe hata kidogo. Mutafata sauti yake na utii na unyenyekevu na mutajua ya kama yeye ananyangula uzito ya ma nafsi yenu juu ya wokovu yenu katika neema ya Mungu. Kama dada moja anakataa kumusikia, analeta taabu kwa Mungu mumoja.

Siku ingine, kwani ugonjwa wake ilikuwa kuliko kibaya, aliomba na alipewa Mwili na Damu ya Kristu. Kisha alimutembelea askofu ya hii njimbo na wa padri wengine. Alisuburia na askofu saa mingi ja mafundisho wa roho.

Kisha walikuja watawa wanaume ya hile monasteri huyu aliisha kuijenga na aliwaambia:

-Ninamiaambia, hii saa mimi nitaondoka ya hii uzima na ninamiomba, kupumuzika katika utii yenu padri mkubwa ya roho yetu, kwa sababu, munajua ya kama hivi anafurahi na anapumzika Mungu katika utii yenu. Padri ya roho yetu alifanyika mutumwa wetu juu ya mapendo ya wokovu wetu.

Walikuja na wandugu na toka monasteri ingine na watu wingi toka muji. Na huyu mt. Melani, aliteswa sana juu ya maumivu yake, lakini hasikuogope. Aliwashauria watu wote wale walikuja kwake amutembelee na waombe baraka yake.

Wakati nguvu yake ilibakia kidogo, watu watakatifu wingi walikuja kwake. Walimutakia hivi: Mungu amusaidie kuweka nafsi yake katika kundi ya Watakatifu wake.

Walinamisha na walimubusu mukono yake na walimuwaambia:

-Weye ulitumika ushindani ya roho nzuri, sasa unatembea na furaha ku Bwana na malaika wote wanashangilia juu yako. Halafu sisi tunataabu juu ya hii uchanisho, kwani tunapotesha saidio na mafundisho yako.. .

Na huyu aliwajibu sauti yake wa mwisho: Sawa vile ilifanyika nzuri kwa Bwana, hivi ilitimizwa! Mara moja alitoa nafsi takatifu yake kwa Bwana wake na amani kubwa.

Vile alichukua matunda ya michoko yake na alipanda mbinguni ya kupambwa na mafazila yake.

hasikuogope hata kidogo majeshi ya ma shetani pa njia yake mbinguni, kwani wale hawakupate hata tendo moja yao kwake! Na malaika Watakatifu walikuja wamupokelea na furaha, kwa sababu alifata katika mwili yake wa uharibifu uzima yao isiyoharibika. paka na hii namna walimupokelea na Ma nabii na Mitume, kwani alitimiza mu uzima yake mafundisho yao. Na Mashahidi watakatifu, kwani alitukuza makumbusho yao, walimukuta na shangilio.

Hivi sasa anashangilia mbinguni vitu vyote, hile richo ya mtu moja haikuione na risikio haikuisikie na ndani ya roho ya mtu moja haikuingie.. .

## Mt. Mutawa Venediktos

Hile wakati mt. Venediktos alipashwa atoke ya hii uzima, alisema mbele ya wakati, kwa wanafunzi wake, hile siku ya ondoko yake ya hii uzima.

Basi, masiku sita mbele ya lufu yake, alihamuru kufungula kaburi yake na mara moja ilimubamba kivukutu na nguvu ya mwili yake kila siku ilishuka. Hile siku wa sita, alisema amupeleke ndani ya kanisa. Kule alipewa Mwili na Damu ya Kristu. Kisha alinyanyua mikono yake mbinguni na mukuona pa fasi ya mashariki, pamoja na maombi yake alituma na nafsi yake mbinguni.

Hile siku ya mwisho yake wa ndugu wa wili, moja alikuwa ndani ya nyumba yake ya monasteri yake na mwingine aliikaa mbali, waliona ono moja umoja: waliona, kila moja ya kuachana, ya kama ilifungulia njia kutoka inchi mpaka mbingu na pa njia ilikuwa chini nguo moja murefu na pempeni yake ilikuwa ma taa ya kuwaakishwa! .. . Na tazama, mtu moja na mavazi meupe alionekana na aliotembea pa hii njia na utukufu na uso wa furaha. Aliwauliza:

-Ni ninyi hii njia wa kabaila?

Na, kwa sababu wale hawakuweze kumujibu, huyu aliwaambia:

-Hii ni njia, pahali anapanda mbinguni mutumishi mupendwa ya Mungu Venediktos!

Sawa vile, basi, wale watoto wa roho yake, wenye walikuwa karibu ya mt. Venediktos, baba ya roho yao, waliona mwisho yake, hivi na wale wa wili, wenye walilofa, waliona na hawa ku mbali lufu ya padri yao.

## Askofu Provos

Askofu ya muji Reate ya muji Italia wa zamani alianguka na ugonjwa nguvu pa kitanda yake. Baba yake alienda kuita wanganga. Lakini, wale, wakati walimuhamakia, walisema ya kama atakufa na haraka.

Wakati ilikuja saa ya chakula, mugonjwa askofu, aliangalia ku saidia wa ndugu wake na hapana maungo yake. Joo vile alisema kwa wale walikuja amutembelee, waende yulu ya nyumba yake pamoja na baba yake wakule juu ya kupata nguvu. Paka mtoto moja alibakia karibu yake.

Kwa rafla mtoto aliangalia wanaume filani, waliyekuja ndani na walinyolosha mwendo yao kwa askofu. Walivaa manguo wa mwangaza na meupe! Nuru ya uso yao ilikuwa kuliko mingi ya mwangaza ya manguo yao. Mtoto, kwani alishituka juu ya hii ono, alianza kupaza sauti. Kwa ajili ya ma sauti nguvu yake, askofu mugonjwa alisimama pa kitanda kidogo, aliangalia pempeni na alifamia wale walikuja kwake. Alianza kusema kwa mtoto:

-Usiogope. Tazama, walikuja kwangu mtakatifu Yuvenalios na mt. Eleftherios Washahidi wa wili!

Lakini mtoto, kwa sababu hasikuweze kuvumilia hii maono wa ajabu, alikimbia mbio na aliaambia hii ono kwa baba ya askofu na kwa wanganga. Walishuka mbio, lakini walipata askofu mufu! Watakatifu wa wili waliisha kuchukua nafsi yake mbinguni!

## Mutawa mwanamuke Romila

Mu muji Roma wa Italia zamani waliishi watawa wanawake wa wili na mama mkubwa yao, mutawa Redemba. Moja mutawa aliitwa Romila. Huyu alikuwa kupita mkubwa mu fazila ya dada yake mwingine. Alikuwa kweli mutilivu, mwenye kunyamasha na mwenye kuomba ma siku zote!

Mara mengi watu wanazania ya kama mtu moja ni mukamilifu, lakini mbele ya ma macho ya Mungu hana mukamilifu. Eko na ma kosa na zambi filani na inapashwa kutumika nguvu juu ya kutakaswa kabisa.. Vile ilifanyika mambo na kwa huyu mutawa Romila. Katika mapenzi ya Mungu alianguka pa kitanda na ugonjwa ya kupooza! Kwani alibakia pa kitanda miaka mengi, hasikuweze kutenga vitu vya mwili vyake. Lakini huyu mutawa aliishi na uvumilia. Hasikuweze kufanya kintu na mikono na miguu yake, lakini aliongeza michoko juu ya kusema ma saa yote sala ya Bwana Yesu Kristu: «Bwana Yesu Kristu, Mwana wa Mungu, unihurumie, mimi mwenye zambi».

Usiku moja, basi, mutawa Romila aliita mama wa roho yake Redemba.

-Ee mama wangu, kuja kwangu. Kuja.

Huyu mara moja alienda kwake pamoja na dada mwingine. Hile saa waliona nuru moja iliyeshuka toka mbingu na chumba umaskini yake ilijaza na iliangaziwa yote! Walisikia tena makelele sawa iliingia ndani hasina moja ya watu wingi. Mulango ya nyumba yake sawa ilitetemeka kwa ajili ya wale watu wingi waliingia ndani. Walisikia ya kama waliingia ndani watu, lakini hawakuweze kuwaangalia, kwa sababu ma macho yao iliisha kufungwa juu ya mwangaza mingi. Hii nuru iliifata harufu wa ajabu na walifuraha sana sasa hawa wa wili!

Kwa sababu, basi, hawakuweze kuvumilia hii nguvu ya mwangaza, alianza mutawa Romila amutulivu Mama wa roho yake, aliyesimama karibu ya kitanda ya Romila.

-Usiogope, mama wangu! Misitakufe mara moja.

Wakati alisema hii sauti yake, nuru ilishuka, lakini harufu ilibakia. Vile ilipita siku ya mbili na wa tatu na harufu ilibakia.

Siku wa inne aliita mara ingine mama wa roho yake. Alimuomba amuletee Mwili na Damu ya Kristu.. . Wakati alipewa Vitu Vitakatifu, walionekana mbele ya mulango ya nyumba wake ma kundi wa wili ya waimbaji! Walisikia na ma sauti ya wanaume na wanawake. Wanaume walisema mistari (shairi) ya wimbo na wanawake waliimba wimbo. Hii majeshi ya waimbaji alikuwa mbele ya mulango na waliongojea kubeba nafsi ya mutawa Romila. Na hivi mara moja nafsi yake aliwafata mbinguni!

Hile saa alipanda mbinguni, makundi ya waimbaji walipanda ku mbele na ma sauti yao pole-pole ilizimishwa.

## Mt. mutawa Theodosios wa muji Kievo ya Rusia

Mt. Mutawa Theodosios wa muji Kievo, mujengaji ya Monasteri Lavra wa pango, alisikia mbele ya kuondoka siku ya lufu yake. Kwa hivi alihamuru wafike karibu yake kundi ya watawa wake wote. Na hawa walikuwa ma shamba na wale walikuwa kununua vitu mujini na wale walikuwa ndani ya monasteri yake.

Alianza kuwafundisha. Aliwaambia nguvu juu ya kufanya kila mutawa kazi yake na woga ya Mungu na mapendo. Aliwasuburia juu ya wokovu na uzima gani inamufurahi Mungu. Aliwaambia kuchunga kanisa safi na kuonyesha woga na matayarisho ya roho yao, mbele ya kuingia mu Kanisa. Tena kuishi na mapendo na utii hapana paka kwa watawa wakubwa, lakini na wale walikuwa na kipimo umoja. Ku mwisho aliwapatia baraka yake na aliwasalimia na machozi pa ma macho yake.

Hile saa alimutembelea na mkubwa ya inchi jina lake Zviatoslavos. Alimufundisha na huyu muzuri. Alimushauria kuchunga imani ya Kristu, kulinzi Orthodoksia na kusaidia ma kanisa matakatifu.

-Ninaomba, alimwaambia, kwa Bwana na Mungu wetu na kwa Mzazi-Mungu wakupatia uzima mu ufalme wako katika amani na ukimya. Tena ninaacha na hii monasteri yangu kwa ulinzi ya mikono yako, kwani ni Hekalu ya Mzazi-Mungu na ujengaji yake ilitokea kwa mapenzi Yake.

Kisha kivukutu na baridi ilimubamba mtakatifu mara moja. Alilaria pa kitanda. Mpaka hile siku hasikularie hata mara moja mu uzima yake.

Alisema: mapenzi ya Mungu itafanyika. Bwana atafanya kila matakio yake kwa mimi. Lakini, ninakuomba, ee Rabi wangu Yesu Kristu, juu ya kuonyesha wema wako kwa nafsi yangu. Ninakuomba malaika wako wamupokelee na hapana ma shetani walimubamba. Malaika wako, ninakuomba, wamupitishe katikati ya ma duani ya ma shetani wa ngiza na watamupeleka mu nuru ya huruma wako.

Kisha hii ma sauti yake alisimama kusema. Alikuwa na unyamasha. Hasikuweze kusema sauti moja. Wa ndugu wake na umivu ya roho waliangalia hii hali yake, iliyekuwa na ma siku tatu.

Kisha ma siku tatu, ugonjwa ilishuka kidogo. Wa ndugu wake walikuja karibu yake mara ingine.

-Wa ndugu na wapadri, aliwasema, sasa wakati ya uzima yangu inaisha. Aliisha kuniambia Bwana Yesu, hile wakati ya Kwarezima niliomba mu pango yangu. Hile kintu niliomba ya mweye ni hii: Mutasanyikwa yote juu ya kuchakula padri mkubwa wenu mupya na mimi nitamuweka pa kiti yangu.

Wakati walisikia hii ma sauti yake wa ndugu walisikia huzuni ya roho na walianza kulia. Wote pamoja walichakula padri Stefano sawa mkubwa baba ya roho yao, aliyekuwa mpaka hile siku musaidizi ya kanisa. Siku ingine mt. Theodosios aliita kundi ya watoto wake na aliwaita:

-Watoto wangu, mulikamata mpango gani? Munachakula mtu gani sawa mkubwa yenu?

-Padri Stefanos ni mustahili, walisema wote na kinywa moja.

Mtakatifu aliita karibu yake padri Stefanos, alimubariki na mkono takatifu yake na alimupatia cheo ya kuwa padri mkubwa yao.

-Sasa mtoto wangu, alimwaambia, ninakupatia pa mikono yako Monasteri! Utachunga nzuri ma sheria ya uzima utawa. Utachunga mapokeo ya uzima yetu muzuri. Usigeuze desturi ya ma Ibada ya kanisa yetu, lakini utatumika katika kutim na sheria yetu.

Kisha aliwaita wa ndugu wote na aliwashauria kumutii padri mkubwa yao mupya. Ku mwisho aliwaambia na mwisho ya uzima yake.

-Mu Posho, hile saa Jua atashuka chini, nafsi yangu itaacha mwili yangu.

Mtakatifu alisikia ya kama pole-pole ugonjwa ilianza kumubamba nguvu. Padri mkubwa mupya Stefanos alikuwa karibu yake, na alimusaidia na unyenykevu. Alisikia na ma shauria yake juu ya kutumika muzuri kazi kipya yake.

Mu posho asubui aliita wa ndugu wote na alisalimia moja moja ya kuachana. Kisha aliwaambia hapana kumusifu, kisha lufu yaa mwili yake.

-Na sasa, ninamiomba, mutanizika ndani ya pango yangu, pahali nilifanya ma sala yangu hile ma siku ya kifungo. Musinawe mwili yangu, wala kutosha manguo yangu na mutavaa manguo mapya. Tena hata mtu mwingine misipende kufika mu kiliyo yangu, paka mweye.

Wa ndugu wote walipokelea ma sauti yake na machozi na maombolezo. Hule, juu ya kuwatulivi, aliwaambia:

-Ewe ndugu wangu, ninamilaka, haina mambo kwani ninatoka na mwili yangu, lakini na roho yangu nitakuwa ma siku zote karibu yenu.

Hii saa aliacha wa ndugu watoke. Alitaka abakie paka huyu wa pekee. Ndugu moja, aliyemusaidia hii ma siku ya mwisho yake, alibakia kwake na aliangalia hii ma saa ya mwisho yake:

Mtakatifu alilamuka ku kitanda lake, alipika magoti na alianza kuomba na machozi kwa Mungu Mwema amuokoe nafsi yake. Aliomba mbele ya Watakatifu wote na kabisa kwa Mzazi-Mungu, kwa ulinzi wake aliacha monasteri na kundi ya wandugu wake. Kisha alilaria pa kitanda mara ingine juu ya kupumzika kidogo. Kisha saa kidogo alisimama kidogo pa kitanda. Aliangalia mbingu na uso yake ilijaza na furaha. Hile saa na sauti nguvu alisema:

Mungu ni Mubarikiwe! Kama ni vile, misiogope hata kidogo. Lakini ninafurahi kabisa juu ya ondoko yangu ku dunia hii.

Bila shaka, aliona ono moja ya ajabu. Kisha alilaria pa kitanda yake. Aliweka mikono yake osawa alama ya msalaba na alitoa nafsi yake kwa Mungu.. Hii siku ilkikuwa mu Posho, magaribi, mu tarehe 3-5-1074. Waaminifu wingine, wakati waliskia ya kama alikufa baba ya roho yao, walikuja kule. Tena walikuja na wakubwa ya inchi. Wote walimbakia inje ya monasteri, kwa sababu watawa waliisha kufunga mulango katika sauti ya baba ya roho yao. Waliongolea pale juu ya kufata kundi ya watawa mu maziko yake. Lakini hakuna namna kufanya watawa maziko yake. Mungu alitengeneza hii mambo. Ilinesha nvula mingi. Waaminifu wote walikimbia. Hile saa watawa walipeleka maiti ya baba wao mu pango yake na alimuzika na masifu mengi. Walirudia na jua ilionekana sasa mara ingine. Hile siku walitaabu sana na hawakukule hata kidogo.

Mkubwa ya inchi Zviatoslavos alikuwa mbali, hile siku alikufa padri mkubwa Theodosios. Lakini topka mbali aliona ono moja. Aliona ya kama yulu ya monasteri ya Lavra yake aliona nguzo (kolone) moja murefu iliyekuwa toka monasteri mpaka mbinguni.. Katika hii ono alisikia huyu mkubwa yaka Mtakatifu aliacha hii uzima na alipanda mbinguni.

## **Mutawa mwanamuke Theodoti**

Theodoti alikuwa mama ya mwenye hekima mtu, jina lake Mikaeli Pselos, aliyeishi mu mji Konstantinopoli (1018-1078).

Huyu alikuwa mwema sana na mwaminifu wa kweli. Alipendeza kuita nyumbani yake wamaskini, hapana juu ya kutukuzwa ya watu wengine ao juu ya kunyenyekesha wamaskini. Huyu mama alijua kusaidia katika amri ya Mungu. Aliwapokelea mumoja wamaskini, aliwanawa miguu yao, aliwasaidia wagonjwa, na mapendo mingi sawa wale walikuwa wakubwa ya inchi! Alisoma ma siku zote Madiko Takatifu. Kila siku, asubui, magaribi alifanya sala wa moto. Nafsi yake alipanda kwa Mungu na aliona maono wa ajabu.

Kabisa alitumika juu ya kukomesha muzuri mtoto wake Mikaeli tangu kipimo kidogo zake. Alikombana tangu miaka madogo yake kumufundisha kuwa mtoto wa heshima na wa akili. Kila magaribi, alimuelejea ma hadisi toka Agano la kale na Agano Jipya na uzima ya Watakatifu wetu.

Na kisha lufu ya bwana wake, mapendo yake juu ya mtoto yake ilikuwa kuliko mingi. Kwani alifanya kifungo mingi, baba yake alimutuma chakula. Lakini huyu aliita wamaskini na aliwapatia chakula zake. Hivi kila siku aliisha kukonda sana. Juu ya aende mu Misa, ilipashwa amukamate watu wa wili!

Hasikukuwe mutawa, kwa sababu alizania ya kama hana mustahili ya hii sifa munene. Lakini alipenda sana kuwa mutawa. Lakini ndoto moja ilimusukuma kukamata na haraka mpango yake.

Usiku moja aliona ya kama rafiki yake moja mwanamuke alikuwa mu hile fasi wanakimbia ma punda ya inchi. Alizania, ya kama alikuwa ndani ya nyumba ya mfalme na pale aliona kiti moja wa ajabu na wa zahabu. Pempeni yake, mu fasi ya kuume na kushoto ilikuwa na viti vizuri vingine. Aliuliza hii kiti wa katikati ilikuwa ya mtu gani?  Sauti moja ilimujibu hivi:

-Hii kiti ni ya Theodoti. Mufalme, nikusema Mufalme ya mbingu, Yesu Kristu, alihamuru hii kiti inapashwa kuwa tayari, kwa sababu kisha saa kidogo atakuja kuikaa Theodoti.

Hii ilikuwa tangazo juu ya lufu wake na haraka!  Hile saa Theodoti alikamata mpango kufanyika mutawa.

Ibada ya ndoa wa roho ilikuwa wa furaha na kubwa!  Kanisa ya Monasteri ilikuwa ya kupambwa muzuri!  Watawa wanawake walijaza ma kundi ya waimbaji. Mikaeli Pselos, mtu mkubwa ya inchi, alikuwa na huyu mbele yake, mu mustari wa kwanza. Watu wote walishangaa, kwa sababu walimuona Theodoti kusimama, lakini aliisha kulekea sana!  Alitembea ku mbele na uso wa mwangaza, pasipo kumukamata mtu mwingine. Na hile saa ya Ibada ya utawa alikuwa ya kusimama. Mtoto wake, Mikaeli, kisha ya kufata mama yake uzima ya utawa, alianguka mbele ya mama yake, mutawa Theodoti na aliomba baraka yake. Mama yake alimwaambia:

-Ninakutakia, mtoto wangu na weye kupima hii furaha na neema ninasikia sasa mimi, mama yako!

Hii saa uso yake iligeuza ragi na mwangaza ilijaza ma macho yake. Ilikuwa mwisho yake! Alipenda kuikaa kidogo na aliikaa pa kiti kimoja. Pale alilala na amani pumuziko wa milele.. .

Muji Konstantinopoli muzima ilikuja mu kiliyo yake. Watu wote walikombana kubusu mwili wake, mikono na uso ya mutawa mtakatifu Theodoti.

## <u>**Mt. Mutawa Simeoni wa inchi Servia**</u>

Mtawa Simeoni, aliyekuwa zamani mufalme ya inchi Serbia, aliacha ufalme wake na alikuja mu Kilima Takatifu, karibu ya mtoto wake, padri Savvas. Aliishi mu monasteri yake Khilandarion. Aligonjwa mu mwezi ya mbili ya mwaka 1200. Alisikia ya kama mwisho yake inakuja. Hile saa aliita mtoto mupendwa wake na alimwaambia:

-Mtoto mupendwa wangu, nuru ya ma macho yangu, utulivu na ulinzi ya uzee wangu, ilikaribia saa ya ondoko yangu ya hii uzima.. .  Usitaabu, mtoto yangu juu ya hii ondoko, kwa sababu na mara ingine sisi tutakutana, pa hile fasi hasikukuwe uchanisho, mu Paradizo!

Aliweka mikono yake pa kichwa ya mtoto wakle, aliomba kwa Mungu saa mingi. Kisha alimubatia, alimubusu mara ya mwisho na alimwaambia ma kazi fulani inapashwa kusopoka na

kuimaliza. Tena, alimwaambia, mifupa yake, kisha maziko, ataitosha na ataipeleka mu monasteri ya Studenicha ya Serbia. Mtoto wake, padri Savvas, alimukikisha ya kama atafata ma sauti yake yote.

Kisha mutawa Simeoni aliita wa ndugu wote na alianza kuwabusu moja moja. Aliwashauria wote wamuombe kwa Mungu juu ya wokovu wake. Tena aliwaambia ya kama atawaacha kwa mikono ya Mungu na Mzazi Wake.

Usiku alivaa nguo takatifu ya uzima wa utawa, alikumunika Mwili na Damu ya Kristu na aliomba kwa Mungu.

Wakati alikuja asubui mapema, mtoto wake alimupeleka mu kipande wa kwanza ya kanisa, inayeitwa Pronaos ao Narthikas. Kwani, alisikia muzee ya kama saa yake wa mwihso ilikuja, alisema kwa mtoto wake, padri Savvas:

-Mtoto wangu, uniletee Picha ya Mzazi-Mungu, hile ni pamoja na Yesu Kristu, kwa sababu nilimuwaambia ya kama ninataka kuacha nafsi yangu mbele ya hii Ikone.

Wakati matakio yake ilitimizwa, mt. Simeoni alisema:

-Mtoto wangu, fanya mapendo na univae raso (nguo meushi) juu ya maziko yangu. Tayarisha mwili yangu juu ya kuwa mimi tayari ya maziko yangu. Chini ya kichwa yangu weka riimbwe moja na chini moja nguo. Vile nitaongojea mpaka atanitembelea Bwana wangu. Pempeni yake walisimama wa ndugu wake na waliria, kwa sababu kisha saa kidogo, watabakia yatima, bila baba ya roho yao.

Mt. Simeoni, aliwaambia hapana kuliya. Uso yake ilijaza na mwangaza! na furaha mingi aliangalia Picha ya Bwana Yesu na Mzazi wake. Aliimba pamoja na misafiri wasiyoonekana. Ku mwisho ya hii zaburi aliimba, alisema: «Kila mwenye pumuzi, amsifu Bwana».

Watawa wengine walisikia ya kama mt. Simeoni anaondoka ya hii uzima na wimbo wa malaika na utukufu kwa Mungu. Kisha saa kidogo pepo ilijaza na harufu nzuri na wale walikuwa pale pempeni walishangaa. Vile alilala katika Kristu mu tarehe 13 Februarie (Mwezi ya mbili) ya 1200.

Hile saa mtoto yake, padri Savvas, alianguyka yulu ya mwili yake na alimimiya na machozi yake wa moto. Kisha alikamata mikono yake aliibusu na aliiweka pa kilari ya baba yake. Kisha pamoja na kundi ya watawa walimuzika ndani ya kanisa mu kaburi muzuri, hile ni mpaka sasa mu Kanisa ya Monasteri yao ya Kilima Takatifu.

Kisha ya kulala mt. Simeoni, mtoto wake, alimuomba kila usiku amupatie tangazo moja juu ya wokovu wake. Na kweli usiku moja alimuonekana mt. Simeoni pamoja na malaika na walikuwa ndani ya utukufu na mwangaza mingi. Alivaa mt. Simeoni taji moja wa utukufu na alitaka kumusimamisha mtoto wake toka taabu yake. Na alimuelejea na furaha:

-Usiliye na usitaabu juu ya mimi, mtoto wangu mupendwa, lakini uwe na furaha na shangilie, kwa sababu, tazama, Mungu katika maombi yanko, anakuelejea juu ya mimi! Sawa vile na weye unaniona Bwana mwema alinitukuza na vitu vitakaitfu ya uzima wa milele mu ufalme wake. Nilipata hile ulinisema hile wakati nilikuwa pamoja na weye. sasa ninafurahi na ninapata furaha isiyo na mwisho. Ninakutakia kuwa mubarikiwa toka Mungu, kwa sababu ulinisaidie kuingia na mimi mi uzima wa milele»

## Mt. Mutawa Theodora wa Sykhla ya Rumania

Mt. Mutawa Theodora wa fasi Sikla ya Rumania alizaliwa mu mukini Vinyatori ya njimbo Neamchu ya Rumania katikati ya milelekumi na saba.

Aliowa bwana moja, jina lake Eleftherios, lakini, kwa sababu hawakuweze kuzala watoto, wote wa wili waliingia mu monasteri ya kuachana ku fata uzima utawa.

Theodora aliingia mu monasteri Kidogo Varzaresti, lakini bwana wake mu monasteri Mare Poyana. Kisha wakati kidogo monasteri ya Theodora, ililungua na huyu aliingia mu pori na

alikuwa mutawa ya jangwa ya nyakati miaka 30, ndani ya pango moja., sawa zamani mt. maria wa Misri.

Aliishi bila kumufamia watu na alikuwa na kitumaini yake paka kwa saidio ya Mungu! Alikombana ma shetani ndani ya pango yake sawa malaika. Kisha miaka mengi, ma shetani walisimama kumuuzi na kumukombana. Na huyu mutawa asisikie baridi wala njaa. Anaomba bila kusimama kwa Mungu kila siku. Na akili yake anaona ma fumbo matakatifu, na uso yake inajaza na mwangaza. tena, wakati anaomba, mwili yake inanyanyua yulu pa pepo, sawa mwili ya mt. Maria wa Misri!

Manguo yake iliisha kuharabika. Tena na chakula hake hakuna namna kuitafuta. Kwa hivi ma ndege ya mbingu walianza kufanya hii kazi. Na amri ya Muumba Mungu wetu, kila siku walikamata vipande-vipende vidogo mikate toka meza ya monasteri Sikhastria na waliipeleka mu pango ya mt. Theodora. Mt. Theodora alifanya maombi juu ya dunia mzima na alifuraha kwa sababu kisha ma siku filani ataondoka ya uzima na mwili yake.

Ma siku makumi inne (40), mbele ya mwisho yake alimuomba kwa Mungu amutume padri moja juu ya kupewa Mwili na Damu ya Kristu. na Bwana Yesu hasikumuache matakio yake bila kuitimiza.

Siku moja, ndugu wa wili ya monasteri Sikhastria walifata ma ndege kuangalia wanaenda wapi hii mikate pa pua yao. Vile, waliwaza ya kama atakuwa mtu moja mu pori. Walimutafuta huyu mt. Theodora. Huyu aliwaambia:

-Musiogope, wa ndugu wangu. Mimi ni mutumwa ya Mungu munyenyekevu. Lakini, ninamiomba, munipatie nguo yenu moja juu ya kuvaa, kwani mwili yangu ni utupu.

Kisha aliwaita kusuburia na hawa. Aliwaelejea mateso na jambo ya uzima yake na aliwaambia ya kama mwisho ya uzima yake inakaribia. Aliwapatia amri waseme kwa padri mkubwa ya monasteri yao atume padri Antonio na shemasi Lavrentios na Vitu Vitakatifu juu ya kukomunika mara ya mwisho.

-Namna gani tutaenda mu monasteri hii usiku, walimuuliza wa ndugu, kwani tusijue njia?

-Mufate hii nuru munaiona mbele ya ma macho yenu na mutafika na haraka.. .

Asubui mapema ya siku ingine walienda mu pango yake p. Antonio, shemasi Lavrentio na hawa wa wili. Walimupata Mt. Theodora kuwa chini ya muti moja. Huyu aliwambia juu ya uzima yake. Alisema Simvolo ya Imani: «Nasadiki Mungu moja.. . », alipewa Mwili na Damu ya Kristu na mara moja alitoa nafsi yake kwa mikono ya Kristu. Mara moja mwili yake ilijaza na harufu muzuri! Walimuzika ndani ya hii pango aliisha miaka makumi tatu.

Mwili yake Mungu aliitukuza na isiyoharibifu. Tena alitosha harufu na alifanya miujiza mengi! Ilibakia ndani ya Pango yake miaka miya moja (100). Kisha miaka kidogo, katika mapenzi ya Mungu, mwili yake ililekea. Ku mwaka (1828-1834) walipeleka Mifupa Matakatifu yake mu monasteri Lavra ya muji Kievo ya Rusia. Na mpaka sasa kule ni mifupa mtakatifu mwake na yulu yao ni mandiko moja inayeandikwa: «Mt. Theodora wa milima Karpathia».

## Mt. Mutawa Serafim wa Sarofi ya inchi Rusia

Mu tarehe 1 Yanuarie ya mwaka 1833, siku ya Juma ya Mungu, alikuja mt. Serafim mara ya mwisho mu kanisa ya Watakatifu Zosima na Savatios. Aliwaakisha mishumaa mbele ya ma picha ya Watakatifu wote na aliiabusu na hii kazi alifanya mara ya kwanza. Alipewa Mwili na Damu ya Kristu na kisha Ibada ya Liturgia aliomba hurumia ya wale wa ndugu walikuwa kule. Aliwabariki, aliwabusu na aliwatulivu. Kisha aliwaambia:

-Ninamitakia kuokolewa. Musiishi na uzaifu. Mutumike kwa wokovu wenu. Mungu alitayarisha ma taji juu ya mweye!

Kisha saa kidogo inje ya kanisa alimutembelea mutawa mwanamuke Irini Vasilievna. Mt. Serafim alimupatia makuta kidogo na alimwaambia:

-Hii makuta utamupatia kwa mutawa mwanamuke Paraskevi juu ya kununua mukate kusaidia mukini fulani.

Hile wakati mali ya monasteri iliisha kuisha na watawa wanawake walikuwana mambo munene juu ya maisha yao.

Padri Serafim hasikuwa na musaidizi ya nyumba na maisha yake. Kila waakti alimusaidia padri Paulo, aliyeikaa karibu yake. Huyu p. Paulo alisema juu ya padri Serafim, ya kama ataingia mu ufalme mbinguni, bila muchoko na ugumu. Hasihukumu hata mtu moja! Anajua paka zambi yake na uzima wa bure wake.

Mt. Serafim, wakati aliondoka mu jangwa, mu nyumba yake mu monasteri, aliwaakisha mishumaa bila kuizimisha. Padri paulo aliisha amuwaambie mara mingi ya kama mishumaa ya kuwaakishwa ni hatari ya moto na kulungua wote. Padri Serafimi alimwaambia:

-Mpaka mwisho ya uzima yangu haitakuwe moto. Halafu, kama nitakufa, lufu yangu mutaisikia na alama ya moto.

Mu tarehe 1 Mwezi ya kwanza ya 1833, mt. Paulo alimuona mtakatifu Serafim ya kama alienda mara tatu pa kaburi yake. Aliikaa kule na aliangalia saa mingi. Usiku padri Paulo alimusikia padri Serafim kuimba wimbo ya ufufuo ya Kristu nyumbani yake.

Mu tarehe 2 Mwezi ya kwanza, asubui saa wa sita, hile wakati padri paulo alikwenda mu kanisa, aliona kutoka simoko ku nyumba ya padri Serafim. Alimuita na alianza kukokola mulango. Mulango ilikuwa ya kufungwa ku ndani na jibu asikusikie. Alienda hile saa mu balkon na aliona ndani ya ngiza paka wale watawa walienda mu Misa.

-Ee Wa ndugu na wapadri, aliwaita. Ninapumuzi harufu ya simoko. Ninazania ya kama padri Serafim aliisha kuondoka mu jangwa na nyumba yake ilianza kulungua na moto.

Ndugu moja, jina lake Anikitos, alibomoa mlango ya chumba yake. Aliingia ndani na aliona ya kama moto mkongo ya mulango yake. Inje ilikuwa ngiza. Nyumba ya padri Serafim haikukuwe moto ya kuona huyu ndugu Anikitos kama yeye (padri Serafim) alikuwa ndani. Asikumuone na hasikumusikie. Watawa wengine walizania ya kama padri Serafim alipumzika. Walimutafuta ndani ya ngiza ya nyumba yake. Walimupata. Aliisha kufa! Alikuwa na fasi ya kusimama mbele ya ma Picha ya Watakatifu. Aliisha kuvaa nguo urefu meupe, bila kofya na msalaba pa sigo yake na mikono yake katika alama ya msalaba pa kilari yake!

Walizania ya kama alilala pa hile fasi ya maombi yake. Walimusukuma, lakini hakuna jibu yake. Ma macho yake ilikuwa ya kufungwa na uso yake ilijaza na mwangaza ya Mungu. Mwili yake ilikuwa tena na kivukutu.

Watawa na baraka ya padri mkubwa walimunyanyua maiti yake, waliitengeneza na waliipeleka mu kanisa kubwa ya monasteri. Tangazo ya lufu ya mtakatifu Serafim ilienda ma fasi yote na haraka. Watu wote walitaabu juu ya lufu yake na walilia sana. Walitaabu kabisa watawa wanawake ya monasteri yake Ntiveyevo.

Maziko ya mt. Serafim ilifanyika na padri mkubwa Nifoni. Hakuna mahubiri mu maziko yake. Ukumbusho ya uzima na matendo yake na mahadisi hile walisema hile saa ya maziko yake ilikuwa fundisho kupita kubwa na ilikombola kila kuhubiri.

## **Watawa wa kumi ya Mulima Takatifu**

Katikati ya monasteri Iviron na jangwa ya Milopotamos mu Kilima Takatifu ya grekia, ndani ya pori ilikuwa nyumba moja wa Watawa na kanisa ya Utatu Mutakatifu.

Padri mukubwa na watawa tisa waliishi pamoja sawa kundi moja katika mapendo na heshima. Kwa ajili waliishi katika mapendo, walimuomnba Mungu juu ya kufa na wote pamoja.

Siku moja watawa wengine waliyeikaa pempeni yao, waliona ya kama hakuna mutaw aya kutoka inje, sawa kila asubui. Walienda ku mulango na katika desturi waliwaita na ombi: Kwa maombezi ya Watakatifu wapadri wetu.. . » na waliongolea jibu, ni kusema neno: «Amina», lakini hakuna jibu yao! Hile saa tatu watawa waliingia ndani poole-pole. Walipumuzi harufu

kutoka ya fasi moja. Walienda mu Misa na waliona pempeni ya padri mkubwa yao watawa wote pa hile fasi waliomba kila usiku hurumia ya padri mkubwa wao. Waisha kufa wote pamoja na padri mkubwa yao!

Walibakia pa hile fasi ma siku kumi na tano, bila kukauka sawa vile inafanyika hii mambo kwa wafu wote! Tena walitosha harufu nzuri sana.

Wale watawa waliwazika katika sheria ya Kanisa yetu sawa waliwapata nikusema na hile manguo na kofya na vilato vyao. Vile na silaha ya roho waliondoka ya hii uzima na waliingia mu uzima wa milele.

## Mtakatifu Parthenios wa Kisanga Khios

Ilikuja nyakati na mt. Parthenios alipokea tangazo ya ondoko yake ya hii uzima. Huyu alipenda sana mu uzima nzima yake hii safari wa mbingu. Siku ya furaha ilikuwa hile siku ya safari yake mbinguni. Iliisha kupitisha wakati ya miaka 45 ya uzima utawa. Tangu kipimo ya miaka yake 23 mpaka mu kipimo yake sasa miaka 68 aliishi uzima nguvu katika mapenzi ya Kristu.

Usiku moja, wakati alipumzika usiku ndani ya pango yake, ndoto moja ilimushituka na ilimufurahisha. Aliona Mzazi-Mungu Mama Maria!

-Ee Parthenie, alimwaambia, kisha ma siku tatu fasi ya pumziko yako itakuwa tayari. Watakatifu wanakuongojea!

Mtakatifu mutawa Parthenios alilamuka. Alizania ya kama alisikia tangza wa mbingu toka kinywa ya Mama Bikira Maria.

-Misikufanye kintu kizuri mu uzima yangu, alisema na sasa alikuja Mama mkubwa ya wa malaika anitangaze juu ya ondoko yangu mu uzima wa milele?

Vile alisemaka juu ya unyenyekevu wake. Alilamuka, Alisema hii tangaza na kwa watawa wengine.

-Kisha ma siku tatu, nitakufa, aliwaambia:

Hile siku wa tatu, alilaria pa kitanda, ilikuwa mu tarehe ya 8 Mwezi kumi na mbili ya mwaka 1883, biula ugonjwa ya kumuteswa. Alipewa Mwili na Damu ya Kristu.

-Walimuuliza, unataka wapi juu ya kukuzika sisi?

-Mutanichukua na muguu yangu moja na mutanitupa ndani ya mutoni, aliwaambia na unyenyekevu.

Mbele ya mwisho ya uzima yake, walikuja Watakatifu na Watawa toka mbinguni juu ya kumusidikiza mu nyumba yake mu mbingu. Huyu Mutawa Parthenios aliwasalimia hivi:

-Wafu wako, wakubwa wangu, wafu wako.. . Na sauti yake wa mwisho ilikuwa hii: «Natumaini ufufuo wa wafu.. . »

Walikuja watawa wote na waaminifu ya hii Kisanga juu ya kumusalimia padri na mwongozi ya roho yao.

Wagonjwa waliponyeshwa, wakati walimuomba na imnai mu maziko yake na walibusu mwiti takatifu yake. Walimuzika ndani ya kipande wa kwanza ya kanisa ya monasteri. Alipanda mbinguni tena na mtakatifu mwingine! Maiti yake ilitosha harufu nzuri. Nafsi yake ilifurahi karibu ya Kiti ya Mungu Mwenyezi. Mama Maria alimupokelea mutumishi wake sawa amalaika.

## Mutawa Silvestros

Mutawa Silvestros alikuwa mu monasteri Nturau ya inchi Rumania. Alikuwa mutilivu na munyenyekevu na alisaidia watawa wote katika ma fazila na tabia takatifu yake. Hasikujue ma fundisho mengi. Aliomba ma siku zote na alitumika ma shamba. Alikuwa na heshima kubwa kwa Mazi-Mungu. Mbele ya Picha yake alifanya sala kila siku.

-Ee Mama wa Bwana wangu, unisaidie mimi mwenye zambi!  Mama Mzazi-Mungu, unipe mwisho muzuri!

Kisha alibusu Picha yake na aliende mu kazi yake. Wakati aliku na kipimo miaka makumi tisa (90), alipotesha nguvu ya kusikia. Lakini hasikulofe ku Kanisa. Siku moja Wapadri walimuuliza:

-Namna gani unalamuka usiku, padri Silvestro na unakuja mu Misa, kwa sababu usisikie kengele?

-Ananisaidia mimi Mama Mzazi-Mungu. Wakati ninalaria pa kitanda yangu juu ya kupumzika, ninaserma kwa Mama Maria:  Mama Mzazi-Mungu, unilamuka usku juu ya sala takatifu!  Na usiku, wakati kengele ilipikwa, alikuja kwangu mtu moja, alinigusu pa manguo yangu, alinisukuma kidogo na mimi nililamuka mara moja.

Wakati ingine alisemaka hivi kwa wapadri ndugu wake:

-Halafu, juu ya ninyi inachelewa kuja na kwa mimi lufu?  Ninawaza ya kama mimi niko mtu mwenye zambi kabisa na Mungu bado kunihurumia!  Ee wapadri ndugu wangu, mumuombe kwa Mungu juu ya mimi.

Aliishi mu monasteri kuliko mengi ya miaka makumi mbili. Watawa wote walimupenda, wani alikuwa mufazili na musiyeroho mubaya. Na, sawa vile uzima yake ilikuwa takatifu, vile na mwisho ya uzima yake ilikuwa takatifu.

Mu waakti ya nvula ya mwaka 1919, hile saa Waimbaji waliimba mu Kanisa:  «Uliye wa thamani kwashinda waKheruvi.. .  », padri Silvestros alifanya metanies (kupika magoti), mbele ya Picha ya Mzazi-Mungu. Kisha alipika magoti chini na alinamisha na kichwa yake chini. Wapadri wengine walizania ya kama alipumzika. Ku mwisho ya Ibada ya asubui walimukaribia na walimuwaambia:

-Ee.  Silvestro, lamuka, simama, ibada ya Asubi iliisha!

Lakini padri Silvestros aliisha kutoka nafsi yake kwa Mikono ya Mungu na Mzazi wake Mama maria!

Hile saa wapadri walimufunika na nguo yake, walimuweka katikati ya kanisa na siku wa tatu walimusidikia mu inchi wa milele.

## Padri Mkubwa Athanasios

Mu Mwezi kumi na mbili ya mwaka 1953 ilifika saa na siku juu ya kuondoka ya hii uzima padri mkubwa ya Monasteri ya Mt. Grigorio ya Kilima Takatifu, padri Athanasios. Aliisha kufika na kipimo yake miaka makumi mnane (80) na alianguka pa kitanda yake. Ma siku ya mwisho yake hasikuweze akule kintu, paka aliishi na Mwilina damu ya Kristu kila siku!  Akili na roho yake walikuwa daima mu ono ya sala. Kila waakti alinyanyua mikono yake mbinguni, alibariki watawa sawa alifanya Ibada ya Liturgia takatifu.

Ma siku mbili, kisha Siku Kuu ya Kuzaliwa Kristu alisema kwa musaidizi wake, padri Artemios awaita watawa wote pempeni yake. Alitaka awasalimia, kwani alisikia karibu mwisho yake. Na kweli walisanyikwa..

-Ee Muzee na baba wetu, alimwaambia mufwasi yake, padri mkubwa Visarioni, kama utapata uwezo mbele ya Mungu, na utapata bila shaka, usitusahau.

-Kama nitapata uwezo, nitakukumbuka na weye na wapadri wote nitamikubusha.

Sasa kujeni karibu yangu moja-moja juu ya kusalimiwa na kuhurumiwa. Watawa, watoto wa roho yake, walimusalimia na walibusu mukono na walibeba baraka yake:

-Matakio yako karibu yetu, walimuwaambia.

-Njia muzuri mu Paradizo!

-Mapatano muzuri mbinguni!

Siku ingine asubui alikuw akidogo muzuri. Mungu alimupatia kidogo nguvu juu ya kutayarisha manguo ya mwili yake, mbele ya lufu yake. Alilamuka, alinawa mwili na uso yake. Alivaa manguo mapya. Na manguo ingine aliipatia kwa musaidizi ya wazee na alimusema:

-Beba hii manguo misina na lazima yao.

Mutawa moja kijana, kwani alimuona ya kama hile siku alisikia kidogo nzuri, alimukaribia juu ya kuungama na alimuuliza:

-Ee Muzee, namna gani unajua ya kama hii usiku utaondoka mu uzima wa milele?

-Mtoto wangu, hii usiku ninaondoka! Hii ni wa kweli. Nilikamata tangazo. lakini namna gani. Usiniulize.

Kisha, kati ya muchana, aliita padri mkubwa mupya, na alimwuelejea:

-Padri Visarioni, kisha ma saa madogo, nitaondoka. Weye fanya nguvu kusaidia wa ndugu wetu na Mzazi-Mungu atakusaidia. Uende sasa unilete huku Mwili na Damu ya Kristu.

Kisha alisema kwa mutawa kijana Andreas, aliyetaka amuvaa manguo yake mapya:

-Padri Andrea, usinitosh manguo yangu, kwa sababu nilivaa manguo mapya. Paka utachona manguo yangu na shindano na kazi yako iliisha.

Alipewa Mwili na Damu ya Kristu na ma sauti yake ya mwisho ilikuwa: «Ee Bwana wangu, unipokee leo ku Karamu yako ya mwisho.. . ». Kisha Komonyo Takatifu hasikusema neno ingine. Alikuwa na unyamasha na sala kwa siri.

Ilifika magaribi. Watawa wote, kisha sala ay Apodipnon Kidogo, walipanda mu chumba yake. Uso ya padsri mkubwa yao ilijaza na nuru kimungu. Huyu aliweka mikono yake pa kilari sawa alama ya msalaba. Alifunga ma macho yake na kishaa saa kidogo ndani ya amani kitakatifu na utulivu alitoa nafsi yake kwa mikono ya Mungu.

## <u>Mutawa Yosefu wa Pango (Spileotis)</u>

Mutawa Yosefu wa Spileotis aliishi mu Kilima Takatifu mu jangwa na ndani ya ma pango uzima moja kabisa ugumu na michoko mingi juu ya kupata neema ya Mungu.

Sasa ku mwisho ya uzima yake, aliisha kuzombelea fumbo ya lufu na aliiongojea sawa siku kuu moja! Alikuwa na tangzazo ya kama Mungu atamuhurumia, lakini ku mwisho yake alilia sana. Juu ya kumubebelesha mutawa yake moja, padri Arsenios alimwaambia:

-Ee Muzee, michoko mingi na ma sala mingi ulifanya mu uzima yako na machozi tena kuliko mingi.. . na sasa unalia mara ingine?

-Ee Muzee Arsenie! Ni kweli ma sauti yako, lakini na mimi niko mtu. Namna gani ninajua ya kama hii matendo nilifanya walimufurahisha Mungu? Huyu ni Mungu, Hasihukumu sawa sisi watu. Kama nilimusikitikisha na kosa yangu fulani, nitafanya ninyi? Nitaweza kurudia huku juu ya kutubu? Hapana. Basi, kila mtu inapashwa kutengeneza mambo ya wokovu yake.

Mapendo ya padri Yosefu mbele ya Mazai-Mungu ilikua munene. Kama alikumbuka jina lake, aliliya juu ya mapendo. Alimuwaambia tangu zamani amuvhukue juu ya kupumuzika na Mzazi-Mungu alimusikia maombi yake! Alimutangaza mwezi moja, mbele ya lufu yake ya kama atamubeba. Pumuziko wa milele yake itakuja mu Siku Kuu ya Kulala Mzazi-Mungu 15 Mwezi ya Mnane 1959.

Siku moja mbele ya kulala yake alimutembelea rafiki moja, mwaaminifu toka muji Volos ya Grekia, jina laki Sotiris Skinas na alimuuliza:

-Munafanya ninyi, ee Muzee. namna gani ni afya yenu?

-Kesho, Sotiri, ninaondoka mu inchi wa milele. Wakati utasikia ma kengele ya Siku Kuu ya Kulala Mzazi-Mungu utanikumbuka na mimi.

usiku ya Shangilio ya Mama Maria na huyu, pamoja na watawa wengine aliimba wimbo ya Siku Kuu. Ku mwisho ya Liturgia alipewa Mwili na Damu ya Kristu mara ya mwisho.

Ilikuja Siku ya tarehe 15 Mwezi ya Mnane. Muzee Zosefu aliikaa mu lupago ya nyumba yake. Aliongojea saa.. .  Siku inapita.. .  Jua inaanza kuanguka. Aliita mtoto ya roho yake padri Efremi:

-Mtoto wangu, juu ya nini Mungu anachelewa akuje na nibebe?  Jua aliisha kupanda mbinguni na mimi niko tena huku?

-Ee Muzee, usisikitike, sasa tutafanya sala na utaondoka.

Alipata utulivu kidogo. Machozi yake ilisimamishwa. Kisha alisema kwa padri Efremi:

-Ita wapadi wote kuomba hurumia ya mimi na mimi nitawahurumia na hawa kuhurumia mimi, kwa sababu saa ya ondoko yangu ilikuja.

Wandugu waliomba hurumia na walipika magoti mbele yake mara ya mwisho

Kisha huyu alinyanyua ya ma dadika wa wili ma macho yake mbinguni. Kisha alisema na akili safi kwao:

-Iliisha sasa uzima yangu. Ninaondoka.. .  Munibariki!

Vile alisema na alinamisha kichwa yake pa fasi ya kuhume. Alifungula na alifunga mara mbili-tatu kinywa yake, kisha alitoa nafsi yake kwa mikono ya Mungu, aliyemupenda sana mu uzima  yake na alimutumikia bila muchoko.

## **Padri na mutawa Tikhoni wa jangwa ya Kilima Takatifu**

Padri na mutawa ya jangwa ya  Kilima  Takatifu alifurahi kweli kwani ilikuja mwisho wake wa heri.

Huyu mumoja alifugula kaburi yake na mikono yake. Pa bulongo aliweka posholo moja na alisema kwa mtoto ya roho yake kutupa bulongo ndani kisha maziko yake.

Alijua mbele ya masiku filani ya kama atakufa. Joo vile alisemaka kwa watawa wengine:

Mimi papa Tikhoni ninakufa. Mufanye sala juu ya yangu.

Musiseme ya kama mimi papa Tikhoni niko mtu muzuri.. .  Paka Mungu hile siku ya Uhukumu wa matata atasema kama mimi niko muzuri.. .

tena aliandika na ma barua juu ya kutuma mtoto ya roho yake, mutawa Paisios, kisha lufu yake. Alituma na barua na kwa patriarkhi ya inchi Rusia na kwa wakubwa ingine ya inchi yake Rusia. Aliandika hivi kwa patriarki na wapadri wengine:  «Mimi rafiki yako nilikufa siku.. . . . . . . .  ninakuomba andika sala moja juu ya pumziko yangu».

Mara mingi watawa wengien kila mwaka wlaiumuuliza:

-Ee Muzee Tikhoni tutakata kuni yako juu ya wakati ya baridi hii mwaka?

-Mutakata kuni,  kama mimi  misitakufe. Kama nitakufa haipashwe kukata kuni.

Siku moja aliita mtoto ya roho yake padri Paisios na alimuwaambia:

-Mimi papa Tikhoni, kama Mungu anapenda, kisha juma moja nitaenda Kwake..

Siku moja aliingia ndani ya nyumba ya padri Tikhoni na alimuona kutafuta kintu kimoja. Alimuuliza:

-Ee, Muzee, unatafuta ninyi?

-Eee, eko wapi Mtakatifu kamili Mzazi-Mungu Maria, Mtakatifu Sergios, mt. Serafim.. . ?

Alikamata nguo mweushi ya mutawa, mtoto wake, Paisios na alimuuliza:

-Weye uko mt. Sergios?

-Hapana, Muzee, mimi ni Paisios.

Alipumzika kidogo Muzee na kisha padri paisios alimuuliza:

Ee, Muzee, Mzazi-Mungu Maria alikuwaambia ninyi?

-Aliniambia ya kama, kisha ma siku wa wili ya Siku Kuu ya kuzaliwa Yake, mu tarehe 8 Mwezi ya Tisa (Septembrie), nikusema mu 10-9-1968 atanibeba mbinguni. Na kwel;i ghile siku alipewa Mwili na Damu ya Kristu na katika uso wa mwangaza mingi, alifanya alama ya msalaba na alipumzika musingizi wa milele.

Kiliyo yake ilifanyika na furaha mingi. Pa Msalaba ya kaburi yake huyu padri Tikhoni aliandika hii mandiko: « Mimi mwenye zambi Tikhoni, mpadri na mutawa. Hapa mu Kilima Takatifu, niliishi miaka 60. Utukufu kwako, ee Mungu wangu».

## Padri arhim. Amfilokhios Makris

Padri mkubwa ya roho na mujengaji ya monasteri Habari Njema ya Mama wa Bwana Yesu Kristu mupendwa wetu mu Kisanga Patmos ya Grekia, padri Amfilokhios Makris (1889-1970) alifika mu uzee murefu. Lakini mapendo yake juu ya uzima utawa ilibakia umoja mpaka mwisho yake!

Mu Juma moja, mukongo ya Siku Kuu ya Matawi mu mwaka 1970 kati ya muchana aliikaa pa kiti yake na alipaza sauti kusema:

Tulikuja na tulitoka mu Yerusalema wa juu! Dada Mutawa Agathi ita mama mkubwa na watawa wanawake wote.

Aliisha kubeba tangazo kutoka mbinguni! Waliomba hurumia na kila dada alibusu mukono na aliomba baraka yake. Alikuwa pa kitanda yake ma siku kidogo, lakini hasikusimame kuwafundisha hivi:

-Munapashwa kuwa watoto ya mapendo! . Musiogope shetani.. . Misina na furaha na matakio ingine paka nimiona ndani ya paradizo yote mweye! Mungu ninatakia amiingisha mu utukufu mwake. Nikona furaha mingi, kwa sababu niko na karibu yangu watoto wa roho wangu wote.. . Hakuna namna kuitwa mtu moja mukristu kama hana na mapendo ndani ya roho yake. Muishi na maungano katikati yenu. Kristu ninamitakia aikae ndani ya ma roho yenu ma siku zote.. . Mumuombe kwa Mungu anihurumie, kwani nilikuwa baba wenu maskini na misikuweze kumipatia hata kintu kimoja kizuri.. .

Mama mkubwa yao alimujibu:

-Muzee wetu, weye ulitupa kila kintu mu uzima yetu.

Hile saa mama mkubwa alisimama ya kupika magoti mbele yake, padri mkubwa alimwaambia:

-Mungu amipatie nguvu Yake juu ya kuongeza muzuri kundi ya watawa wanawake wenu. Ninataka kufata mweye ma shauria yangu. Nitafuraha mbinguni, kama munafata ma sheria ya uzima utawa.. . Mungu ninatakia atustahili sisi wote kuishi mu utukufu ya Paradizo.. .

Saa ya mapenzi takaitfu ya Mungu ilifika: 16 Mwezi ya mnane 1970! Siku mu kazi inee, saa 2, 15 kisha kati ya muchana alitoa nafsi yake kwa mikono ya Yesu Mupendwa wake.

Uso yake ilijaza na amani na upole. Taabu ilikuwa uzito, lakini ndani ya ma roho ya watu ilikuwa furaha moja ya kama padri mkubwa yao aliisha ku ingia Paradizoni!

## Mama Despina mupenda wanadamu

Mama Despina alikuwa mfano moja muzuri sana katikati ya waaminifu wote mu muji Seres ya inchi Grekia. Alizala watoto wa wili wanaume na mudogo mtoto alifata uzima utawa mu Kilima Takatifu mu monasteri ya Mt. Grigorio, jina lake padri Nikitas. Huyu mama alipenda sana wamaskini. Aliacha kila wakati ma kazi ya nyumba yake na aliendа kusaidia wamaskini. Alikuwa na ruhusa ya bwana wake. Alienda kusafisha ya wayttoto waenye yatima, kusafisha wazee, kuwapatia chakula. karibu ya watu wamaskini alipitisha ma saa mengi ya uzima yake kila siku. Kisha lufu yake, kama kwa mfanao alionekana mama moja mwingine na alisaidia na namna umoja wazee na wamaskini, wale waliummuliza: Weye uko mama Despina?

Ku mwaka 1971 alifanya mahamakia mu obitalo na waganga walisema ya kama kancer iliharabisha matumbo yake yote.

Huyu mama alisikia ya kama atakufa. Alifanya hii sala mbele ya Mungu:

-Ninakushukuru, Kristu wangu, kwani ulinitembelea mbio mbio, mu kipimo yangu miaka 41! Ninakuomba sasa, unipe nguvu yako juu ya kuvumilia mpaka mwisho ya uzima yangu.

Mu tarehe 30, Muposho ya Mwezi ya kumi 1971, alisema kwa bwana na watoto wake na kwa mama ma dada na ma jirani yake wengine:

Hii magaribi nitakufa! Musienda ma fasi ingine. paka mutayarisha nyumba yetu kwa sababu watakuja waaminifu na kesho mutafanya maziko yangu.

Ya masiku makumi mbili, asikuweze kukula hata kidogo. Pakas alikunywa chai kidogo. Wa ndugu wote walilia, lakini huyu mama alisimama bila woga na aliwatulivu wa ndugu wengine. Aliwaambia: Juu ya kutoka mbio, muanza kusoma ma zaburi ya Nabii Daudi.

Watoto wake walianza kusoma. Huyu alilamuka ya kitanda yake na alisimama. Bwana wake na ma dada walimwaambia kularia pa kitanda yake. Huyu aliwaambia:

-Ni zambi kusikia Zaburi na nitaikaa pa kitanda. Inapaswa kusimama pa miguu yangu. Na huyu pamoja na watoto wake alisoma bila kuona na ma zaburi filani.

Kisha somo ya ma zaburi yote alimushaurtia mama yake ambakie nyumbani yake juu ya kusaidia watoto wa yatima yake. Kisha aliita bwana yake na alimwaambia:

-Kisha lufu yangu, kwa sababu uko kijana, utaowa bibi mwingine. Watoto wetu weko wanaume. Mweye mukona lazima ya mwanamuke moja katikati yenu juu ya kumisaidia. Joo vile weye inapaswa kuoa mbio. Usisikie watu ya dunia. Weye angalia kazi na nyumba yako.

Kisha mama Despina alitosha pete ya kilole yake na alimupatia kwa bwana wake mukusema hivi:

-Tangu sasa weye uko muhuru ya mimi..

Bwana yake alikamata pete na aliiweka mara ingine mu kilole yake mukusema kwake ya kama hasitakufe. Lakini bibi yake alijua jambo nini itafata. Tena, kisha lufu yake watoto wake walipata pete ndani ya kitambaa moja kuifungwa, chini ya kintu ya kichwa yake.

Alitengeneza ma nguo yote yake, aliomba hurumia na kisha alipinduka kuangalia Picha ya Bwana Yesu Kristu. Alimusema hivi:

-Sasa, Kristu wangu, niko tayari! Kuja kunibeba!

Mara moja alimubamba kikohozi moja, bila kivukutu. Dada yake alienda amuletee maji, lakini mama Despina amuwaambia:

-Hailazimishwa! Hii haina kikohozi. Ni pumuzi ya mwisho ya uzima yangu. Kisha saa kidogo ninaondoka.

Kisha bwana wake alimukamata kichwa yake juu ya hapana kuteswa na bibi yake alipumuzi mara tano-sita na alitoa nafsi yake kwa mikono ya bwana yake.

Vile katika amani na mapendo mbele ya watu wote aliishi mama Despina na aliondoka kwa Mungu na kipimo yake miaka 41. Alienda Kwake, kwa sababu hapa alimupenda kabisa ya vitu vingine vyote vya hii dunia.


**Ufasiri kutoka lugha kigreki mu lugha kiswahili mu**

**MONASTERRI YA MT. GRIGORIO**
**KILIMA TAKATIFU**
**GREKIA**
**2000**